

**NJEO, HALI NA DHAMIRA KATIKA KITENZI CHA KITIKUU: MTAZAMO WA
UMINIMALISTI**


RUKIYA HARITH SWALEH

**Tasnifu imewasilishwa katika kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamifu
ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Pwani**

JULAI, 2017


UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu na kwa maoni yangu haijawahi kutolewa katika mahitaji ya kutosheleza shahada katika chuo kingine chochote. Ni tasnifu ya kutimiza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Pwani.


08.11.2017 C82/PU/2095/11

RUKIYA HARITH SWALEH
TAREHE
NAMBARI YA USAJILI

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii:


PROF. YAKOBO MUTITI (MSIMAMIZI)
08.11.2017
TAREHE

DR. HELGA SCHROEDER (MSIMAMIZI)
8.11.2017
TAREHE

TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa:

Harith Swaleh na Aisha Turuba.

Pamoja na familia yangu; mume wangu Ismail Barrow na
watoto wangu, Ismat, Muhammad na Amina

SHUKRANI

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wasimamizi wangu kwa msaada wao wa dhati, Prof. Yakobo Mutiti na Dr. Helga Schroeder. Shukrani zangu kwa Marehemu Prof. Karisa Beja, ambaye alikuwa msimamizi wangu, Mungu aiweke roho yake peponi. Siwezi pia kumsahau Prof. Deo Ngonyani wa Chuo Kikuu cha Michigan State, kwa kunisaidia na kuniongoza, alipokuwa likizoni katika Chuo Kikuu cha Pwani. Mkuu wa Idara, Dr. Catherine Mwangi, nakushukuru kwa kunihimiza nimalize kazi yangu, na wenzangu wote tunaofanya kazi pamoja katika Chuo cha Pwani kwa kunihimiza na kunitakia mazuri katika kazi yangu.

Napenda pia kutoa shukrani zangu kwa wale walionisaidia nilipokuwa nakusanya data yangu, hasa kwa ndugu yangu, Khadija Harith, ambaye kila nikikwama alinisaidia. Shukrani zangu za dhati kwa wazazi wangu, hasa babangu aliyekuwa akinishajiisha ili nimalize shahada yangu. Namshukuru sana mume wangu ambaye kila mara alinifariji na kutaka nitamatishe kazi yangu. Siwezi kuwasahau watoto wangu, ambao kila nikijifungia kufanya kazi walinielewa bila kunisumbua.

IKISIRI

Tasnifu hii inahusu uchanganuzi wa kiufafanuzi wa kimofosintaksia wa njeo, hali na dhamira katika kitenzi cha Kitikuu. Njeo, hali na dhamira ni kategoria za kisarufi zinazopatikana katika kitenzi. Kitikuu ni lahaja mojawapo kati ya lahaja za Kiswahili. Kitenzi cha Kitikuu kina uwezo wa kubeba mofimu anuwai zenyenye uamilifu wa aina mbalimbali. Kati ya mofimu zinazopatikana katika kitenzi cha Kitikuu ni mofimu za njeo, hali na dhamira. Njeo ni kategoria ya kisarufi inayohusu uhusiano wa kiwakati wa kutendeka kwa tendo hasa kwa kurejelea wakati wa sasa. Hali nayo huangalia jinsi kitendo husika kinavyotendeka na wakati na kueleza kutimilika au kutotimilika kwa kitendo hicho. Nayo dhamira huonyesha nia au lengo la msemaji kama ni kuarifu, kuamuru, kusihii na kadhalika.

Madhumuni ya utafiti huu ni kuelezea na kuainisha njeo, hali na dhamira katika lahaja ya Kitikuu na kuonyesha muingiliano wake katika lahaja hii. Nadharia ya Uminimalisti imetumika kuonyesha jinsi ukaguzi wa sifa unavyofanya kazi kwa vipashio hivyo vya njeo, hali na dhamira. Sentensi anuwai zenyenye kutumia mofimu hizo zimeonyeshwa na mifano ya uchanganuzi ya baadhi za sentensi, kwa kutumia nadharia ya Uminimalisti. Kulingana na Uminimalisti mofimu za njeo, hali na dhamira hupachikwa katika kitenzi kupitia mchakato wa kimkokotoo. Leksika za vitenzi na nomino hupewa mofimu zao katika leksikoni. Numerali huchagua sifa za kimofosintaksia za lugha fulani, baadaye muungano hutokea kwa kuunganisha chembechembe mbalimbali za lugha na kuunda maneno, virai na sentensi, hivyo kuunda miundo. Usogezi hutokea panapokuwa na haja, kwani usogezi huchochewa na haja za kimofosintaksia. Kitikuu kwa sababu ni lugha ambishi bainishi yenye ukwasi wa mofolojia, huruhusu usogezi ili kukagua sifa za uzalishaji kuhakikisha ukubaliano na mahali pa kisintaksia katika sentensi. Mofimu za njeo, hali na dhamira katika kitenzi cha Kitikuu hukaguliwa katika sehemu

mbalimbali kuangazia ukubaliano wa kisarufi ili zisionekane katika umbo la kifonetiki (UF).

Data juu ya njeo, hali na dhamira ilikusanywa kutoka maeneo ya Kizingitini, Tchundwa na Rasini, kwa watu wasiopungua umri baina ya miaka 45 hadi 70. Mtafiti pia alitumia umilisi wake alionao kuhusu lahaja hii ya Kitikuu, kama data msingi. Data ya ziada ni ya kutoka maktabani, ambapo upekuzi wa maktabani ulifanywa kuhusu lahaja ya Kitikuu, nadharia ya Uminimalisti na sarufi ya Kiswahili Sanifu.

Kitikuu kina njeo mbili kuu: njeo iliyopita **{li}** na njeo ijayo **{ta}**. Kitikuu, kwa nadra hutumia njeo iliyopo **{a}** hasa katika vitenzi visaidizi. Kwa upande wa hali imegawanywa katika hali timilifu na hali isiyo timilifu. Hali timilifu hutumia mofimu **{ndo}** na **{ie}**. Hali isotimilifu hugawika katika hali mbalimbali kama hali ya mazoea **{hu}**, hali ya mfululizo **{ka}** na hali ya kuendelea **{hu}** na **{ki}**. Kuna dhamira mbalimbali zinazoonyeshwa kwa mofimu za kiishio **{a}** na **{e}** na dhamira za masharti zikionyeshwa kwa mofimu **{ki}** na **{ngali}**.

ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA

| | | |
|-------------------|---|--------------------------------|
| a | - | Athari ya kile kilichohamishwa |
| AN | - | Kauli ya kutendana |
| ak | - | Athari Kiima. |
| at | - | Athari Kitenzi |
| ay | - | Athari yambwa. |
| at _{kuu} | - | Athari ya kitenzi kikuu |
| at _s | - | Athari ya kitenzi kisaidizi |
| B | - | Bainishi |
| DHAM | - | Dhamira |
| E | - | Kielezi |
| Fok | - | Fokasi |
| H | - | Kihuishi |
| HAL | - | Hali |
| IA | - | Kauli ya kutendea |
| IW | - | Kauli ya kutendewa |
| ESH | - | Kauli ya kutendesha |
| J | - | Jirejea- hali ya kujirejelea |
| KAN | - | Ukanusho |
| KB | - | Kirai bainishi |
| KE | - | Kirai elezi |
| KH | - | Kirai Kihuishi |
| Kiamb.yambwa- | | Kiambishi cha yambwa |
| KIJ | - | Kijalizo |
| KN | - | Kirai Nomino |

| | | |
|------------------|---|-----------------------------|
| KR | - | Kirai rejeshi. |
| KT | - | Kirai Tenzi |
| KU | - | Kitenzi Kisoukomo |
| KUPk | - | Kirai upatanishi kiima |
| KUPy | - | Kirai cha upatanisho Yambwa |
| KV | - | Kirai Kivumishi |
| KU | - | Kitenzi kisoukomo |
| N | - | Nomino |
| NJ | - | Njeo |
| nk | - | Na kadhalika |
| O | - | Kionyeshi |
| R | - | Rejeshi |
| RE | - | Urejelezi wa mtenda |
| SB | - | Sarufi bia |
| SPES | - | Spesifaya |
| SWAL | - | Swali |
| SZGM | - | Sarufi Zalishi Geuza Maumbo |
| T | - | Kitenzi |
| T _{kuu} | - | Kitenzi kikuu |
| T _s | - | Kitenzi kisaidizi |
| TEW | - | Mofimu ya yambwa tendwa |
| U | - | Kiunganishi |
| UF | - | Umbo Fonetiki |
| UM | - | Umilikifu na Masharti |
| UP | - | Upatanisho |

| | | |
|-----|---|---------------------|
| UPk | - | Upatanisho Kiima |
| UPy | - | Upatanisho Yambwa |
| US | - | Umbo Mantiki |
| W | - | Kauli ya kutendwa |
| V | - | Kivumishi |
| Y | - | Yambwa |
| * | - | Si sawa |
| { } | - | Mipaka ya mofimu |
| ' | - | Alama ya mpumuo |
| → | - | Inabadilika na kuwa |

ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA

Alomofu (Allomorph) – Ni maumbo tofauti ya mofimu.

Kanuni na Vigezo (Principles and Parameters) - Kanuni kwa maana ya zile sheria za lugha zote zinazofanana na Vigezo kwa maana ya zile sheria ambazo ni za lugha mahsusini.

Kanuni ya Kuchelewesha (Principle of Procrastinate) – Huelezea kuwa usogezi hutokea tu pale panapokuwa na haja na kukubaliwa na sheria za kimofosintaksia au kileksika katika lugha husika.

Kanuni ya Ubinafsi - (Greed Principle) – Huelezea kuwa viambajengo havisogezwi kutimiza lengo la viambajengo vingine, bali husababishwa na sababu za kibinafsi kutimiza haja ya kiambajengo kinachosogezwa.

Kanuni ya Ufafanuzi wa Kina (Principle of Full Interpretation) – Ni kanuni inayosema kuwa kiwakilishi cha habari fulani lazima iwe tu na elememnti zote zinazochangia moja kwa moja katika ufanuzi wa kiwango husika.

Kanuni ya Usogezi mfupi zaidi (Principle of relativised Minimality) - Huelezea kuwa viambajengo husogezwa mahali karibu zaidi na panapostahili.

Kanuni za Iktisadi (Principle of Economy) - Hujumuisha sheria mbalimbali ambazo huonyesha ule uchache au uchumi wa mambo fulani kufanyika, nazo ni Usogezi mfupi zaidi, kuchelewesha na Ubinafsi.

Kiambajengo/Elementi (Element) – Neno linalitumiwa kumaanisha sehemu ya kitu, katika isimu.

Kizinga sifa (Isogloss) - Mpaka unaolizungusha eneo ambalo lina sifa maalum za matamshi, sarufi au msamiati katika ramani ya kiisimu.

Lugha Dhaifu (Weak language) – Ni lugha ambazo ni tenganishi, hazina sifa za kimofosintaksia.

Lugha Imara (Strong language) – Ni lugha zenyе sifa za kimofosintaksia, lugha ambishi bainishi.

Mdhihiriko Wazi (Spell-out) Hapa ni sehemu katika mfanyiko wa kimkokotoo ambapo sifa za kifonolojia na kisemantiki zinadhirishwa katika sehemu mbili za kisarufi, umbo fonetiki (UF) na umbo mantiki (US) mtawalia.

Mfanyiko wa Kimkokotoo (Computational Process) – Ni mchakato unaohusisha hatua zote zinazohusika katika uundaji miundo hadi kufikia mjumuiko.

Mofimu (Morpheme) – Ni kipashio kidogo cha kisarufi chenye maana.

Mofu (Morph) – Ni kiwakilishi cha kifonolojia cha mofimu.

Msikiko (Prominence) – Hali itokeayo ambapo lugha fulani hutumia kwa kiwango kikubwa zaidi njeo au hali au dhamira katika matumizi yake.

Muungano (Merge) – Huunganisha viambajengo (elementi) mbalimbali ili kuunda maneno, virai ili kuunda miundo.

Numerali / Hisabati (Numeral) - Huhusika na kuchagua leksika na sifa za kimofosintaksia ya lugha husika.

Umbo Fonetiki (Phonetic Form) – Huhusisha zile habari zinazotoa sifa za kifonolojia , za kimatamshi.

Umbo Mantiki (Logical Form) – Ni zile habari zinazohusika katika kuamua sifa za kisemantiki, za maana.

Usogezi (Movement) - Kusogeza hutokea kwa sababu ya kukagua sifa dhahania za uzalishaji ambazo hukaguliwa kuhakikisha usahihi wake dhidi ya mahali pa kisintaksia katika muundo wa sentensi.

Umilikifu na Masharti (UM) (Government and binding) (GB) – Ni nadharia ya sintaksia iliyօasisiwa na Chomsky miaka ya themanini (1980). Ni nadharia ambayo ilikuwa imeleta mabadiliko makubwa tofauti na nadharia za mbeleni za Geuza Maumbo

na Sarufi Zalishi. Nadharia ya UM ilikuwa na vijinadharia vingi ndani yake na ndiyo mageuzi yakafanywa na kuibuka na Nadharia ya Uminimalisti, ambayo ilirahisisha kwa kupunguza nadharia nyingi za utata za UM .

Usonde (Deixis) – Sifa ya lugha ambapo hurejelea katika muktadha wa muda wa usemaji/uneni.

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|--|----|
| Jedwali 1 Jedwali la Konsonanti | 9 |
| Jedwali 2 Jedwali la Mnukuu wa Konsonanti za Kitikuu | 11 |
| Jedwali 3 Ngeli kwa Mkabala wa Kimofolojia..... | 12 |
| Jedwali 4 Ngeli kwa Mkabala wa Kisintaksia..... | 14 |
| Jedwali 5 Viambishi vya Upatanishi vya Ngeli | 48 |
| Jedwali 6 Kiambishi Si- cha Ukanushi..... | 50 |
| Jedwali 7 Viambishi vya Urejeshi katika Kitikuu..... | 56 |
| Jedwali 8 Viambishi vya Yambwa Tendwa na Tendewa..... | 58 |
| Jedwali 9 Muundo wa mzizi wa kitenzi | 61 |

YALIYOMO

| | |
|---|------|
| UNGAMO | ii |
| TABARUKU | iii |
| SHUKRANI | iv |
| IKISIRI | v |
| ORODHA YA VIFUPISHO NA ISHARA | vii |
| ISTILAHU MUHIMU ZILIZOTUMIKA | ix |
| ORODHA YA MAJEDWALLI | xii |
| YALIYOMO | xiii |
| SURA YA KWANZA: UTANGULIZI | 1 |
| 1.0 Kitangulizi | 1 |
| 1.1 Usuli wa Mada | 1 |
| 1.2 Swala la Utafiti | 3 |
| 1.3 Madhumuni / Malengo ya Utafiti | 4 |
| 1.4 Maswali ya Utafiti | 5 |
| 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti | 5 |
| 1.6 Natija ya Utafiti | 5 |
| 1.7 Sarufi ya Kitikuu | 6 |
| 1.7.1 Njeo, Hali na Dhamira | 7 |
| 1.7.2 Fonolojia ya Kitikuu | 9 |
| 1.7.3 Ngeli za Kitikuu | 11 |
| 1.8 Hitimisho | 14 |
| SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA | 15 |

| | |
|---|-----------|
| 2.0 Kitangulizi | 15 |
| 2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Sarufi ya Kiswahili na Kitikuu | 15 |
| 2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia..... | 19 |
| 2.3 Msingi wa Nadharia..... | 22 |
| 2.3.2 Mifanyiko ya Kimkokotoo..... | 24 |
| 2.3.3 Kanuni ya Ukaguzi wa Sifa katika Uminimalisti..... | 28 |
| 2.4 Hitimisho | 31 |
| SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI..... | 32 |
| 3.0 Kitangulizi | 32 |
| 3.1 Ukusanyaji wa data | 32 |
| 3.2 Utaratibu wa utafiti | 32 |
| 3.2.1 Uteuzi wa sampuli..... | 33 |
| 3.2.2 Mbinu za kukusanya data..... | 34 |
| 3.3 Uchanganuzi wa data | 34 |
| 3.3.1 Uwasilishaji wa Data | 35 |
| 3.4 Hitimisho | 35 |
| SURA YA NNE: KITENZI NA MOFOLOJIA YAKE | 36 |
| 4.0 Kitangulizi | 36 |
| 4.1 Sarufi ya Kitenzi | 36 |
| 4.2 Aina za Vitenzi | 37 |
| 4.2.1 Vitenzi Vikuu | 37 |
| 4.2.2 Vitenzi Visoukomo | 40 |
| 4.2.3 Vitenzi Vishirikishi | 42 |
| 4.2.4 Vitenzi Visaidizi | 43 |
| 4.3 Mpangilio wa Maneno | 44 |

| | |
|--|-----------|
| 4.4 Mofolojia ya Kitenzi cha Kitikuu | 45 |
| 4.4.1 Viambishi awali vya kitenzi..... | 45 |
| 4.4.1.1 Viambishi vya upatanishi au mofimu za upatanishi | 46 |
| 4.4.2 Mzizi wa Kitenzi..... | 61 |
| 4.4.3 Viambishi Tamati..... | 62 |
| 4.5 Hitimisho | 81 |
| SURA YA TANO: UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA | 83 |
| 5.0 Kitangulizi | 83 |
| 5.1 Njeo..... | 83 |
| 5.1.1 Njeo na Wakati..... | 85 |
| 5.1.2 Njeo katika Kitikuu | 85 |
| 5.1.2.1 Njeo Iliyopo..... | 88 |
| 5.1.2.2 Njeo Iliyopita..... | 94 |
| 5.1.2.3 Njeo Ijayo..... | 96 |
| 5.2 Hali | 96 |
| 5.2.1 Hali katika Kitikuu..... | 97 |
| 5.2.1.1 Hali Timilifu..... | 100 |
| 5.2.2 Hali Isotimilifu | 109 |
| 5.2.2.1 Hali ya Mazoea..... | 112 |
| 5.2.2.2 Hali ya Mazoea / Kuendelea..... | 113 |
| 5.2.3 Hali ya Mfululizo | 122 |
| 5.3 Dhamira | 125 |
| 5.3.1 Dhamira Arifu | 126 |
| 5.3.2 Dhamira Ulizi..... | 129 |
| 5.3.3 Dhamira Agizi | 131 |

| | |
|---|-----|
| 5.3.4 Dhamira Tegemezi | 138 |
| 5.4 Muingiliano wa Njeo, Hali na Dhamira katika Sentensi Ambatano | 161 |
| 5.4.1 Mofimu {-ta-} katika sentensi ambatano | 162 |
| 5.4.2 Mofimu {-li-} katika sentensi ambatano..... | 164 |
| 5.4.3 Mofimu {-ndo-} | 166 |
| 5.4.4 Mofimu {ki}..... | 168 |
| 5.4.5 Mofimu { hu-} | 171 |
| 5.4.6 Mofimu {ngali}..... | 174 |
| 5.5 Hitimisho | 178 |
| SURA YA SITA: MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO | 179 |
| 6.0 Kitangulizi | 179 |
| 6.1 Matokeo..... | 179 |
| 6.2 Hitimisho | 193 |
| 6.3 Mapendekezo..... | 186 |
| Marejeleo..... | 188 |
| KIAMBATISHO A : Idhini ya kimaadili ya kufanya utafiti | 193 |
| KIAMBATISHO B : Hojaji 1 | 194 |
| KIAMBATISHO C : Hojaji 2 | 197 |

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Kitangulizi

Sura hii inaangazia usuli wa mada hasa kwa kuelezea kuhusu lahaja ya Kitikuu. Swala la utafiti ambalo ndilo swala linalofanya kuwepo kwa utafiti huu limeelezewa, kwani bila swala la utafiti hakuna utafiti. Madhumuni ya utafiti ambayo ndiyo malengo ya kufanya utafiti huu yameelezwa. Upeo na mipaka ya utafiti, na natija ya utafiti yameelezwa vilevile. Kwa kifupi, sarufi ya Kitikuu imeelezewa mwishoni, kwa kuangazia fonolojia na ngeli za Kitikuu. Maelezo kwa ufupi juu ya dhana za njeo, hali na dhamira yametolewa.

1.1 Usuli wa Mada

Kiswahili ni lugha yenye lahaja nyingi zinazoanzia Kismayu nchini Somalia, Kenya, Tanzania hadi Msumbiji na Zaire. Wataalam mbalimbali wametofautiana kuhusu idadi kamili ya lahaja za Kiswahili. Kwa mfafo, Chiraghdin na Mnyapala (1978:25) wanasema ni zaidi ya kumi na tano, Myachina (1981:2) anasema ni kama lahaja 20 na Mohlig (1985:43-44) anataja 21. Kwa maoni yangu Kiswahili kina lahaja 20 ambazo ni: Chimiini, Kiamu, Kitikuu, Kisiu, Kipate, Kimvita, Kijomvu, Kivumba, Chichifundi, Kipemba, Kiunguja, Kimtang'ata (Kimrima), Kingare, Kimgao, Kimakunduchi, Kitumbatu, Kihadimu, Kingazija, Kimwani na Kingwana.

Lahaja za Kiswahili zimegawanywa katika makundi tofauti tofauti. Nurse (1982) anasema kuwa, njia mwafaka zaidi ya kugawanya lahaja hizi ni kwa kipengee cha kizinga sifa. Tofauti za lahaja zinaweza kuwa za kifonolojia, kimsamiati au kimofolojia. Nurse amezigawanya lahaja hizo katika makundi mawili makuu: Lahaja za kusini na lahaja za kaskazini mwa upwa wa Afrika Mashariki. Lahaja za kaskazini ni Chimiini (nchini Somalia), Kitikuu, Kisiu, Kipate na Kiamu (nchini Kenya), Lahaja za kusini ni

pamoja na Kivumba (Kenya), Kimtang'ata, Kipemba, Kitumbatu, Kihadimu na Kimakunduchi (nchini Tanzania). Lahaja za Kimvita, Kijomvu (nchini Kenya), Kingare, Chichifundi (nchini Kenya) na Kiunguja (nchini Tanzania), ameziweka kando kwani anasema lahaja hizi zinachanganya sifa za lahaja za kaskazini na kusini.

Kitikuu kinazungumzwa kusini mwa nchi ya Somalia na visiwa vilivyoko kaskazini mwa Lamu nchini Kenya kama Kiunga, Shanga, Ndau, Kiwayuu, Kizingitini, Mbwajumwali, Myabogi, Tchundwa na Rasini (Faza). ‘Tikuu’ ni neno linalomaanisha ‘nchi kuu’ na watu wanaitwa Watikuu, kumaanisha ‘watu wa nchi kuu’ na lugha yao ni Kitikuu. Japo Watikuu wote katika visiwa hivi huzungumza Kitikuu, kuna tofauti ndogo ndogo za kimatamshi zinazopatikana. Watikuu wanajulikana kwa majina mengine kama Wabajun na Wagunya, lakini jina linalofaa na kupendwa zaidi ni Tikuu, kwani Gunya linahusisha Watikuu wa zamani zaidi waliohama na kuathiriwa na lahaja nyingine mbalimbali za Kiswahili (Nurse na Hinnebusch, 1993). Na neno ‘Bajun’ lilizuka tu karibuni baada ya Kenya kupata uhuru. Kitikuu ni lahaja ambayo haina athari kubwa ya maneno ya kigeni kama zilivyo lahaja nyinginez. Kimejaribu kwa kiasi kikubwa, kuhifadhi misamiati na sarufi yake, kama anavyosema, Myachina (1981:2) kuwa; ‘Lahaja ya Kitikuu ni lahaja yenye mfuatano wa sifa za kipekee katika sarufi na misamiati yake’.

Nurse na Hinnebusch (1993) pia wamezungumzia lahaja hii na wakasema ‘kati ya lahaja nne za kaskazini (Amu, Tikuu, Siyu na Pate), Tikuu ndiyo kiisimu tofauti kabisa, kwa vile iko mwishoni mwa kaskazini na imejitenga, ndiyo imefanya ibakishe misamiati ya zamani sana’.

Guthrie (1971) alipanga lugha mbalimbali zilizotokana na mamelugha ya Kibantu kulingana na mashina yake. Tunapata kuwa, kati ya lahaja za Kiswahili, Kitikuu kina misamiati mingi ambayo hufanana sana na lugha za Wabantu wengine wa Kaskazini

Mashariki wanaopatikana Kenya, kama Wakikuyu, Wakamba, Wameru, Wapokomo, Wataita na Wamijikenda.

Kwa mfano maneno ya Kitikuu kama noni (ndege), munu (chumvi), isi (samaki), hondre (shamba), kijaa (kidole), igege (gego) na mengine mengi. Uhusiano huu uliopo baina ya Kitikuu na lugha nyingine za Kibantu za Afrika Mashariki pengine ni sababu tosha ya kuonyesha vile lahaja hii imeendeleza misamiati yake asilia pamoja na watu waliokuwa wametoka sehemu moja wakizungumza lugha moja. Kwa mintarafu hiyo basi, nikavutiwa katika kuifanyia utafiti lahaja hii ambayo ina ukwasi wa sifa za kipekee, kati ya lahaja nyingi za Kiswahili. Kuhusu idadi ya wazungumzaji wa Kitikuu, inakuwa shida kusema hasa ni wangapi, kwa sababu Watikuu wametapaka sehemu mbalimbali nchini Kenya na hata Tanzania. Makadirio yanayaofanywa nchini Kenya baada ya kila miaka kumi, haina sehemu inayoonyesha wazungumzi wa lahaja mbalimbali. Kwa upande wa Waswahili, wote wamerundikwa pamoja kama kabile la Waswahili. Kwa hivyo, inakuwa shida kusema kuna Watikuu wangapi, Waamu wangapi na Wajomvu wangapi nchini Kenya, kwani wote wamewekwa kama Waswahili.

1.2 Swala la Utafiti

Dhana za njeo hali na dhamira, zimekuwa na utata katika kuelezwu kwake, kwani kazi za Kiswahili zilizoandikwa kuhusu dhana hizo hazitoi bayana maana zake kama inavyotakikana. Dhana hizo zimekuwa zikichanganywa bila kuweza kuona tofauti iliyopo kati yazo. Kazi ya Mohammed (2001) kwa mfano, inaangazia viambishi vyote vya njeo, hali na dhamira kama viambishi vya njeo, anaziita sehemu ya kwanza ya njeo, sehemu ya pili ya njeo na sehemu ya tatu ya njeo. Kwa hakika sehemu ya pili ni ya hali na ya tatu ni ya dhamira. Mohammed anazirundika zote kama njeo. Dhana ya njeo nayo, inachanganywa pia na dhana ya wakati, hivyo kazi mbalimbali zinatumia wakati

(Mgullu, 1999) kama kisawe cha njeo, au neno nyakati linatumwiwa kama kisawe cha njeo (Waihiga, 1999). Kwa hivyo, tukisema vielezi vyta wakati kama jana, kesho, asubuhi, saa saba au jioni ina maana vielezi hivi ni njeo?

Utafiti huu unaweka bayana dhana za njeo, hali na dhamira kwa kuzieleza kwa kina na kuzionyesha kuwa ni vipashio vyta kisarufi vinavyoambishwa katika vitenzi. Kwa hivyo, ni tofauti na vielezi vyta wakati kama ‘jana, saa saba na jioni’.

Kazi zilizofanywa kuhusu sarufi ya Kitikuu haziangalii lahaja hii kwa misingi ya nadharia za kiisimu bali zimetoa maelezo ya kiisimu ya kijumla bila kuzamia kwa undani maswala hayo, ndiyo tukaonelea kuifanyia utafiti lahaja hii kimofosintaksia kwa misingi ya kanuni ya ukaguzi wa sifa chini ya mtazamo wa Uminimalisti. Kazi hizo hazijachunguza lahaja hii kwa mapana kiisimu kwani wanaangazia tu lahaja hii kihistoria au kiulinganishi na lahaja nyingine za Kiswahili au lugha nyingine za Kibantu kwa ujumla.. Kazi nyingi ambazo zimefanyiwa utafiti wa kiisimu ni za Kiswahili Sanifu. Kazi za lahaja mbalimbali za Kiswahili hazijafanyiwa utafiti wa kiisimu kama zinavyostahili.

Nurse na Hinnebusch (1993) kwa, mfano wamejaribu kufanya utafiti wa kiisimu lahaja ya Kitikuu kiulinganishi na kihistoria katika nyanja za fonolojia na mofolojia, lakini hawaziangalii kazi hizo kwa kina.

1.3 Madhumuni / Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo mahsus yafuatayo:

- i. Kubainisha viambishi vyta njeo vinavyopatikana katika vitenzi vyta Kitikuu.
- ii. Kuainisha viambishi vyta hali vinavyopatikana katika vitenzi vyta Kitikuu.
- iii. Kubainisha sentensi anuwai za Kitikuu kwa misingi ya dhamira katika vitenzi.
- iv. Kuchunguza jinsi kitenzi cha Kitikuu kinavyochanganuliwa katika misingi ya

Uminimalisti chini ya ukaguzi wa sifa

1.4 Maswali ya Utafiti

- i. Kwa kuwa Kitikuu ni lahaja ya Kiswahili, je kina viambishi vyta njeo na hali kama vyta ya Kiswahili Sanifu au ni tofauti?
- ii. Dhamira mbalimbali zinajidhihirishaje katika sentensi za Kitikuu?
- iii. Nadharia ya Uminimalisti hasa kuitia ukaguzi wa sifa inafanya kazi VIPI katika kirai tenzi cha Kitikuu?

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kazi hii inashughulikia kirai tenzi cha Kitikuu zaidi kwa kuangazia njeo, hali na dhamira zinazopatikana katika lahaja ya Kitikuu. Hii si kazi ya kiulinganishi na Kiswahili Sanifu, lakini fasiri zake kwa Kiswahili Sanifu zinatolewa ili kueleweka vyema.

Kazi hii inashughulikia mofosintaksia kwa sababu ya kuonyesha vili njeo, hali na dhamira mbalimbali zinavyotumika katika sentensi za Kitikuu. Vipashio hivyo vyote vinapatikana katika mofolojia ya kitenzi, na kitenzi ni mlingoti wa kati katika mpangilio wa sintaksia. Kazi hii inaangazia zaidi mofosintaksia na kwamba haitajishughulisha sana na maana, dhima au matumizi ya njeo, hali na dhamira. Mofosintaksia zenye kubeba mofimmo za njeo, hali na dhamira katika sentensi za Kitikuu ndizo zinazoshughulikiwa katika kazi hii na sio maana wala dhima zao katika sentensi.

1.6 Natija ya Utafiti

Kazi nyingi za lahaja ya Kiswahili hazijapata fursa ya kushughulikiwa kwa kina kiisimu, Kitikuu kikiwa ni lahaja mojawapo. Lahaja hii isipofanyiwa utafiti na mambo

mbalimbali yakaandikwa, kuna uwezekano wa kusahauliwa au kuchanganywa na lahaja jirani kama Kimvita na Kiamu, kama anavyodai Hillewart (2011) katika kazi yake ya uzamifu na karatasi yake aliyoiwasilisha katika Kongamano la RISSEA, kwamba:

‘Kuna uwezekano wa vijana kuacha Kibajun na kutumia Kimvita au Kiswahili Sanifu kwa sababu mbalimbali kama vile kuhusishwa na watu walio nyuma kimaendeleo na sera ya serikali, hivyo uwezekano wa lahaja hii kupotea kabisa’ (2010:141-2).

Kazi za sarufi ya lahaja husaidia sana katika kuelewa zaidi sarufi ya lahaja iliyosanifishwa, kwani mambo ya kidayakronia yanapatikana katika lahaja. Kwa hivyo kazi za sarufi ya lahaja hutoa mwangaza katika kuelewa lahaja sanifu. Utafiti huu kwa hivyo, unatarajia kuifanya utafiti lahaja ya Kitikuu katika nyanja ya kimofosintaksia ili iwe hazina katika nyanja za usomi.

Dhana za kisarufi za njeo, hali na dhamira zina utata katika kazi zilizoandikwa za lugha ya Kiswahili. Kazi hii kwa hivyo imejaribu kuondoa utata huo kwa kuweka wazi maana na matumizi ya njeo, hali na dhamira. Utafiti huu unatarajia kuziba pengo hilo kwa kuweka bayana dhana hizo na kuzitofautisha ili zisichanganywe kama ilivyokuwa ikifanywa na wengi.

Utafiti huu unatumia nadharia ya Uminimalisti, ambayo kulingana na utafiti wangu haijashughulikiwa kwa lugha ya Kiswahili, katika kiwango cha uzamifu na hata kuchapishwa. Kazi nyingi zimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, kazi hii ni hazina kubwa kwa wanafunzi wa isimu wa uzamili na uzamifu.

1.7 Sarufi ya Kitikuu

Kazi hii zaidi inajikita katika kitenzi cha Kitikuu hasa kwa kuangazia kwa ufupi njeo hali na dhamira; kuna umuhimu vilevile kuangalia kwa ufupi fonolojia na mfumo wa ngeli wa lahaja ya Kitikuu.

1.7.1 Njeo, Hali na Dhamira

a) Njeo

Kazi za njeo, hali na dhamira mara nyingi huchanganywa na wataalam wengi na wanafunzi wa lugha.

Njeo, kulingana na Crystal (1991), inarejelea jinsi sarufi inavyoangalia tendo linalotendeka kwa kurejelea wakati kwenye kitenzi.

Naye Lyons (1968), anasema njeo inahusisha wakati wa kitendo kinapotendeka na kurejelea wakati wa usemi/kutamka (wakati wa kutamka ukiwa ni sasa). Hivyo njeo inaangaliwa ikiwa ni wakati uliopita, sasa na ujao.

Njeo, kwa hivyo ni wakati wa kutendeka kwa tendo ukihuishwa na wakati wa usemi. Wakati wa kutendeka kwa tendo unaangaziwa kwa muktadha wa sasa katika kitenzi, na ndipo tunapata njeo iliyopita, ya sasa na ijayo kwa kuhusisha na wakati wa sasa. Comrie (1985) na Lyons (1968) wameonyesha uhusiano huu kwa mchoro, tukichukulia kuwa wakati unawakilishwa kwa mstari kama ifuatavyo:

Kabla

Baada

Wakati wa usemi

(Lyons, 1968: 305 na Comrie, 1985:6)

Vitendo vinavyotendeka kabla ya wakati wa usemi ni njeo ya wakati uliopita, wakati wa usemi ni njeo iliyopo na baada ya wakati wa usemi ni njeo ijayo. Wakati huweza kuelezwa kwa vielezi kama jana, usiku, kesho, mchana na saa saba. Njeo hapa tunaangazia vile viambishi vyta kisarufi vinavyoambishwa kwenye vitenzi. Kwa mfano, katika Kiswahili Sanifu njeo kama *li, ta na a*, na katika Kitikuu tunapata pia njeo kama *li, ta na a*.

Reichenbach (1947), katika nadharia yake ya njeo, anazungumzia namna tatu muhimu za kiwakati tunapoangazia njeo katika sentensi yoyote:

U - wakati wa usemi

T - wakati wa tukio

R - wakati wa urejelezi

Kwa mfano: Amina ameondoka.

Hapa wakati wa usemi ni sasa, kwa hivyo tunaangalia kitendo kimefanyika muda kidogo na kimekamilika. Wakati wa tukio ni je, tukio lilikuwa katika wakati gani, ndiyo tunapata hali timilifu. Mwisho wakati wa urejelezi, pale tunaporejelea tukio hilo na kulizungumzia, ni baada ya muda gani na kadhalika. Nadharia ya Reichenbach ilikuwa na kasoro zake nyingi ndipo Comrie na wengine wakaja na nadharia bora zaidi baadaye.

b) Hali

Hali ni kipengele cha kisarufi ambacho hakiweki matendo katika mstari wa kiwakati, bali inahusu kuonyesha tofauti za matendo zinazoelezwa na vitenzi: timilifu, kuendelea, mazoea na kadhalika.

Massamba (2004) anasema, hali ni kipengele cha kisarufi ambacho hutumika kwa kuandamana na kitenzi, kimsingi, kikiwa na uamilifu wa kuonyesha ama kukamilika au kutokamilika kwa tendo linalotajwa.

Kwa mfano katika Kiswahili Sanifu viambishi vyat hali ni *me, ka, ki na na hu* na katika Kitikuu viambishi vyat hali ni *ndo, ie, ka, ki na hu*.

c) Dhamira

Ni kategoria ya kisarufi yenyе kutofautisha vitenzi katika hali mbalimbali. Dhamira hutafsiriwa kama lengo la msemaji au hali, vile kitendo kilivyotumika. Kuna dhamira tatu kuu: dhamira arifu, dhamira agizi na dhamira tegemezi.

Dhamira arifu - hutumika kwa kutoa maelezo au kuuliza maswali. Mfano: Amina anapika chakula. Je! Amina atakula hapa leo?

Dhamira agizi - hutumika katika kutoa amri. Mfano: Lete chakula haraka!

Dhamira tegemezi - Huonyesha matamano hasa yale ambayo hayapatikani. Mfano: Ningekuwa tajiri ningejenga jumba kubwa.

1.7.2 Fonolojia ya Kitikuu

Sehemu hii inaangazia kwa ufupi fonolojia ya Kitikuu. Kitikuu kina vokali tano na konsonanti ishirini na tatu. Konsonanti za Kitikuu zinaweza kuainishwa katika jedwali lifuatalo:

1.7.2.1 Konsonanti za Kitikuu

Jedwali 1

Jedwali la Konsonanti za Kitikuu

| | Midomo | Meno/ Midomo | Meno | Ufizi | Kaakaa Gumu | Kaakaa laini | Glota |
|---------------------|--------|-----------------|-------|-------|----------------|-----------------|-------|
| Vipasuo | p b | | t̪ d̪ | | | k g | |
| Vikwaruzo | | f, v | θ ð | s | ʃ | | h |
| Vipasuo/ Kwaruzo | | | | | tʃ ʃ | | |
| Vilainisho | | | | l r | | | |
| Viyeyusho | w | | | | j | | |
| Nazali | m | | ɳ | | n | ɳ | |


(Bakari, 1982)

Konsonanti za Kitikuu hufanana na za Kiswahili Sanifu, lakini Kitikuu hakina sauti /χ/, /z/ na /x/ kama zinazopatikana katika Kiswahili Sanifu. Vilevile mahali pa kutamkia sauti /t/, /d/ na /n/ ni tofauti kati ya Kiswahili Sanifu na Kitikuu. Kiswahili Sanifu hutamka sauti hizi katika ufizi lakini katika Kitikuu sauti hizi hutamkiwa menoni. Mifano ni kama ŋama (nyama), ŋoki (nyuki), ʈasi (tafi), ʈambi (tambi), dumu (dumu) na ɖaima (daima).

1.7.2.2 Vokali za Kitikuu

Kitikuu kina vokali tano kama vile Kiswahili Sanifu, nazo ni /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/. Kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu, Kitikuu hakina irabuunganifu. Hata kama vokali mbili au tatu zimefuatana basi hutamkwa mojamoja. Kwa mfano: #kiachu# - \$ki\$a\$chu\$, #choo# - \$cho\$o\$, #maingi#- \$ma\$i\$ngi\$.

Vokali za Kitikuu zinaweza kuainishwa katika mchoro ufuatao:



Vokali /i/ ni ya juu, mbele

Vokali /u/ ni ya juu, nyuma

Vokali /ɛ/ ni ya mbele, kati

Vokali /ɔ/ ni ya nyuma kati

Vokali /a/ ni ya mbele chini

Hapa mifano ya maneno ya Kitikuu yatatatolewa kulingana na konsonanti zake.

Jedwali 2

Mnukuu wa Konsonanti za Kitikuu

| Herufi | Mnukuu wa kifonetiki | Mfano wa Kitikuu | Kiswahili Sanifu |
|--------|----------------------|------------------|------------------|
| p | /p/ | pamba | pamba |
| b | /b/ | bafuta | kitambaa cheupe |
| t | /t/ | tambu: | tambuu |
| d | /d/ | amu | damu |
| k | /k/ | kija: | kidole |
| g | /g/ | gali | ghali |
| f | /f/ | fua | fua |
| v | /v/ | vava | chungu |
| th | /θ/ | œawabu | thawabu |
| dh | /ð/ | zawadi | zawadi |
| s | /s/ | sa: | saa |
| sh | /ʃ/ | ʃai | chai |
| h | /h/ | havule | msichana |
| ch | /tʃ/ | tʃakula | chakula |
| j | /j/ | jauri | jeuri |
| l | /l/ | laumu | laumu |
| r | /r/ | rarua | rarua |
| w | /w/ | uwε | wewe |
| y | /j/ | iyε | yeye |
| m | /m/ | mamε | mama |
| n | /n/ | nama | nyama |
| ny | /ɲ/ | ɲavu | nyavu |
| ng' | /ŋ/ | ŋɔmbε | ng'ombe |

1.7.3 Ngeli za Kitikuu

Kitikuu kama lahaja mojawapo ya Kiswahili, ina mpangilio wa nomino katika mfumo wa ngeli. Hii ni sifa inayopatikana katika lugha zote za Kibantu. Ngeli ni ule utaratibu wa kupanga nomino katika makundi yenye sifa zinazofanana kisarufi. Mpangilio wa awali ulizingatia viambishi awali vya nomino zenye sifa zinazofanana (mkabala wa kimofolojia). Ingawaje, kwa sababu ya matatizo mbalimbali yaliyojitekeza kwa kutumia viambishi awali katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika shule za msingi na upili

nchini Kenya, ngeli za kisintaksia zinazoonyesha upatanisho wa kisarufi ndizo zilizookeana bora na hivyo kutumiwa zaidi.

Tutaangalia mkabala wa ngeli kimofolojia na kisintaksia katika lajaja ya Kitikuu.

1.7.3.1 Ngeli kwa Mkabala wa Kimofolojia

Ngeli kwa mkabala wa kimofolojia ni vile viambishi vya kwanza /awali za nomino katika lugha husika. Ijapokuwa, wakati mwingine unapata kuwa baadhi ya maneno yanaweza kuwa katika ngeli husika na yasianze na viambishi hivyo. Mfano ni ngeli ya 9/10 (n-n) ambapo sio maneno yote yanaanza na **n** kwa umoja na **n** kwa wingi. Ngeli hizi (9/10) zinarundika maneno yote ambayo hayabadiliki katika umoja na wingi hata kuku, sungura, ndovu, baba, sakafu na kadhalika. Lakini ikumbukwe kuwa katika upatanishi, viumbe wenye uhai kama kuku, samaki na sungura watachukua upatanishi wa ngeli ya 1/2 (**a** / **wa** Kiswahili Sanifu na **a** /**va** kwa Kitikuu). Kwa mintarafu hiyo, ikawa ni shida kwa wanafunzi kutumia ngeli hizi za kimofolojia katika shule za msingi na upili, kwani zilikuwa zinawakanganya wanafunzi. Kwa hivyo, Taasisi ya Elimu ya Kenya mwaka 2001, ikaamua kuamuru matumizi ya ngeli za kisintaksia ambazo ni za upatanishi, katika kufunzia katika shule za msingi na upili. Jedwali lifuatalo linaonyesha ngeli za kimofolojia za Kitikuu na mifano.

Jedwali 3

Ngeli kwa Mkabala wa Kimofolojia

| Nambari | Ngeli za Kitikuu | Ngeli za Kiswahili Sanifu | Nomino katika Kitikuu | Mifano ya sentensi katika Kitikuu | Maana ya sentensi katika Kiswahili Sanifu |
|---------|------------------|---------------------------|----------------------------|-------------------------------------|---|
| 1 | n, mu | m, mu | <i>nchu, ndhee, muke</i> | <i>Ndhee wa mui alikufa yudhi.</i> | Mzee wa mji alikufa juzi |
| 2 | va | wa | <i>vachu, vadhee, vake</i> | <i>Vadhee va mui valikufa yudhi</i> | Wazee wa mji walikufa juzi |
| 3 | n, mu | m, mu | <i>nkono, muili</i> | <i>Nkono wake</i> | Mkono wake |

| | | | | <i>waliumia</i> | uliumia |
|-----|------|------|------------------------------------|--|-------------------------------|
| 4 | mi | mi | <i>mikono, miili</i> | <i>Mikono ake iliumia</i> | Mikono yake iliumia |
| 5 | i/ø | ji/ø | <i>ipipa, ingi, ienyō</i> | <i>Ienyo hunivava</i> | Jino lanuma |
| 6 | ma | ma | <i>mapipa, maingi, menyō</i> | <i>Menyo hunivava</i> | Meno yanuma |
| 7 | ki | ki | <i>kisu, kiachu</i> | <i>Kisu hukacha</i> | Kisu kinakata |
| 8 | dhi | vi | <i>dhisu, dhiachu</i> | <i>Dhisu hukacha</i> | Visu vinakata |
| 9 | n | n | <i>nadhi, numba</i> | <i>Nadhi indoanguka</i> | Nazi imeanguka |
| 10 | n | n | <i>nadhi, numba</i> | <i>Nadhi zindoanguka</i> | Nazi zimeanguka |
| 11 | u | u | <i>udhi, uficho</i> | <i>Udhi haushoni</i> | Uzi haushoni |
| 10a | n, ø | n,ø | <i>nyudhi, ficho</i> | <i>Nyudhi hadhishoni</i> | Nyuzi hazishoni |
| 14 | u,vu | U | <i>vuyi, vunga, uchafu, udhuri</i> | <i>Vuyi huchokocha</i> | Uji huchemka |
| 15 | ku | ku | <i>kutedha, kuimba,kusoma</i> | <i>Kutedha kwake kulichufurahisha</i> | Kucheza kwake kulitufurahisha |
| 16 | pa | pa | <i>hapa,hapo</i> | <i>Musitedhe hapa</i> | Msicheze hapa |
| 17 | ku | ku | <i>huku,kulee</i> | <i>Musendre kulee</i> | Msiende kule |
| 18 | - | mu | | - | Nyoka umo humu |

1.7.3.2 Ngeli kwa Mkabala wa Kisintaksia

Ngeli za kisintaksia ni viambishi vyta upatanishi katika kitensi. Kwa kuwa kitensi ni neno muhimu katika sentensi, basi nomino husika hutegemea kitensi kwa upatanishi wake. Katika uainishaji wa ngeli kisintaksia kulingana na upatanishi, hakuna kuwachanganya wanafunzi bali nomino hupata upatanishi wake katika kitensi bila kukanganya. Kwa mfano, nomino zote za viumbe zitaingia katika ngeli ya **a/wa** katika Kiswahili Sanifu na **a/va** katika Kitikuu. Vilevile nomino zote ambazo hazina uhai na hazibadiliki katika umoja na wingi, basi zitaingia katika ngeli ya upatanisho wa **i/zi** Kiswahili Sanifu, na **i/dhi** katika Kitikuu. Jedwali lifuatalo linaonyesha mofimu za kisintaksia au za upatanishi katika Kitikuu na mifano.

Jedwali 4

Ngeli kwa Mkabala wa Kisintaksia

| Nambari | Ngeli za Kitikuu | Ngeli za Kiswahili Sanifu | Mifano ya viambishi vyatya ngeli katika sentensi za Kitikuu | Mifano ya viambishi vyatya ngeli katika sentensi za Kiswahili Sanifu |
|---------|------------------|---------------------------|---|--|
| 1 | a | a | <i>Mwana andokuya</i> | Mtoto amekuja |
| 2 | va | wa | <i>Vana vandokuya</i> | Watoto wamekuja |
| 3 | u | u | <i>Nchi ulikachwa</i> | Mti ulikatwa |
| 4 | i | i | <i>Michi ilikachwa</i> | Miti ilikatwa |
| 5 | li | li | <i>Ijiwe liliuswa</i> | Jiwe lilitrushwa |
| 6 | ya | ya | <i>Majiwe yaliuswa</i> | Mawe yalirushwa |
| 7 | ki | ki | <i>Kiachu kindokachika</i> | Kiatu kimekatika |
| 8 | dhi | vi | <i>Dhiachu dhindokachika</i> | Viatu vimekatika |
| 9 | i | i | <i>Nadhi itavoaa</i> | Nazi itaoza |
| 10 | dhi | zi | <i>Nadhi dhitavoaa</i> | Nazi zitaoza |
| 11 | u | u | <i>Udhi utakachika</i> | Uzi utakatika |
| 10 | dhi | zi | <i>Nyuzi dhitakachika</i> | Nyuzi zitatatika |
| 14 | u | u | <i>Udhivu undodhidi</i> | Uvivu umezidi |
| 15 | ku | ku | <i>Kutedha kwake kulichufurahisha</i> | Kucheza kwake kulitufurahisha |
| 16 | pa | pa | <i>Palipochekechea ni hapa</i> | Palipoteketea ni hapa |
| 17 | ku | ku | <i>Kuimba huku ni kudhuri</i> | Kuimba huku ni kuzuri |
| 18 | - | mu | - | Mahali humu mnapendeza |

1.8 Hitimisho

Sura hii imeangazia usuli wa mada kwa kutoa maelezo ya kimsingi juu ya lahaja ya Kitikuu na sehemu kunakozungumzwa lahaja hii. Swala la utafiti limefafanuliwa kuonyesha umuhimu wa kuwepo kwa utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti. Malengo, maswala ya utafiti, upeo, mipaka na natija ya utafiti yameshughulikiwa katika sura hii vilevile. Sarufi ya Kitikuu imeangaziwa kwa kifupi, kwanza kwa kuelezea dhana za njeo, hali na dhamira. Pili, fonolojia ya Kitikuu kwa upande wa konsonanti na vokali zake zimeainishwa. Tatu, ngeli za Kitikuu zimeelezewa kwa kurejelea mkabala wa kisintaksia na mkabala wa kimofolojia.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA

2.0 Kitangulizi

Sura hii inaangalia mapitio ya maandiko ya lahaja ya Kitikuu, sarufi ya Kiswahili Sanifu na mapitio ya maandiko kuhusu nadharia ya Uminimalisti. Katika sehemu ya pili ya sura hii inashughulikia msingi wa nadharia ya Uminimalisti hasa kwa kutilia mkazo kanuni ya ukaguzi wa sifa ambayo ndiyo itakayotumiwa katika kazi hii.

2.1 Yaliyoandikwa kuhusu Sarufi ya Kiswahili na Kitikuu

Nurse na Hinnebusch (1993) wamefanya ulinganishi wa Kihistoria wa Kiswahili na lahaja zake na lugha za Sabaki kifonolojia na kimofolojia. Kazi yao, japo kwa ufupi inaangazia mofolojia ya kitenzi cha Kitikuu, na haiangalii kwa undani juu ya kirai tenzi. Inataja kwa mfano, kitenzi cha Kitikuu kina upekee wake wa kukipatia kiambishi cha njeo iliyopo kama **a**, na **hu**, katika lahaja hiyo na kutoa mifano kama; *chwataka kuimba eo*, (twataka kuimba leo) *chwayiva* (twajua) na wanasema kiambishi hiki hakitumiki kwa vitenzi vyote, kama kwa mfano huwezi kusema **chwafanya kadhi* (tunafanya kazi), hali hii ni kama katika Kiswahili Sanifu, ambapo sio vitenzi vyote vinavyotumia njeo iliyopo **a**, lakini vitenzi vyote hutumia kiambishi **na** kwa njeo hiyo. Pia wanataja kitenzi kama *chwenende* (*twende*), wakisema hakionekani kiambishi cha njeo kiko wapi, kazi hii itaonyesha kuwa hapo kuna mfanyiko wa kifonolojia wa kudondosha yokali, na ndiyo yokali {**a**} ya njeo iliyopo imedondoshwa. Nurse na Hinnebusch wametaja kidogo tu juu ya hali timilifu ya Kitikuu **ndo** ambacho ni kiambishi cha hali, sawia na **me** katika Kiswahili Sanifu. Kazi hii inaangazia mofimu zote hizo za njeo, hali na dhamira kwa mapana na marefu.

Ashton (1944) ameandika kuhusu sarufi ya Kiswahili Sanifu. Ameangazia vitenzi katika Kiswahili Sanifu, akielezea pia viambishi vya njeo na hali lakini bila ya kuvitofautisha. Anaelezea kuwa kuna viambishi vya njeo sita za kimsingi ambazo ni **li, na, ta, a, me** na **hu**. Katika utangulizi wake, Ashton anaonya kuwa tusifananishe viambishi vya njeo vya Kiswahili na vya Kiingereza kwa sababu katika Kiswahili njeo haziangaliwi tu kwa muktadha wa wakati, bali pia huonyesha hali ya matendo kama ya kukamilika au kuendelea (uk.35). Ashton hatofautishi viambishi vya hali na njeo, bali anaviangalia vyote sita kama viambishi vya kimsingi vya njeo. Pia anaangazia viambishi vingine vya njeo mbali na hivyo vya msingi ambavyo ni **ka, ki, nga, nge** na **ngali** pamoja na ukanushi wake. Utafiti huu ni tofauti na kazi ya Ashton kwani inatofautisha viambishi hivyo vya njeo, hali na dhamira na kutoa mifano katika Kitikuu.

Vitale (1981) ameandika kuhusu sintaksia ya Kiswahili Sanifu. Vilevile ametaja kwa ufupi juu ya sarufi ya Kiswahili Sanifu kwa kuangazia mofolojia ya kitenzi. Anaelezea viambishi mbalimbali vya kitenzi; njeo na hali vikiwemo. Anataja viambishi vya njeo na hali vinavyopatikana kama viambishi awali katika kitenzi cha Kiswahili Sanifu, baada ya kiambishi cha nafsi, navyo ni njeo iliyopo **na**, iliyopita **li**, ijayo **ta**, timilifu **me**, na mazoea **hu**, haelezei zaidi bali anatoa tu mifano katika sentensi. Hataji viambishi vya dhamira. Utafiti huu unaweka bayana dhana hizo za njeo, hali na dhamira. Mofimu ya **{na}** kulingana na utafiti huu ni hali ya kuendelea na siyo njeo iliyopo kama inavyodaiwa na Vitale. Mofimu zaidi za hali na dhamira zimeangaliwa katika utafiti huu tofauti na kazi ya Vitale.

Mohammed (2001) ameangazia sarufi ya Kiswahili Sanifu ambapo ameangalia juu ya njeo, hali na dhamira. Mohammed katika kazi yake hatofautishi dhana hizi, yaani

huenda akizichanganya kwa kurejelea viambishi vya na hali dhamira kama za njeo. Anagawanya njeo hizo katika makundi manne makuu. Kundi la kwanza, analiita ‘Njeo I’, hapa anataja viambishi vya njeo iliyopo **a** na **na**, njeo iliyopita **li** na **ali**. Kundi la pili, ‘Njeo II’, anasema ni njeo ijayo **ta** na timilifu **me**. Kundi la tatu, ‘Njeo III’, anasema ni ya mazoea **hu**, ya masharti **ki** na ya mfululizo **ka**. Kundi la nne, ‘Njeo IV’ ni kundi la **nge**, **ngali** na **ngeli** ambazo anaziita njeo za masharti. Mohammed pia ametoa mifano ya sentensi mbalimbali katika hali yakinishi na kanushi za ‘njeo’ hizo mbalimbali. Utafiti huu utarekebisha hayo kwa kuweka wazi dhana za njeo, hali na dhamira.

Kazi mbili za Comrie (1976, 1985) zinatoa mwangaza katika uelewa wa dhana za njeo na hali, vilevile katika kuweka mipaka ya dhana hizo. Ijapokuwa ni kazi zilizoandikwa kwa Kiingereza, kwa hivyo mifano yake ni ya Kiingereza na Kifaransa zaidi, lakini zinatupatia taswira juu ya dhana za njeo na hali. Comrie (1976) katika utangulizi wake, anaanza kwa kufafanua dhana ya njeo, hali na dhamira na kutoa mifano katika lugha ya Kiingereza na Kifaransa kama tutakavyoona katika kazi hii kwa kumnukuu. Anakubali kuwa wataalam wengi huwa wanazichanganya dhana hizi. Comrie (1976,1985) anafafanua kwa kina dhana za njeo na hali na kutoa mifano katika lugha za Ulaya.

Beaudoin-Lietz (1999) tasnifu yake ya uzamifu anaangazia ukarusha wa njeo, hali na dhamira katika Kiswahili Sanifu. Kazi ya-Beaudoin inaonyesha matumizi ya mofimu za njeo, hali na dhamira na ukarusha wake, muingiliano wa mofimu hizo katika sentensi ambatano na nafasi zinazochukua mofimu za ukarusha katika kitende cha Kiswahili Sanifu. Hata hivyo kazi yake haikujihusisha na kuangazia mofosintaksia ya Kiswahili, imejishughulisha tu na matumizi ya mofimu hizo za njeo, hali na dhamira na ukarusha

wake. Kazi ya Beaudoin-Lietz ni tofauti na kazi yangu kinadharia na Beaudoin ameshugulikia zaidi ukarusha katika Kiswahili Sanifu na siyo Kitikuu.

Mgullu (1999), ameshughulikia mofolojia ya kitensi cha Kiswahili Sanifu. Mgullu, anapajaribu kutoa maelezo juu ya dhana ya njeo anaeleza kuwa huonyesha wakati tendo lilipotendeka, ambapo dhana hiyo ni tatanishi. Tukirejelea vielezi vya wakati kama vile kesho, mchana, na saa tano pia huonyesha wakati, je hizo pia ni njeo? Anatoa viambishi vya njeo tatu, wakati uliopo **na**, uliopita **li** na ujao **ta**. Haelezei maana ya hali, bali anasema kuwa mofimu nyininge katika Kiswahili Sanifu kabla ya mzizi, ni mofimu za hali na anatoa mifano ya hali ya kuendelea **na**, timilifu **me** na hali ya mazoea **hu**. Ameelezea pia juu ya dhamira, akisema kuwa huonyeshwa kwa mofimu za viishio vya kitensi; dhamira elezi, ulizi na amrishi katika hali yakinishi na kanushi. Utafiti huu ni tofauti na kazi ya Mgullu kwani unatoa maelezo ya dhana za njeo, hali na dhamira kwa njia inayostahili na kuelewaka zaidi.

Waihiga (1999) ameandika juu ya sarufi ya Kiswahili Sanifu. Amekiangalia kitensi na kuangazia mofolojia ya kitensi; hasa njeo, hali na mnyambuliko. Hata hivyo, Waihiga, anachanganya viambishi hivyo vya njeo, hali na dhamira. Ametumia neno njeo kama kisawe cha ‘nyakati’ na akatoa nyakati tatu zenye kutumia viambishi **na**, **li** na **ta** kwa wakati uliopo, uliopita na ujao mtawalia. Kiambishi **na** cha wakati uliopo kimeleta utata, kwani kuna wanaodai kuwa kiambishi hicho ni cha hali ya kuendelea na siyo njeo. Vilevile amerundika viambishi vya dhamira na hali vyote pamoja na kuviangalia kama viambishi vya hali yaani viambishi **me**, **a**, **ki**, **ka**, **ngali**, **ngeli**, **nge**, na **hu**. Utafiti huu, umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuvitofautisha viambishi hivyo mbalimbali na sio kuvirundika pamoja kama alivyofanya Waihiga.

Bybee na Dahl (1989) wameshughulikia dhana za njeo na hali kwa undani, na kutoa aina mbalimbali za njeo na hali katika baadhi za lugha mbalimbali za ulimwengu. Kazi yao inaangazia hali na njeo na namna zinavyotumika katika lugha takriban sitini na nne kutoka sehemu tofauti tofauti. Kazi yao haikuangazia Kitikuu na viambishi vya dhamira, kwa hivyo inakuwa muhimu kwa utafiti huu kushughulikia lahaja hii ya Kitikuu na viambishi vya dhamira.

Lindfors (2003) kazi yake ya uzamili ameangazia njeo na hali katika Kiswahili Sanifu. Ameangazia maana ya njeo na hali na kuonyesha matumizi yake. Katika kazi yake anaonyesha mofimu {na} ni hali na sio mofimu ya njeo kama baadhi ya kazi za awali zinavyoonyesha. Lindfors haangalii dhamira katika kazi yake na hatumii nadharia katika kuainisha njeo na hali katika Kiswahili Sanifu.

2.2 Yaliyoandikwa kuhusu Nadharia

Cook na Newson (1996) wameelezea kuhusu nadharia ya Uminimalisti wakiilinganisha na nadharia ya Umilikifu na Masharti (UM) huku wakionyesha tofauti kati yazo. Wanaifananisha nadharia ya Uminimalisti na nadharia ya Umilikifu na Masharti wakisema zinafanana sana isipokuwa kwa uchanganuzi wao, wakidai kuwa Uminimalisti ni mwendelezo wa UM na sio mkengeuko (uk. 312). Wamejaribu kwa kiasi kikubwa kuonyesha kuwa nadharia ya Uminimalisti ni maendelezo na uzibaji pengo wa nadharia ya UM. Wanaelezea matatizo ya nadharia ya Umilikifu na Masharti ambayo yameweza kutatuliwa na Uminimalisti kwa kuondosha vijinadharia vingi ndani yake. Wanadai kuwa lugha ni ushirikiano baina ya sauti (UF) na maana (US), hivyo vitengo hivi viwili hushirikiana kwa upande mmoja wa sauti na kwa pili utambuzi wa maana katika akili (uk. 313). Hivi ndiyyo vitengo vya lazima katika mjumuiko: UF na

US. Kazi yao imetua maelezo ya Uminimalisti kwa njia sahili na rahisi kueleweka, kupitia mifanyiko ya kimkotoo hadi kufikia mjumuiko. Hata hivyo, kazi yao haituonyeshi mifano ya ukaguzi wa sifa na uhamisho kama tunavyotarajia katika kazi hii.

Baker (1988) anaangalia mofolojia na sintaksia, ni kazi ya kimofosintaksia. Kazi yake inaangazia kuchanganua nomino kwa uhusiano na sintaksia ya uhamishaji wa kitenzi. Kuhamishwa huku husababishwa na kitenzi. Baker anaangazia haya katika kazi yake ya nadharia ya Ugubikaji. Umuhimu wa nadharia hii ni kuwa neno moja lenye kujisimamia kisemantiki linagubikwa na lingine. Haya yanaendelezwa katika nadharia kuu ya Umilikifu na Masharti. Vilevile aliendeleza Kanuni ya Kioo inayodai kuwa mofolojia nyambuaji lazima ihusiane moja kwa moja na unyambuaji wa kisintaksia. Hii ni kuonyesha ule uhusiano uliopo kati ya mofolojia na sintaksia. Kazi yetu inashughulikia uhusiano huu wa kimofosintaksia kwa kuzingatia mtazamo wa Uminimalisti.

Hornstein na wenzake (2005) wameshughulikia kwa kina nadharia ya Uminimalisti wakilinganisha na kuikosoa nadharia ya Umilikifu na Masharti (UM). Wamevieleza vile vijinadharia au kanuni zinazohusishwa na nadharia ya Uminimalisti kama kanuni ya iktisadi, kanuni ya ukaguzi wa sifa, kanuni ya ukaguzi mfupi, kanuni ya usogezi, kanuni ya kuchelewesha na kanuni ya ubinafsi. Usogezi huhamasishwa na sababu za kibinafsi ili kutimiza malengo ya kiambajengo kinachosogezwa. Sifa za umbo la kifonetiki (UF) ni zile tu zinazohusika kuamua umbo la kifonetiki na umbo la kimantiki (US) huhusika kuamua umbo la kisemantiki. Kanuni ya usogezi huhusika na kukagua sifa za kimofolojia na kisintaksia katika sentensi na hivyo kitenzi cha Kitikuu chenye ukwasi wa kimofolojia husogezwa na kukaguliwa katika hatua mbalimbali.

Kazi za Radford za 1997(a) na 1997(b) zinaelezea kwa ufasaha na uwazi zaidi nadharia hii ya Uminimalisti. Anaelezea nadharia ya ‘Kanuni na Vigezo’ kwa kuonyesha kuwa Kanuni ni zile sheria za lugha zinazofanana kwa lugha zote ulimwenguni kisha kuna sheria ambazo ni za lugha mahsus ambazo ni Vigezo ambapo kila lugha ina sheria zake. Ameonyesha na kueleza vipengele vyote kuanzia leksikoni katika mifanyiko ya kimkokotoo hadi mjumuiko, hivi huwa ni katika ule umilisi alionao mzawa wa lugha fulani.

Schroeder (2008), ameellezea nadharia ya Uminimalisti na inavyofanya kazi kupitia ukaguzi wa sifa akiitumia kwa lugha mojawapo ya Kiafrika. Ameangalia nadharia ya ukaguzi wa sifa katika lugha ya Toposa inayozungumzwa kusini mwa Sudan. Ni lugha ambishi bainishi kama ilivyo lahaja ya Kitikuu. Hata hivyo kazi yake inaangazia mpangilio wa maneno katika sentensi za Toposa, hivyo kazi yake ni tofauti na utafiti huu unaoangazia njeo, hali na dhamira katika Kitikuu.

Schroeder (2005), makala ya seminaa ya Chuo Kikuu cha Nairobi alitoa maelezo ya nadharia ya Uminimalisti kwa njia ya muhtasari, ambayo ni ya kueleweka kwa urahisi hasa maelezo yake kuhusu mifanyiko ya kimkokotoo kutoka leksikoni hadi kwa mjumuiko wa UF na US. Sheria zinazojitokeza kama nadharia ya iktisadi yenye kanuni kama usogezi mfupi zaidi, kanuni ya kuchelewesha na kanuni ya ubinafsi zimefafanuliwa.

Kazi ya Swaleh (2005) ya uzamili kuhusu mofosintaksia ya kishazi cha Kitikuu ni chanzo tu cha utafiti wa kimofosintaksia. Kazi ya Swaleh ya awali iliangazia kwa jumla kishazi huru cha Kitikuu kwa kutumia nadharia ya Uminimalisti. Kazi hii inaendeleza kwa kushughulikia kwa mapana zaidi kitenzi cha Kitikuu hasa kwa kurejelea viambishi

vya kisarufi vya njeo, hali na dhamira. Muingiliano wa njeo, hali na dhamira katika sentensi ambatano zimeainishwa katika utafiti huu.

2.3 Msingi wa Nadharia

Nadharia ya Uminimalisti iliasisiwa na mwanaisimu Noam Chomsky, mwaka wa 1993. Ni nadharia inayojaribu kuelezea muundo wa lugha kwa kutumia sheria sahili na finyu iwezekanavyo. Kuanzia miaka ya hamsini Chomsky amejaribu kupendekeza nadharia mbalimbali za sarufi bia. Chomsky anaamini kuwa lugha zote zina sifa za kiulimwengu ambazo zinafanana, na ndiyo maana akawa na hamu ya kuibuka na nadharia ambayo ingeweza kutumiwa na lugha zote ulimwenguni. Japo kuna sifa za lugha za kiulimwengu, pia kuna vigezo ambazo ni za lugha mahsus. Mwaka wa 1957, Chomsky alibuni Sarufi Miundo, na mwaka wa 1965 akafanya marekebisho na kuibuka na Sarufi Zalishi Geuza Maumbo. Kufikia miaka ya sabini, alifanya mabadiliko na kuibuka na Nadharia ya Wastani, ambayo baadaye ilirekebishwa na kuwa Nadharia ya Wastani Panuzi. Kufikia hapa, nadharia hizi zilishughulikia sarufi miundo virai.

Mwaka wa 1981, Chomsky aliasisi Nadharia ya Umilikifu na Masharti. Nadharia ya Uminimalisti ilijaribu kuendeleza Nadharia ya Umilikifu na Masharti (UM) iliyokuwa na utata mwingi (Cook na Newson, 1996). Nadharia ya UM ilikuwa na vijinadharia ndani yake kama vile eksibaa, uhusika, umilikifu, masharti, theta, utawala na ufunge. Mnamo mwaka wa 1993, ndipo Chomsky alirahisisha nadharia ya UM yenyе misingi ya kimofosintaksia aliyoita Uminimalisti, kwa kutumia sheria chache iwezekanavyo. Aliangazia kuwa kuna zile sheria zinazotumiwa na lugha zote ‘Kanuni’ na zile za kipekee katika lugha fulani ‘Vigezo’. Kwa hivyo Chomsky aligundua kuwa sheria za lugha moja huweza kuwa tofauti na hivyo kushindwa kuchanganua au kuelezea lugha nyingine. Nadharia hii zaidi imeweza kushughulikia lugha zenye ukwasi wa

kimofosintaksia, ambapo Kitikuu ni lahaja mojawapo yenyе sifa hiyo. Kwa hivyo tukaonelea nadharia hii itatufaa sana katika kazi yetu.

Chomsky, anashikilia katika nadharia hii kuwa vitu vya kimsingi vya kiisimu ni umbo la kifonetiki (UF) ambayo ni matamshi au sauti zinazotolewa na umbo la kisematiki (US) au maana inayokusudiwa na matamshi hayo. Hapa umilisi wa wazungumzaji ndio unaotumiwa katika kuelewana kwao.

Nadharia hii tulionelea kuwa mwafaka kwa utafiti huu, kwa kuwa inashughulikia lugha ambishi-bainishi. Tulionelea kuwa itatufaa kwa lahaja yetu ya Kitikuu yenyе ukwasi wa mofolojia. Vilevile nadharia hii inarahisisha nadharia ya UM ambayo ilikuwa na vijinadharia vingi vya kukanganya. Imetupilia mbali wazo la umbo ndani na umbo nje na sasa kuna tu mjumuiko.

Nadharia ya Uminimalisti inashughulikia mofositanksia ya lugha, mofolojia inachangia katika sintaksia ya lugha husika. Katika Uminimalisti tofauti na nadharia ya Umilikifu na Masharti (UM) yenyе umbo la ndani kisha linavurumishwa hadi umbo la nje, hapa tunapata umbo la kiisimu katika mjumuiko. Umbo la ndani na uvurumishaji yanatupiliwa mbali, kiwango cha mjumuiko kinawakilisha umbo la kimantiki (US) na umbo la kifonetiki (UF).

2.3.1 Mihimili ya Nadharia ya Uminimalisti

- Nadharia ya Uminimalisti husisitiza viwango viwili vya uchanganuzi, umbo fonetiki na umbo mantiki; na kutupilia mbali dhana za umbo nje na umbo ndani, dhana zilizotumiwa hapo awali na UM.
- Hutilia maanani mofosintaksia ya lugha, kwani mofolojia huchangia sana katika sintaksia ya lugha.

- Sifa za uambishaji na unyambuaji hupewa nomino na vitenzi katika leksikoni. Kwa kuwa tayari vimeambishwa vinazalishwa kimsingi katika kirai tenzi katika vichwa vyao tofauti.
- Kuna nadharia ya ukaguzi wa sifa ambapo kanuni ya usogezi huwepo kukagua sifa za uzalishaji kuhakikisha ukubaliano na mahali pa kisintaksia katika umbo la sentensi.
- Nadharia hii hufanya kazi kupitia mfanyiko wa kimkokotoo ambapo huanzia sehemu ya leksikoni ambapo sifa za kileksika na kimofosintaksia huanzia. Sehemu ya hisabati au numerali huhusika na kuchaguao sifa za kimofosintaksia ambazo ndizo zinazohitajika. Muungano huhusisha kuunganisha viambajengo na kuunda miundo. Hii husababisha usogezi ili kukagua sifa za kimofolojia zinasogezwa na kukaguliwa katika hatua mbalimbali.
- Lugha thabiti au imara katika nadharia hii huonekena na kukaguliwa kabla ya mdhihiriko-wazi (Mfano Kitikuu), kwa sababu ya sifa za kimofolojia zinazohitaji kukaguliwa. Kwa upande wa lugha dhaifu hukaguliwa baada ya mdhihiriko-wazi (Mfano Kiingereza) kwa sababu ya kukosa sifa za kimofolojia.


2.3.2 Mifanyiko ya Kimkokotoo

Kutoka kiwango cha leksikoni hadi kufikia kiwango cha mjumuiko, ambapo tuna sehemu ya kisintaksia, kuna hatua mbalimbali zinazopitiwa.

Katika leksikoni kuna leksika zote, sifa za kisarufi na sifa za kimofosintaksia ya lugha fulani. Mfanyiko unaoitwa numerali, huchagua sifa za kimofosintaksia ya lugha fulani. Muungano hutokea na huunganisha vipashio (elementi) mbalimbali na kuunda maneno na vira ili kuunda miundo. Utendaji wa 'kuchagua' na 'kuunganisha' ni sehemu muhimu katika nadharia yoyote ya lugha asilia (Chomsky, 1995: 226). Ujenzi wa miundo katika

Uminimalisti ni tofauti na ule wa UM. Mfumo wa sasa unapunguza vile viwango vinne vya uwakilishi; umbo ndani, umbo nje, umbo la kisemantiki na umbo la kifonolojia hadi viwango viwili vya kujumuika - umbo la kisemantiki na la kifonolojia (Marantz, 1995:353). Umbo la kisemantiki (au mantiki) hujumuika na semantiki au maana na umbo la kifonolojia hujumuika na matamshi.


Kielelezo kifuatacho kinaonyesha muhtasari wa mfanyiko wa kimkokotoo:




(Schroeder, 2005: Makala ya Seminaa)

Nadharia ya Uminimalisti inabakisha nadharia ya Eksi baa, japo kwa marekebisho.

Inabakisha ile sehemu ya uhusiano wa kichwa na spesifaya na uhusiano wa kichwa - kichwa (Chomsky, 1993:6). Mchoro kama ufuatao ndio tunaoupata:



Uundaji miundo huhusisha mfumo wa muungano na usogezi. Uundaji wa miundo unachochewa kukiwa na haja na kuruhusiwa na ushahidi wa kimofosintaksia wa lugha fulani. Nadharia hii hairuhusu utupu wa nafasi yoyote. Kwa mfano tunaweza kuwa na kielelezo chenye kichwa na kisiwe na kirai. Mfano: **Alicheza**, itaweza kuonyeshwa kwenye kielelezo kifuatacho, ambacho hakina spesifaya ya nomino:



Usogezi katika nadharia hii ni sehemu nyingine muhimu. Usogezi upo kwa sababu ya kukagua sifa. Inakagua sifa za uzalishaji kuhakikisha ukubaliano na mahali pa kisintaksia katika umbo la sentensi. Usogezi hadi upatanishi kiima (UPk), njeo (NJ) na upatanishi yambwa (UPy) ni mifanyiko ya kukagua sifa inayofutilia mbali sifa za kidhahania ili zisionekane katika umbo la kifonolojia (Schroeder, 2008:15). Kitendi kinakaguliwa kwa kusogezwa kupitia kwa UP na NJ na sifa za uhusika hukaguliwa kwa kusogezwa mahali kwa spesifaya ya kirai cha upatanishi (KUP) (Cook na Newson, 1996:328).

Usogezi katika nadharia ya Uminimalisti unatoa Kanuni za Iktisadi mbalimbali nazo ni: Usogezi mfupi zaidi, kuchelewesha na ubinafsi. Kanuni ya usogezi mfupi zaidi inasema kuwa usogezi unatokea tu hadi mahali karibu zaidi panapostahili. Kanuni ya

kuchelewesha nayo inasema kuwa, usogezi hutokea tu pale panapokuwa na haja. Kanuni hii huchelewesha usogezi mpaka panapotokea haja inayosababishwa na ushahidi wa kimofosintaksia ya lugha (Schroeder, 2008:3).

Kanuni ya ubinafsi nayo inasema kuwa viambajengo havisogezwi kutimiza lengo la viambajengo vingine; Usogezi huhamasishwa na sababu za kibinafsi, ili kutimiza haja ya kiambajengo kinachosogezwa (Marantz, 1995: 358).

Baada ya mifanyiko ya uundaji miundo, mfanyiko wa kimkokotoo hutoa maelezo ya kileksikoni kwa umbo la kifonetiki (UF) na umbo la kimantiki (US). Mdhihirisho wazi ndiyo sehemu ambapo miundo virai inayozalishwa na mifanyiko ya numerali na muungano, hutoa sehemu mbili tofauti: sehemu ya UF inayozalisha sifa za kifonetiki na US inayozalisha sifa za kimantiki (Radford, 1997: 171-2). Mahitaji haya yanalazimishwa na sarufi bia inayoitwa 'Kanuni ya Ufanuzi wa Kina' (UK). Kanuni hii inafafanua kuwa kiwakilishi cha habari fulani lazima kiwe na elementi zote zinazochangia moja kwa moja katika ufanuzi wa kiwango husika. Kwa hivyo sifa zinazohusika na umbo la kifonetiki ni zile tu zinazohusika katika kuamua umbo la kifonolojia, vilevile umbo la kimantiki ni zile sifa tu zinazohusika katika kuamua umbo la kisemantiki. Hivyo tunapokuwa na uzalishaji wa kiwakilishi cha umbo la kifonetiki kutosheleza matakwa ya UK basi yatakutana katika UF. Vilevile kwa kiwakilishi cha US, kinapotosheleza matakwa ya UK kwa kuchukua tu sifa za kisemantiki, itakutana katika US. Iwapo UF na US za habari fulani yatatimiza matakwa ya UK, basi habari ya uzalishaji huo utakutana na hivyo utaleta maana kisarufi. Ikiwa UF na US itavunja matakwa ya UK, matokeo ya uzalishaji yatagongana; hivyo kutoleta maana kisarufi (Radford, 1997:171). Kielelezo cha Schroeder hapo juu ni muhtasari wa haya yote.

2.3.3 Kanuni ya Ukaguzi wa Sifa katika Uminimalisti


Nadharia ya Uminimalisti inatilia manaani mofolojia ya lugha. Kulingana na Chomsky (1993:32) utendaji kazi katika mfumo wa kimkokotoo unaendelezwa na msukumo wa kimofolojia. Katika Uminimalisti kaida ya kimfosintaksia inachukulia kuwa sifa za uambishaji na unyambuaji zinapewa vitenzi na nomino katika leksikoni. Kwa hivyo nomino na vitenzi ambavyo tayari vimeambishwa vinazalishwa kimsingi katika kirai tenzi, katika vichwa vyao tofauti. Tofauti na nadharia ya UM ambapo vitenzi na nomino vinavurumishwa katika umbo la ndani ili vichukue sifa zake na kuonekana vyenye maana kisarufi katika umbo la nje (Schroeder, 2008:16).

Katika Uminimalisti, usogezi upo kwa sababu ya kukagua sifa ambapo sifa dhahania za uzalishaji zinakaguliwa kuhakikisha usahihi wake dhidi ya mahali pa kisintaksia katika muundo wa sentensi. Katika nadharia ya Uminimalisti kirai tenzi hubeba habari zote. Elementi za upatanisho (UP), njeo (NJ) na hali (HA) zinawekwa katika kitende katika hatua ya leksikoni. Elementi za UP na NJ hutumiwa kukagua sifa za kitende. Mofolojia ya nomino hupima sifa za uhusika na hukaguliwa kwa KUPk na KUPy chini ya spesifaya.

Lugha katika Uminimalisti zinaelezewa kama zenye upatanisho dhaifu au upatanisho imara. Upatanisho imara unaonekana katika umbo la kifonetiki lakini upatanisho dhaifu hauonekani. Lugha zenye upatanisho imara inalazimisha kitende kusogezwa ili kukagua kitita cha sifa dhahania ili ziondolewe kabla mdhihirisho wazi kufikia UF. Lugha zenye upatanisho dhaifu hazilazimishi kitende kusogezwa kwani hakuna sifa za kukaguliwa. Hivyo basi kitende huonekana tangu mwanzo katika UF na US. Kwa mfano lugha ya Kiingereza ina upatanisho dhaifu kwa hivyo kitende kitaonekana tangu mwanzo katika UF na US. Lahaja ya Kitikuu ni aina ya lugha yenye upatanisho imara kwani ina kitita

cha sifa dhahania katika kitenzi chake, zinazohitaji kukaguliwa. Kitita cha sifa dhahania ni kama ngeli, nambari (kama ni umoja au wingi) na nafsi zinazotofautisha kutambulisha ukubaliano wa uamilifu wa majukumu ya kiima na yambwa. Inachukulia umuhimu wa lugha zenyeye uhusika unaoambishwa. Kama nilivyosema mbeleni, umuhimu wa kukagua sifa ni kuwa kila lugha lazima isogeze kitenzi, yaani kitenzi kinasogea kwenye vifundo vyatuzishaji, na virai nomino husogea kwenye spesifaya za KUPk na KUPy kwa kukagua sifa za kiima na yambwa zinazoonekana na kujisimamia. Mfano wa kielelezo matawi chenye kuonyesha usogezi na ukaguzi wa sifa katika Kitikuu:


Amina alinunua nama. *Amina a - li - nunu - a nama.* (Amina alinunua Nafsi 1 umoja njeo iliyopita mzizi kiishio nyama).



Kielelezo matawi hapo juu kinaonyesha usogezi na ukaguzi wa sifa mbalimbali ya sentensi: '*Amina alinunua nama.*' (Amina alinunua nyama). '*Nama*' ambayo ni yambwa

inasogezwa kutoka N ya T' na kuacha athari (ay) hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kinaishia hapo. Kitensi '*alinunua*' husogezwa kutoka T ya T' hadi UPy ya UPy' kukagua sifa ya yambwa na kuacha athari kitensi (at). Kinasogezwa tena hadi NJ ya NJ' kukagua njeo iliyopita ya kitensi hicho na hatimaye husogezwa katika UPk ya UPk' kukagua sifa ya upatanishi kiima na kinabaki hapo. '*Amina*' ni kiima na hivyo kinasogezwa kutoka SPES ya KT na kuacha athari (ak) hadi SPES ya KUPk kukagua sifa ya uhusika kiima na kinabaki hapo.

Sentensi kamili itachukua kielelezo matawi kifuacho katika ukamilifu wake.



(Chomsky, 1995)

2.4 Hitimisho

Katika sura hii maelezo ya baadhi za kazi mbalimbali zilizosomwa kuhusiana na njeo, hali, na dhamira zimeangaziwa kama za Comrie, Mgullu, Bybee na Dahl, Lindfors na Beaudoin. Kazi za sarufi ya Kiswahili Sanifu kama za Waihiga, Mgullu, Ashton na Mohammed zimehakikiwa. Maandiko kuhusu lahaja ya Kitikuu kama kazi ya Nurse na Hinnebusch (1993) imeangaziwa. Kazi mbalimbali zilizosomwa kuhusu nadharia ya Uminimalisti na ukaguzi wa sifa zimeangaziwa vilevile. Msingi wa nadharia ya Uminimalisti; mwasi, historia fupi, mihimili ya nadharia, yote yamemulikiwa kwa urefu. Uminimalisti, jinsi inavyofanya kazi hasa katika lugha zenye ukwasi wa kimofolojia umeelezwa kwa njia sahili na ya kueleweka. Kanuni ya ukaguzi wa sifa, ambayo ndiyo iliyotumika katika kazi hii imeelezewa na mfano kutolewa kuonyesha jinsi ukaguzi unavyofanya kazi.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Kitangulizi

Sura hii inaangazia mbinu za utafiti zilizohusishwa katika ukusanyaji wa data. Utaratibu wa utafiti umeelezwa, uteuzi wa sampuli kwa ajili ya utafiti umefafanuliwa. Mwisho uchanganuzi na uwasilishaji wa data ili kufikia malengo ya utafiti huu yameelezewa.

3.1 Ukusanyaji wa data

Sehemu hii inashughulika na utaratibu wa utafiti, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, vifaa vitakavyotumika na mahali pa kufanya utafiti.

3.1.2 Utaratibu wa utafiti

Utafiti huu unatarajia kutumia umilisi alionao mtafiti kuhusu lahaja ya Kitikuu. Hii ni kutokana na mtafiti kuifahamu lahaja hiyo kwani ndiyo lahaja aliyoitumia tangu udogoni. Maoni haya yanatiliwa nguvu na Chomsky anayeunga mkono ujuzi alionao mzawa wa lugha kama njia ya utafiti. Chomsky anasisitiza kuwa kila mzungumzaji wa lugha yake huwa ana umilisi wa sheria ya sarufi ya lugha hiyo (Chomsky, 1965:79). Vilevile Horrocks, (1987:11) anaonelea kuwa ni sawa kabisa kwa mwanaisimu ambaye ni mzawa wa lugha husika kuijiliza maswali ya kisarufi na kujijibu mwenyewe. Hata hivyo mtafiti anaweza kuongeza na kupunguza kulingana na malengo yake. Kwa hivyo ili kuepukana na hayo, data ilikusanywa kutoka kwa wazungumzaji wengine wa lahaja hiyo.

Wazungumzaji kumi na watano wa lahaja hiyo walichukuliwa kutoka sehemu za Kizingitini, Tchundwa na Faza ili kuthibitisha ukweli wa data. Nilichagua sampuli ya watu kumi na tano kwa sababu ya sehemu tatu ili kila sehemu nipate watu watano.

Nilionelea kuwa idadi hii itatosha katika kujazia pengo pale nitakapokuwa na mushkeli katika utafiti, hasa juu ya matumizi ya viambishi vya njeo, hali na dhamira. Nilichagua sehemu hizo mbalimbali ili kupata data yenyе sampuli kutoka maeneo tofauti yanayozungumza Kitikuu na kuwakilisha hizo sehemu nyingine. Sehemu za mbali kama vile Kiunga, Shanga na Ndau sikuziweka katika sampuli kwa sababu za kiusalama na shida ya usafiri wa sehemu hizo. Matumizi ya hojaji yalitumika, kwa kutafsiri sentensi zilizoandikwa kwa Kiswahili Sanifu hadi kwa lahaja ya Kitikuu.

Vilevile nilitegemea kazi zilizoandikwa na pia mtandao kuhusiana na sarufi na nadharia ili kufidia kazi hii ya utafiti.

3.2.2 Uteuzi wa sampuli

Watu wa umri wa miaka baina ya arobaini na tano hadi sabiini (45-70) ndiyo waliohusishwa katika utafiti huu. Mtafiti alionelea kuwa watu wa umri huo hawana athari kubwa ya Kiswahili Sanifu na lugha nyinginezo, ikilinganishwa na wale wa miaka ya ishirini na thelathini. Hasa nilizingatia wale wazee ambao hawasafiri sana kwenda sehemu nyingine za mwambao kama Lamu, Mombasa, Tanga au sehemu nyengine za ndani ya nchi au nje. Ni wazee ambao mara nyingi wanakaa sehemu za Tikuuni. Watu hao walihojiwa kufuatia matumizi ya hojaji. Nilikuwa na hadhari ya kuwaacha nje wazee sana wa miaka themanini na zaidi, kwa kuhofia wengine wameanza kuchanganyikiwa katika mazungumzo yao na matumizi ya lugha. Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi na mambo ya jinsia hayakuzingatiwa. Angalau sampuli ya watu kumi na tano wa umri huo walihojiwa; watano kutoka Rasini, watano kutoka Tchundwa na watano kutoka Kizingitini.

3.2.3 Mbinu za kukusanya data

Katika utafiti huu tulitumia hojaji kama data msingi, kwa wale wanaojua kusoma na kuandika ili waweze kutafsiri kwa lahaja ya Kitikuu yale yaliyoandikwa kwa Kiswahili Sanifu. Kwa wale wasiojua kuandika, ambao ndiyo wengi, walismewa kwa Kiswahili Sanifu na wakatoa visawe vyake kwa Kitikuu na majibu yaliandikwa na mtafiti na masidizi wake. Vilevile mtahini alitumia umilisi wake kama sehemu ya data msingi vilevile, katika kufidia pale kwenye pengo. Data ya ziada iliweza kukusanya kuitia matumizi ya maktaba na mtandao ili kujazia mwanya, hasa kwa upande wa nadharia na sarufi ya Kiswahili kwa ujumla.

3.2 Uchanganuzi wa data

Katika uchanganuzi wa data tulirejelea hojaji zilizojazwa. Kazi zote zilichunguzwa na kuchanganuliwa kwa minajili ya kupata muundo sahihi wa sarufi ya Kitikuu. Vilevile mtafiti alitumia ujuzi wake alionao kuhusu lahaja hii.

Hatua zifuatazo zilifuatwa katika uchanganuzi wa data:

Hatua ya kwanza ni kuangazia viambishi vya njeo vilivytumika katika Kitikuu vikinganishwa na vile vilivytumika katika hojaji. Kwa hivyo tulipitia hojaji zote kumi na tano tukiangalia hasa visawe vya viambishi vya njeo vilivytumiwa kwa Kitikuu kutoka kwa Kiswahili Sanifu.

Hatua ya pili ilikuwa ni kurejelea kwa upande wa hali na dhamira kuona ni viambishi gani vya hali na dhamira vilivytumiwa katika lahaja ya Kitikuu kutoka kwa Kiswahili Sanifu. Kwa upande wa dhamira tuliangalia sentensi katika dhamira mbalimbali kama arifu, masharti, elezi na agizi.

Hatua ya tatu ni kuangalia mwingiliano wa njeo, hali na dhamira katika lahaja ya Kitikuu. Hatimaye umilisi wa mtafiti pia ulimsaidia katika kuainisha viambishi hivyo na

mwingiliano ili kutumiwa katika mfumo wa uchanganuzi wa kinadharia. Kanuni ya ukaguzi wa sifa ulitumiwa kudhihirisha vile mofimu za njeo, hali na dhamira zinavyokaguliwa katika hatua mbalimbali.

3.2.1 Uwasilishaji wa Data

Data katika utafiti huu iliwasilishwa kwa maelezo, kwa kuonyesha mofimu za njeo, hali na dhamira katika kitenzi cha Kitikuu pamoja na mwingiliano wa mofimu hizo. Mifano mbalimbali ilitolewa na hatimaye mofosintaksia ya sentensi hizo zilionyeshwa kwa michoro matawi kuonyesha vile kanuni ya ukaguzi wa sifa inavyotenda kazi.

3.3 Hitimisho

Sura hii imeangazia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Mbinu za kukusanya data msingi ni matumizi ya hojaji na umilisi wa mtafiti. Mbinu za ziada za kukusanya data ni matumizi ya maktaba na mtandao hasa kwa kazi za sarufi na nadharia ya Uminimalisti. Data ilikusanywa kutoka maeneo ya Kizingitini, Tchundwa na Rasini. Sehemu za mbali na hatari kwa usalama kama Kiunga, Ndau na Shanga ziliachwa nje. Sampuli ilichukuliwa kwa njia ya kimaksudi kwa Watikuu kati ya umri 45 hadi 70. Data ilichanganuliwa kwa kuangazia matumizi ya njeo, hali na dhamira kama zilivyotumika katika hojaji, na ujuzi wa mtafiti nao ukafidia katika uchanganuzi huo.

SURA YA NNE
KITENZI NA MOFOLOJIA YAKE

4.0 Kitangulizi

Sura hii inaangalia kwa urefu kitenzi cha Kitikuu kama lilivyo neno la lazima katika sentensi yoyote ile. Inaangazia aina za vitenzi, mofolojia ya kitenzi; kwani katika aina za maneno, kitenzi ndicho huweza kuambishwa viambishi vingi zaidi na vyta aina mbalimbali, na mwisho kuangazia mpangilio wa maneno katika sentensi za Kitikuu.

4.1 Sarufi ya Kitenzi

Wataaam mbalimbali wakiwemo Habwe na Karanja (2004), Mukwana na Obuchi (2010) na Waihiga (1999) wameiangalia dhana ya kitenzi kuwa ni neno linaloarifu jambo linalotendwa/ linalofanywa na nomino. Kamusi ya Isimu na lugha (1990) pia inaelezea hayo hayo ya kuwa, kitenzi ni aina ya neno ambalo huarifu aina ya tendo linalofanyika. Kwa kiasi fulani, fasili hizi ni sawa, lakini itakuwa tumeacha kando vile vitenzi vyta kuwa na vishirikishi katika fasili hizo. Kwa hivyo, naona fasili hizo zina upungufu na tunaweza kuongezea kwa kusema ya kwamba, kitenzi ni aina ya neno linalotoa maelezo juu ya tendo au hali. Kwa kuongeza, neno hali katika fasili ya kitenzi linahusisha aina za vitenzi vyta kuwa na vitenzi vishirikishi.

- 1a) Ali **ana** shahada ya uzamili.
- 1b) Sophie **ni** mwalimu.
- 1c) Leo **ni** sikukuu.

Maneno yote yaliyokolezwa rangi ni aina za vitenzi ambavyo havionyeshi tendo bali hali fulani.

Kitenzi ni neno muhimu na la lazima katika sentensi ya Kitikuu. Bila kitenzi basi hakuna sentensi. Kitenzi ndilo neno kuu katika kiarifu au kirai tenzi na haliwezi

kukosekana. Tofauti na nomino ambalo ni neno kuu katika kiima, lakini sentensi inaweza kukosa sehemu hiyo ya kiima na sio kiarifu. Mifano:

2a) *Ndokuya.* (Amekuja).

Kitenzi ‘*ndokuya*’ katika Kitikuu kina maana ya ‘amekuja’ katika Kiswahili Sanifu, ni mfano wa sentensi yenye kitenzi pekee. Tofauti na Kiswahili Sanifu, kiambishi cha kiima a- kinaweza kisiambishwe katika kitenzi, kitenzi kinaanza na kiambishi cha hali timilifu **ndo-** bila kiambishi cha kiima **a-**.

2b) *Ndoo.* (Njoo).

2c) *Uiyele.* (Amelala).

4.2 Aina za Vitenzi

Vitenzi huweza kuainishwa kwa kutegemea vigezo mbalimbali kama uamilifu wake, uelekezi, muundo na maana. Kwa mujibu wa kazi hii tutahusisha vigezo tofauti kama vile uamilifu, uelekezi na muundo.

Aina nne kuu za vitenzi:

4.2.1 Vitenzi vikuu

4.2.2 Vitenzi Visoukomu

4.2.3 Vitenzi vishirikishi

4.2.4 Vitenzi visaidizi

4.2.1 Vitenzi Vikuu

Huarifu kuhusu jambo linalofanywa au kufanyiwa nomino (Waihiga, 1999). Vitenzi hivi hueleza matendo katika sentensi yanayofanywa au kufanyiwa kiima. Iwapo vitenzi viwili vimetokea pamoja basi kitenzi cha kwanza ni kitenzi kisaidizi na cha pili ni

kitenzi kikuu. Kitenzi kikuu pia hujulikana kama kitenzi halisi au kitenzi cha kutenda.

Vitenzi vikuu huweza kugawika zaidi katika aina mbili:

- a) Vitenzi elekezi
- b) Vitenzi visoelekezi

4.2.1.1 Vitenzi Elekezi

Vitenzi elekezi ni aina ya vitenzi vyenye kuchukua yambwa ili sentensi iweze kukamilika kimaana. Vitale (1981) anadai kuwa vitenzi elekezi katika sentensi vinaangalia aina ya kirai nomino kitenzi kinaweza kuchukua, hii pia hutegemea mofolioja ya kitenzi. Katika sentensi unaweza kupata nomino ya kiima na nomino ya yambwa, zikichukua nafasi mbalimbali za uamilifu.

- 3a) Juma alifungua mlango.
- 3b) Fatuma anapanda maua.
- 3c) Ahmed alimpiga Badru.

Katika sentensi za 3a,3b na 3c nomino: Juma, Fatuma na Ahmed zina uamilifu wa kiima na nomino: mlango, maua na Badru zina uamilifu wa yambwa (Vitale, 1981:23-24).

Vitenzi elekezi ni aina ya vitenzi vyenye kuchukua yambwa, kwani bila yambwa sentensi hizo hazileti maana. Kwa mfano:

- 3d) * *Mwana hutedhea* (*Mtoto anachezea)
- 3e) * *Baba ndoecha* (*Baba ameleta)

Sentensi hizo hazijakamilika kwani lazima tuongezee yambwa ili sentensi hizo ziweze kukamilika;

Mwana hutedhea basikili. (Mtoto anachezea baiskeli.)

Baba ndoecha chakula. (Baba ameleta chakula.)

Vitenzi elekezi huweza kuchukua yambwa moja au zaidi ya moja. Tunapopata yambwa zaidi ya moja basi moja inakuwa ni yambwa tendewa na ya pili ni yambwa tendwa.

- 4a) *Juma alivunda idirisha.* (Juma alivunja dirisha).

Hapa tunapata yambwa moja tu ambayo ni idirisha.

- 4b) *Juma alinvundia Maria idirisha.* (Juma alimvunjia Maria dirisha).

Katika sentensi ya 4b, tumeongeza viambishi kwenye kitenzi na hivyo kuwa na uwezo wa kuchukua yambwa zaidi ya moja. Viambishi -n- na -i- vimeongezwa katika kitenzi hicho, hivyo kuweza kuchukua yambwa mbili. Katika sentensi hiyo ya 4b), Maria ni yambwa tendewa na idirisha ni yambwa tendwa. Mifano zaidi:

- 4c) *Jumaa alipika chakula.* (Juma alipika chakula)

- 4d) *Hamisi hutedha npira.* (Hamisi anacheza mpira).

- 4e) *Jumaa alinpikia Maria chakula.* (Juma alimpikia Maria chakula).

Sentensi za 4c na 4d zina yambwa moja moja ambazo ni chakula na mpira na sentensi ya (4e) ina yambwa mbili. Yambwa Maria ni yambwa tendewa na chakula ni yambwa tendwa.

4.2.1.2 Vitenzi Visoelekezi

Hivi ni vitenzi vikuu visivyohitaji yambwa ili kukamilisha sentensi. Vitenzi vyta aina hii vinaweza kufuatwa na kielezi au kirai elezi. Mifano ya vitenzi visoelekezi ni kama kuja, kufa, kwenda, lala na kadhalika.

- 5a) *Jumaa alikufa.* (Juma alikufa).

- 5b) *Mwana ndokuya.* (Mtoto amekuja).

- 5c) *Mwanafundi ndoiyala.* (Mwanafunzi amelala).

Kuungezea vielezi au virai elezi tunaweza kupata kama :

- 5d) *Jumaa alikufa yana usiku.* (Juma alikufa jana usiku).

5e) *Mwana ndokuya eo.* (Mtoto amekuja leo).

5f) *Mwanafundi ndoiyala kichandrani.* (Mwanafunzi amelala kitandani).

Maneno **yana usiku**, **eo** na **kichandrani** ni mifano ya vielezi.

Tukitaka kubadilisha vitenzi ambavyo sioelekezi na kuwa elekezi basi lazima tuongeze viambishi.

6a) *Mwana ndoiyala.* (Mtoto amelala).

6b) *Mwana ndoiyalia muto.* (Mtoto amelalia mto).

Sentensi ya (6b) ambayo ni elekezi imeongezwa mofimu {i} ili iweze kuchukua yambwa.

4.2.2 Vitenzi Visoukomu

Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990), inafafanua kitenzi kisoukomu kuwa ni kitenzi kionyeshacho kutobanwa kwa tendo katika hali fulani maalum. Hii ni kumaanisha kuwa vitenzi vya aina hii havionyeshi kuwa tendo linafanywa katika hali gani. Katika lahaja ya Kitikuu, kama vile Kiswahili Sanifu, vitenzi hivi huanza na mofimu **ku-** (au alomofu **kw**) katika hali ya umoja na wingi.

7a) *Alikwenda kunnunulia mwana kitabu.* (Alikwenda **kunnunulia** mtoto kitabu).

7b) *Apenda kutedha sana.* (Anapenda kucheza sana).

7c) *Alipacha kwendra safari.* (Alipata kwenda safari).

Vitenzi visoukomu vina sifa mbalimbali:

i) Vitenzi hivi huweza kuchukua yambwa.

Hapa hufanya kazi kama kitenzi elekezi:

8a) *Apenda kusoma kitabu.* (Anapenda kusoma **kitabu**).

8b) *Atakwenda kunnunulia mwana kitabu.* (Atakwenda kunnunulia **mtoto kitabu**).

ii) Vitenzi hivi havichukui viambishi vya njeo na hali. Viambishi vya njeo na hali vinaweza kuchukuliwa katika vitenzi visaidizi au vitenzi vikuu lakini sio katika kitenzi kisoukomo.

- 9a) *Mwidhi ataka kufa.* (Mwizi ataka kufa.)
- 9b) *Hamisi awedha kusoma Kiswahili.* (Hamisi aweza kusoma Kiswahili).
- 9c) *Alitakikana kwendra kochini yana.* (Alitakikana kwenda kotini jana.)

iii) Vokali ya mwisho katika vitenzi visoukomo inabaki **-a**.

Kuimba, kutedha, kupika, kusoma, kuchora na kadhalika

iv) Vitenzi visoukomo huweza kufanya kazi kama kitenzi na pia kama nomino kutegemea namna kinavyotumiwa katika sentensi. Nomino ya **ku-** hupatikana katika ngeli ya 15 katika Kitikuu na pia katika Kiswahili Sanifu. Inapotumiwa kama nomino basi hufanya kazi kama nomino yoyote ile, na mofimu {**ku**} haibadiliki katika umoja na wingi.

- 10a) *Kusoma sana kundonfanya afaulu.* (Kusoma sana kumemfanya afaulu).
- 10b) *Ukarimu ni kutoa.* (Ukarimu ni kutoa).
- 10c) ***Kuimba** kwavo kulichufurahisha.* (Kuimba kwao kulitufurahisha).

Kama vitenzi vingine, vitenzi visoukomo huweza kufanya kazi kama vitenzi vyoyote vile kwa mfano kunyambuliwa katika hali mbalimbali; kusomea, kutedhesha, kuimbana.

Vilevile huweza kubeba viambishi vya mtendwa/kitendewa. **Kumpondra** (kumpiga), **kukitedhesha** (kukichezesha), **kuvavonea** (kuwaonea). Katika sentensi vitenzi visoukomo huweza kuchukua vielezi; Alikwendra kuimba **mapema**. (Alikwenda kuimba mapema.), Ataka kutedha **sana** (Ataka kucheza sana).

4.2.3 Vitenzi Vishirikishi

Vitenzi vishirikishi ni aina ya vitenzi vinavyoshirikisha kiima na kijalizo chake. Ni aina ambayo haihitaji tendo lolote bali hueleza hali zingine ambazo si matendo. Kama Kamusi ya Isimu na Lughu (1990:18) inavyodai kuwa ni aina ya kitenzi kisicho na uarifu kamili, ambacho huhitaji kijalizo cha kiima ili kukamilisha maana. Mara nyingi kijalizo huwa ni nomino nyingine, kiwakilishi au kivumishi kinachoelezea juu ya kiima. Kama vile ambavyo sentensi elekezi hubeba yambwa basi vitenzi vishirikishi hubeba kijalizo. Kijalizo huweza kuwa kimoja au zaidi.

- 11a) *Hamisi ni mwalimu.* (Hamisi ni mwalimu).
- 11b) *Hamisi ndriye mwalimu ndhuri.* (Hamisi ndiye mwalimu mzuri).
- 11c) *Mariamu si tajiri sana.* (Mariamu si tajiri sana).

Vitenzi vishirikishi huweza kugawanywa katika sehemu mbili kuu:

- a) Vitenzi vishirikishi vya **kuwa**
- b) Vitenzi vishirikishi vya **kuwa na**

4.2.3.1 Vitenzi vishirikishi vya kuwa

Vitenzi vya kuwa ni aina ya vitenzi vishirikishi vinavyofanya kazi ya kushirikisha kiima na kijalizo katika sentensi kwa kuonyesha hali ya kuwa. Mifano ya vitenzi hivi ni kama: **ni, kuwa, yu, ndi-** na pia vya mahali kama **po,ko,mo.**

- 12 a) *Halima ni daktari.* (Halima ni daktari).
- 12 b) *Alii alikuva mwalimu.* (Ali alikuwa mwalimu).
- 12 c) *Hamisi ndriye mwidhi.* (Hamisi ndiye mwizi).

Katika kuzikanusha sentensi hizo za vitenzi vya kuwa, bado hali hiyo itajitokeza:

- 12d) *Halima si daktari.* (Halima si daktari).
- 12e) *Alii hakuva mwalimu.* (Ali hakuwa mwalimu).
- 12f) *Hamisi siye mwidihi.* (Hamisi siye mwizi).

4.2.3.2 Vitenzi Vishirikishi vyatika na

Aina hii ya vitenzi vishirikishi huonyesha ile hali ya kumiliki. Vitenzi vinavyoweza kupatikana katika aina hii ni pamoja na: **kuwa na**, na **-na**. Hapa vitenzi vyatika na vitachukua viambishi vyatika njeo na hali mbalimbali pamoja na viambishi vyatika nafsi au upatanishi. Na vitenzi vyatika **-na** vitachukua viambishi vyatika upatanishi kutegemea ngeli za nomino husika.

Yakinishi

- | | |
|--|---|
| 13a) <i>Maria ana kitabu.</i> (Maria ana kitabu) | <i>Maria hana kitabu.</i> (Maria hana kitabu) |
| 13b) <i>Kitabu kina veneve.</i> (Kitabu kina wenyewe.) | <i>Kitabu hakina veneve.</i> (Kitabu hakina wenyewe.) |
| 13c) <i>Hamisi alikuva na numba kuru.</i> (Hamisi alikuwa na nyumba kubwa). | <i>Hamisi hakuva na numba kuru.</i> (Hamisi hakuwa na nyumba kubwa). |

Ukanushi

4.2.4 Vitenzi Visaidizi

Aina hii ya vitenzi hufanya kazi ya kusaidia kitenzi kikuu katika kukamilisha ujumbe katika sentensi. Yaani ni aina ya kitenzi kinachosaidia kitenzi kikuu katika kukamilisha wazo au ujumbe fulani. Vitenzi visaidizi katika sentensi hutangulia vitenzi vikuu. Vitenzi visaidizi huweza kubeba viambishi vyatika upatanishi, vyatika njeo na hali na vyatika yakinishi au ukarusha kutegemea ujumbe unaotolewa. Mifano ya vitenzi visaidizi ni kama **weza, kuwa, pata, kuja, taka, kwenda na kwisha** (Mohammed, 2004).

Yakinishi

- | | |
|--|--|
| 14a) <i>Huri alikuva akitedha mpwira.</i> (Huri alikuwa akicheza mpira). | <i>Huri hakuva akitedha mpwira.</i> (Huri hakuwa akicheza mpira). |
| 14b) <i>Mwalimu awedha kusikilia mapema eo.</i> (Mwalimu aweza kufika mapema leo) | <i>Mwalimu hawedhi kusikilia mapema eo.</i> (Mwalimu hawezikufika mapema leo) |

Ukanushi

14c) *Salimu alipacha kuandroka mapema.* *Salimu hakupacha kuandroka mapema.*

(Salimu alipata kuondoka mapema) (Salimu hakupata kuondoka mapema).

14d) *Atakuya mapema kusomesha kesho.* *Hayi mapema kusomesha kesho.*

(Atakuja mapema kusomesha kesho). (Hatakuja mapema kusomesha kesho).

Kulingana na mifano ya aina mbalimbali za vitenzi tunaweza kujua ni aina gani pindi vinapotumiwa katika sentensi. Kwa mfano kitenzi kama **kuwa** tunasema ni kitenzi kisaidizi lakini pia kikitumika kama kishirikishi kinakuwa ni kitenzi kishirikishi.

14e) *Mwana alikuva husoma.* (Mtoto alikuwa anasoma).

Hapa ni kitenzi kisaidizi.

14f) *Mwana alikuva hodari.* (Mtoto alikuwa hodari)

Hapa kimetumika kama kitenzi kishirikishi.

4.3 Mpangilio wa Maneno

M pangilio wa maneno hurejelea jinsi lugha inavyopanga maneno yake katika sentensi.

Yaani mpangilio wa kiima, kitenzi na yambwa. Kitikuu kama Kiswahili Sanifu na lugha nyingi za kibantu, hupanga maneno yake kawaida kwa mpangilio wa kiima, kitenzi na yambwa. (SVO- KKY).

15a) *Tabitha alimpondra Halima.* (Tabitha alimpiga Halima).

15b) *Vana valitedhea dhidude.* (Watoto walichezea vidude).

15c) *Mwana ataka chakula.* (Mtoto ataka chakula).

Hata hivyo mpangilio wa maneno katika Kitikuu, kama katika Kiswahili Sanifu, huweza kubadilika kutegemea pale tunapotilia mkazo au aina ya habari tunayotoa (Vitale, 1981:19).

16a) *Vaimbaji valiimba nyimbo ningi.* (Waimbaji waliimba nyimbo nyingi). (KKY,

SVO)

16b) *Nyimbo ningi vaimbaji valiimba.* (Nyimbo nyingi waimbaji waliimba).

(YKK,OSV)

16c) *Kalamu, mwana hutedhea.* (Kalamu, mtoto huchezza). (YKK, OSV)

4.4 Mofolojia ya Kitenzi cha Kitikuu

Mofolojia ni kiwango kimojawapo cha isimu kinachohusika na maumbo ya maneno.

Mofolojia hugawika katika makundi mawili makuu: mofolojia mnyambuliko na mofolojia uundaji. Hapa tutaangalia mofolojia ya kitenzi kwa kurejelea viambishi (mofimu) mbalimbali vinavyounda kitenzi cha Kitikuu. Kazi hii ya ukaguzi wa sifa hutilia maanani mofolojia ya maneno, na kwa vile tunaangalia kitenzi cha Kitikuu hatuna budi kuangazia kwa kina mofolojia ya kitenzi hicho cha Kitikuu.

Kitenzi cha Kitikuu, kama vile kitenzi cha Kiswahili Sanifu kinaweza kuambishwa mofimu mbalimbali zikiwa na majukumu mbalimbali. Kwa hivyo kitenzi cha Kitikuu ni aina ya maneno ambayo ni ambishi hivyo katika mzizi wake viambishi mbalimbali huweza kuambishwa.

Kitenzi cha Kitikuu huchukua viambishi awali na viambishi tamati. Viambishi awali hupatikana kabla ya mzizi wa kitenzi na viambishi tamati hupatikana baada ya mzizi wa kitenzi. Kitikuu hakina viambishi kati, kwani kiambishi kati hupatikana ndani ya mzizi wa kitenzi.

4.4.1 Viambishi awali vyta kitenzi

Kama tulivyotangulia kusema, viambishi awali ni aina ya viambishi vinavyopatikana kabla ya mzizi wa neno. Kitenzi cha Kitikuu kina viambishi awali vyta aina mbalimbali navyo ni:

4.4.1.1 Viambishi vya upatanishi au mofimu za upatanishi

Viambishi vya upatanishi hubadilika kulingana na neno linalopatanishwa. Hapa tunapata viambishi vya aina mbili, viambishi vya nafsi na viambishi vya upatanishi wa ngeli.

i) Viambishi vya nafsi

Tukianza na viambishi vya nafsi, vitenzi vya Kitikuu huchukua viambishi vya nafsi tofauti tofauti:

Nafsi ya kwanza

Katika nafsi ya kwanza umoja, Kitikuu huchukua mofimu {ni} na alomofu {na}

- 17a) *Na - li - kwendr - a sipichali.* (Nilikwenda hospitali).

| | | | |
|------------------|-------------------|-------|---------|
| Nafsi 1 umoja | njeo iliyopita | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|-------|---------|

- 17b) *Ni a - tak - a ku - l - a sasa.* (Ninataka kula sasa).

| | | | | | | |
|------------------|-----------------|-------|---------|--------------------------|-------|---------|
| Nafsi 1 umoja | njeo iliyopo | mzizi | kiishio | kiambishi cha kitenzi | mzizi | kiishio |
| | | | | kisoukomodo | | |

Katika sentensi (17b) mageuko ya kifonolojia yanajitokeza kwa kudondosha vokali ya kwanza /i/ ili kurahisisha matamshi:

/i/ → /∅/ / -a/

/ni - a - tak - a/ → /nataka/

Katika nafsi ya kwanza wingi hutumia mofimu {chu-} pia alomofu {chwa-}

- 17c) *Chu - ta - imb - a kesho usiku.* (Tutaimba kesho usiku).

| | | | |
|------------------|---------------|-------|---------|
| Nafsi 1 wingi | njeo ijayo | mzizi | kiishio |
|------------------|---------------|-------|---------|

- 17d) *Chwa - li - ku - l - a chakula chote.* (Tulikula chakula chote).

| | | | | |
|------------------|-------------------|----------------------|-------|---------|
| Nafsi 1 wingi | njeo iliyopita | kiambishi cha ku* | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|----------------------|-------|---------|

* Kiambishi ku hutumika kama kiambishi cha kitenzi kisoukomodo lakini pia hutumika na kitenzi cha silabi moja, hapa kimetumika kwa muktadha huo wa kusaidia kitenzi cha silabi moja.

Nafsi ya pili:

Katika nafsi ya pili umoja Kitikuu hutumia mofimu {u-}

18a) *U - ta - kw- endr - a sokoni kesho?* (Utakwenda sokoni kesho?)

| | | | | |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|
| Nafsi 2 umoja | njeo ijayo | kiambishi cha ku | mzizi | kiishio |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|

18b) *U - li - m - pondr - a kwa nguvu sana.*

| | | | | |
|------------------|-------------------|--------------------------|-------|---------|
| Nafsi 2 umoja | njeo iliyopita | kiambishi cha mtendwa | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|--------------------------|-------|---------|

(Ulimpiga kwa nguvu sana.)

Nafsi ya pili wingi Kitikuu hutumia mofimu {mu-}

19a) *Mu - ta - kw- endr - a sokoni kesho?* (Mutakwenda sokoni kesho?)

| | | | | |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|
| Nafsi 2 wingi | njeo ijayo | kiambishi cha ku | mzizi | kiishio |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|

19b) *Mu - li - va- pondr - a kwa nguvu sana.* (Muliwapiga kwa nguvu sana).

| | | | | |
|------------------|-------------------|---------|-------|---------|
| Nafsi 2 wingi | njeo iliyopita | mtendwa | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|---------|-------|---------|

Nafsi ya tatu

Katika lahaja ya Kitikuu mofimu ya nafsi ya tatu umoja inayotumika ni {a-}, au {ø}

20a) *Mwalimu a - ta - ku - y - a saa nane.* (Mwalimu atakuja saa

| | | | | | |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|--------|
| Nafsi 3 umoja | njeo ijayo | kiambishi cha ku | mzizi | kiishio | nane). |
|------------------|---------------|---------------------|-------|---------|--------|

20b) *Hamisi a - tak - a ku - fu - a ngovo.* (Hamisi ataka kufua

| | | | | | | |
|------------------|--------|---------|-----------|-------|---------|--------|
| Nafsi 3 umoja | mzizi | kiishio | kiambishi | mzizi | kiishio | nguo). |
| | cha ku | | | | | |

Katika sentensi hizo 20a) na 20b) mofimu ya kiima {a} huweza kudondoshwa, kwa vile nomino za kiima Mwalimu na Hamisi zipo kwa Kitikuu, sio lazima kuwa na mofimu ya upatanishi kiima hiyo ya umoja, na ndiyo sentensi hizo zinaweza pia kuwa:

21a) *Mwalimu* **ø** - ta- ku- y- a ku- som – esh - a saa nane.

21b) *Hamisi* **ø** – tak- a ku – fu- a nguvo.

Katika nafsi ya tatu wingi mofimu {**va-**} hutumika katika lajaja ya Kitikuu.

22a) *Vana vote* **va** - ta - safir- i kesho. (Watoto wote watasafiri kesho.)

| | | | |
|------------------|---------------|-------|---------|
| Nafsi 3 wingi | njeo ijayo | mzizi | kiishio |
|------------------|---------------|-------|---------|

22b) *Vanafundi* **va** - li- imb - a wimbo wa taifa.

| | | | |
|------------------|-------------------|-------|---------|
| Nafsi 3 wingi | njeo iliyopita | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|-------|---------|

(Wanafunzi waliimba wimbo wa taifa).

ii) Viambishi vya upatanishi vya ngeli / Mofimu za upatanishi

Viambishi vya ngeli za kisintaksia pia huainishwa kama viambishi awali katika kitenzi cha Kitikuu. Hivi ni viambishi vinavyochukua upatanishi wa nomino husika. Jedwali la 5 hapo chini linaonyesha viambishi vya kisintaksia kulingana na upatanishi wake.

Jedwali 5

Viambishi vya Upatanishi vya Ngeli

| Nambari ya Ngeli | Ngeli za kimofolojia | Viambishi vya upatanishi | Mifano katika sentensi |
|-------------------------|-----------------------------|---------------------------------|---|
| 1 | n -, mu- | a- | Mwana a -li-ku 1-a wali.(Mtoto alikula wali). |
| 2 | va- | va- | Vana va -li-ku-la wali. (Watoto walikula wali). |
| 3 | n-, mu- | u- | Nnadhi u -li-kach- w-a yana. (Mnazi ulikatwa jana). |
| 4 | mi- | i- | Minadhi i -li-kach-w-a yana. (Minazi ilikatwa jana). |
| 5 | i- | li - | Igego li -ndo- tok a. (Gego limetoka). |
| 6 | ma- | a- | Magego a -ndo-tok-a. (Magego yametoka) |
| 7 | ki- | ki- | Kichi kipiya ki -ta-nunu-liw-a. (Kiti kipyा kitanunuliwa). |
| 8 | dhi- | dhi- | Dhichi dhipiya dhi -ta-nunu-liw-a. (Viti vipyा vitanunuliwa). |
| 9 | n- | i- | Nguvo i -li-shon-w-a yana na fundi. (Nguvo ilishonwa jana na fundi.) |

| | | | |
|-----|-------|------|---|
| 10 | n- | dhi- | Nguvo dhi -li-shon-w-a yana na fundi. (Nguo zilishonwa jana na fundi.) |
| 11 | u- | u- | Udhi u -li-kach-ik-a mara mbili. (Uzi ulikatika mara mbili.) |
| 10a | n- | dhi- | Nyudhi dhi -li-kach-ik-a mara mbili. (Nyuzi zilikatika mara mbili.) |
| 11a | u- | u- | Ugonjwa huu u -ndo-n-kondr-esha. (Ugonjwa huu umemkondesha.) |
| 6a | ma- | a- | Magonjwa haa a -ndo-va-kondr-esha. (Magonjwa haya yamewakondesha). |
| 14 | vu,u- | u- | Udhivu u -ndo-n-koresha kadhi. (Uvivu umemkoresha kazi). |
| 15 | ku- | ku | Kuimba kwake ku -li-mw-ech-ea senti ngingi. (Kuimba kwake kulimletea pesa nyingi.) |
| 17 | pa- | pa- | Mahali pa -li-saf-ish-w-a kwa udhuri. (Pahali palisafishwa vizuri). |
| 18 | ku- | ku- | Mahali kwake ku -ndo-ket-iw-a na vachu. (Mahali kwake kumekaliwa na watu). |

4.4.1.2 Viambishi vya Ukanushi / Mofimu za Ukanushi

Kamusi ya Isimu na lugha (1990) inafasili ukanushi kuwa ni mfanyiko wa kufanya sentensi isiwe yakinishi.

Pei (1968) akinukuliwa na Mdee (1986:55) anadai; Ni umbo lenye kukana tendo lililoelezwa na kitenzi. Kwa hivyo ukanushi ni ile hali ya kuifanya sentensi kutokuwa yakinishi, ijapokuwa aina nyingine za maneno (kama nomino, vivumishi, vielezi) zinaweza pia kufanya kanushi kama anavyodai Mdee (1986). Kwa lengo la kazi hii, tutajikita tu katika vitenzi vya Kitikuu. Vilevile ukanushi unaweza kuonyeshwa na maneno mbalimbali kama vile hapana na la, lakini kwa mujibu wa kazi hii, tunaangalia mofolojia ya kitenzi kwa hivyo hatutaangalia leksia hizo za ukanushi. Tutajikita zaidi na mofimu za kitenzi zinazohusika na kuleta ukanushi katika Kitikuu.

Mofimu tatu ndizo zinazohusika zaidi katika kuleta ukanushi katika Kiswahili, ambazo ni **ha-, -si- na -to**. Katika Kitikuu, mofimu hizo za ukanushi; {**ha**} na {**si**} ndizo hutumika sana, ambazo ni mofimu zinazotangulia nafsi au huchukua mahali pa nafsi na pia ngeli za upatanishi. Kwa kiasi kidogo mofimu {**to**} hutumika kwa kukanusha vitenzi

visoukomu au vitenzi jina. Kuna mofimu nyingine zinazoongezewa kwenye ukanushi ambazo ni mofimu za kukanusha njeo au hali kama ya **-i**, **-ja-** na **ku** katika Kiswahili Sanifu (Beaudoin, 1999). Katika Kitikuu viambishi vya ukanushi vya njeo, hali na dhamira ni pamoja na: mofimu **{ya}** ya kukanusha hali timilifu **{ndo}**, mofimu **{ku}** ya kukanusha njeo iliyopita **{li}** na mofimu tamati **{i}** hukanusha kutegemea njeo au hali inayotumika. Vilevile mofimu tamati **{-ε}** pia hutumika kwa dhamira amrishi na tegemezi katika ukanushi. Dhamira **{ngali}** katika Kitikuu hukanushwa kwa kutanguliwa na mofimu **{si}**, na dhamira ya masharti **{ki}** hutumia mofimu **{sipo}**.

a) Mofimu **{si-}**

Mofimu **{si-}** hutumiwa katika ukanushi wa nafsi ya kwanza umoja, na vitenzi vya dhamira ya amri au ombi na vitenzi vya dhamira tegemezi. Mofimu **{si}** inaweza kusimama kama mofimu tegemezi au mofimu huru. Mofimu tegemezi **{-si-}** hutumiwa kama kiambishi awali katika kitenzi, kuonyesha ukanushi wa nafsi na mofimu huru **{si}** hutumika kukanusha kitenzi kishirikishi **ni**. Kwa mujibu wa kazi hii mofimu tegemezi **{si-}** ndiyo itakayoshughulikiwa zaidi. Mofimu **{si-}** haiwezi kutumiwa pamoja na mofimu **{ha-}** katika kitenzi kimoja.

Mifano ifuatayo huonyesha matumizi ya mofimu **{si}** ya ukanushi:

Jedwali 6

Kiambishi si- cha ukanushi

| | Nafsi Yakinishi | Njeo, hali, dhamira | Sentensi | Nafsi Kanushi | Sentensi | | |
|---|----------------------------|------------------------------------|-----------------|---|-----------------|---|---|
| 1 | Ya umoja | 1 | Iliyopita | <i>Yana na-li-anguk-a.</i> (Jana nilianguka). | Ya umoja | 1 | <i>Yana si-ku- anguk-a.</i> (Jana sikuanguka). |
| 2 | Ya umoja | 1 | Ijayo | <i>T'a-ku-y-a kesho.</i> (Nitakuja kesho). | Ya umoja | 1 | <i>Si-y-i kesho.</i> (Sitakuja kesho). |
| 3 | Ya umoja | 1 | Mazoea | <i>Imi hu-l-a wali.</i> (Mimi hula wali) | Ya umoja | 1 | <i>Imi si-li wali.</i> (Mimi sili wali). |
| 4 | Ya umoja | 1 | Timilifu | <i>Ni-ndo-ku-l-a wali ote.</i> (Nimekula wali wote.) | Ya umoja | 1 | <i>Si-ya-l-a wali ote.</i> (Sijakula |

| | | | | | wali wote.) | | |
|----|-------------|---|-----------|--|-------------|---|---|
| 5 | Ya umoja | 1 | Kuendelea | <i>Hupika bodo na isi.</i> (Ninapika sima na samaki). | Ya umoja | 1 | <i>Si-pik-i bodo na isi.</i> (Sipiki sima na samaki). |
| 6 | Ya umoja | 2 | Amrishi | <i>Pik-a!</i> | Ya umoja | 2 | <i>U-si-pik-e</i> |
| 7 | Ya wingi | 2 | Amrishi | <i>Pik-an-i!</i> (Pikeni!) | Ya wingi | 2 | <i>Mu-si-pik-e!</i> (Msipike!) |
| 8 | Ya umoja | 2 | Tegemezi | <i>U-l-e chakula.</i> | Ya umoja | 2 | <i>U-si-l-e chakula.</i> (Usile chakula) |
| 9 | Ya wingi | 2 | Tegemezi | <i>Mu-l-e chakula.</i> (Mle chakula) | Ya wingi | 2 | <i>Mu-si-l-e chakula.</i> (Msile chakula) |
| 10 | Ya umoja | 3 | Tegemezi | <i>A-l-e wali.</i> (Ale wali). | Ya umoja | 3 | <i>A-si-l-e wali.</i> (Asile wali). |
| 11 | Ya wingi | 3 | Tegemezi | <i>Va-l-e wali.</i> (Wale wali) | Ya wingi | 3 | <i>Va-si-l-e wali.</i> (wasile wali) |
| 12 | | | Masharti | <i>A-ngali-ku-y-a angalikula wali.</i> (Angelikuja angelikula wali.) | | | <i>A-si-ngali-ku-y-a a-si-ngali-ku-l-a wali. Asingelikuja asingelikula wali.)</i> |

Katika Kitikuu, tofauti na Kiswahili Sanifu katika ukanushi wa njeo ijayo, mofimu ya ukanushi **{ta}** haitumiki, hudondoshwa kama ilivyo katika hali ya kuendelea au njeo iliyopo.

23a) *Ni- ta- ku- y- a kesho - Si- y- i kesho.*
 Nafsi 1 njeo kiambishi mzizi kiishio nafsi 1 mzizi kiishio cha
 umoja ijayo cha ku umuja kanushi ukanushi
 (Nitakuja kesho - Sitakuja kesho.)

Katika hali timilifu **{ja}** ya ukanushi katika Kiswahili Sanifu, hubadilika **{ya}** kwa Kitikuu:

23b) *Ni- ndo- ku- l- a wali. Si- ya - l - a wali.*
 Nafsi 1 hali kiambishi mzizi kiishio Nafsi 1 umoja ukanushi mzizi kiishio
 umoja timilifu cha ku kanushi hali timilifu
 (Nimekula wali). (Sijakula wali).

b) Mofimu {ha-}

Mofimu {ha-} ndiyo inayotumika sana katika ukanushi wa vitenzi vyta Kitikuu. Mofimu {ha-} hutumiwa kwa ukanushi wa nafsi zote arifu, isipokuwa nafsi ya kwanza umoja, na ukanushi wa ngeli nyingine zote za upatanishi (mkabala wa kisintaksia), hutumia mofimu {ha}:

Yakinishi

Kanushi

24a) Chwa- li- imb- a (Tuliimba) **Ha-** chu- ku- imb- a (Hatukuimba).

| | | | | | | | | |
|---------|-----------|------|---------|-----------|---------|----------|-----------|---------|
| Nafsi 1 | njeo | mziz | kiishio | kiambishi | nafsi 1 | ukanushi | mzizi | kiishio |
| wingi | iliyopita | | | kanushi | wingi | njeo | iliyopita | |

24b) U- ta- som- a **Hu-** som - i (Hutasoma)

| | | | | | | |
|---------|-------|-------|---------|-----------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | njeo | mzizi | kiishio | kiambishi | mzizi | kiishio cha |
| umoja | ijayo | | | kanushi | wingi | ukanushi |

24c) Mu- li- tedh- a (Mlicheza) **Ha -** mu- ku- tedh- a (Hamkucheza)

| | | | | | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|-----------|--------|----------|-----------|---------|
| Nafsi 2 | njeo | mzizi | kiishio | kiambishi | nafsi2 | ukanushi | mzizi | kiishio |
| wingi | iliyopita | | | kanushi | wingi | njeo | iliyopita | |

24d) A - ta- imb- a **Ha -** imb- i (Hataimba)

| | | | | | | |
|---------|-------|-------|---------|-----------|-------|-------------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kiishio | kiambishi | mzizi | kiishio cha |
| umoja | ijayo | | | kanushi | wingi | ukanushi |

25e) Va - li - ku - l- a (Walikula) **Ha -** va - ku - l- a (Hawakula)

| | | | | | | | | | |
|----------|-------|-----------|-------|---------|-----------|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi ya | njeo | kiambishi | mzizi | kiishio | kiambishi | nafsi 3 | kiambishi | mzizi | kiishio |
| 3 wingi | ijayo | ku | | | kanushi | wingi | cha ku | | |

Katika mfano wa 24b) kiambishi {hu-} kimetumika badala ya {ha-} kwa sababu ya mabadiliko ya kimofofonolojia ambapo {ha-} ya ukanushi ikifuatwa na {u}, basi kunatokea udondoshi wa vokali ya kwanza ambayo ni {a}.

/ha-u-som-i/ → [hu-som-i]

Sheria: /a/ → [∅] / -/u/

Vilevile mofimu ya njeo ijayo katika ukanushi haitumiki, tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo mofimu {ta} ya njeo ijayo huwekwa katika ukanushi, kama mfano 24b) na 24d) unavyoonyesha.

Katika ukanushi wa ngeli mbalimbali, mofimu **{ha-}** ya ukanushi ndiyo inayotumika mwanzoni.

Yakinishi

25a) *Muembe u - li - anguk - a*

Kipatanishi njeo mzizi kiishio
cha ngeli iliyopita

(Mwembe ulianguka)

Kanushi

Muembe ha- u - ku- anguk- a

kiambishi kiambishi ukanushi mzizi kiishio
cha ukanushi cha ngeli njeo iliyopita

(Mwembe haukuanguka).

25b) *Asali i- ndo- suk- a.*

Kiambishi hali mzizi kiishio
cha ngeli timilifu

(Asali imemwagika.)

Asali ha- i- ya- suk- a.

kiambishi kiambishi ukanushi mzizi kiishio
kanushi cha ngeli hali timilifu

(Asali haijamwagika.)

25c) *Kichi ki- ta- chengedh- w- a.*

Kiambishi njeo mzizi kauli kiishio
cha ngeli ijayo ya kutendwa

(Kiti kitatengenezwa)

Kichi ha- ki- chengedh - w - i.

kiambishi kiambishi mzizi kauli kiishio
kanushi cha ngeli ya kutendwa

(Kiti hakitatengenezwa)

Hapa tunaangalia tu viambishi vya ukanushi vya awali, yaani kabla ya mzizi, ambavyo tumesema katika Kitikuu, kama Kiswahili Sanifu ni **{si}**, **{ha}** na **{to}**. Kuna viambishi vya ukanushi ambavyo ni tamati, yaani vinapatikana baada ya mzizi wa kitenzi, navyo ni **{e}** na **{i}**, vitaangaziwa chini ya viambishi tamati. Vilevile, katika ukanushi, kutegemea njeo hali na dhamira viambishi vyake hubadilika kwa njia mbalimbali na hivyo vitaangaziwa katika uchambuzi wa njeo, hali na dhamira baadaye kwa urefu zaidi.

c) Mofimu {-to-}

Mofimu **{-to-}** katika ukanushi hutumika katika aina ya vitenzi visoukomu. Katika vitenzi visoukomu vya Kitikuu kama vile Kiswahili Sanifu huanza na kiambishi **ku-**. Katika ukanushi kiambishi **ku-** hubakishwa kikifuatiwa na kiambishi **-to-** cha ukanushi.

Yakinishi

26a) *Ku - tedh - a* (Kucheza).

Kiambishi mizizi kiishio
cha kitenzi kisoukomu

Kanushi

Ku- to- tedh- a (Kutocheza).

Kiambishi kiambishi mzizi kiishio
cha kitenzi kanushi kisoukomu

26b) *Ku - imb - a* (Kuimba). *Ku- to- imb- a* (Kutoimba).

Kiambishi mizizi kiishio
cha kitenzi
kisoukomu

Kiambishi kiambishi mzizi kiishio
cha kitenzi kanushi
kisoukomu

26c) *Ku - pik - a* (Kupika). *Ku - to- pik - a* (Kutopika).

Kiambishi mizizi kiishio
cha kitenzi
kisoukomu

Kiambishi kiambishi mzizi kiishio
cha kitenzi kanushi
kisoukomu

Katika Kitikuu hali ya ukarusha ya vitembi visoukomu havitumiki sana, katika hali yakinishi ndiyo vinatumika zaidi. Iwapo vitembi visoukomu vimetumika na vitembi visaidizi au vitembi vikuu, basi vitembi visaidizi au vitembi vikuu ndivyo vinavyokarusha. Isipokuwa pale tu kitenzi kisoukomu kinapotumika peke yake bila kitenzi kingine, ndipo kitenzi kisoukomu hukanusha .

Yakinishi

26d) *Amina apenda kulia.*

Kanushi

Amina hapendi kulia.

26e) *Sarah awedha kuimba.*

Sarah hawedhi kuimba.

(Sarah anaweza kuimba.)

(Sarah hawezo kuimba).

26f) *Vachu vataka kula.*

Vachu havataki kula.

(Watu wataka kula)

(Watu havataki kula).

Kitenzi kisoukomu kinapotumika na kitenzi-jina katika sentensi, hali ya ukarusha pia hubadilika kwani kitenzi jina kinatumika katika muktadha huo wa sentensi kama nomino na kitenzi kinachofuata kisoukomu hukanusha kwa njia tofauti. Kitenzi kisoukomu **ku** hubakishwa, na njeo au hali husika ndiyo inayokarusha.

Yakinishi

27a) *Ku- imb- a kw - ake - ku- li- chu - furah- ish- a.*

Kiambishi mizizi kiishio kiambishi ku kimilikishi kiambishi njeo iliyopita nafsi 1 mzizi kauli ya kiishio
kitenzi-jina upatanishi kitenzi kisoukomu wingi kufanyisha

(Kuimba kwake kilitufarahisha.)

Kanushi

Ku- imb- a kw- ake ha- ku- ku- chu- furah- ish- a.

Kiambishi mzizi kiishio kiambishi kimilikishi kiambishi kiambishi kanushi nafsi 1 mzizi kauli ya kiishio
kitenzi-jina upatanishi ku kanushi kitenzi njeo wingi kisoukomo iliyopita kufanyisha

(Kuimba kwake hakukutufurahisha.)

Yakinishi

27b) *Ku- tedh- a kw- ake ku - ndo - mu- harib- i- a .*

Kiambishi mzizi kiishio kiambishi kimilikishi kiambishi hali timilifu mtendwa mzizi kauli ya kiishio
Kitenzi-jina kipatanishi kitenzi kisoukomo kufanyia

(Kucheza kwake kumemuharibia.)

Kanushi

Ku- tedh- a kw- ake ha- ku- ya - mu- harib- i- a.

kiambishi mzizi kiishio kiambishi kimilikishi kiambishi kiambishi ukunushi mtendwa mzizi kauli kiishio
kitenzi-jina kipatanishi kanushi kitenzi hali timilifu ya kufanyia

(Kucheza kwake hakujamharibia.)

Kiambishi cha ukunushi cha kimilikishi kw- ake, kimepitia mageuko ya kifonolojia, kwani mofimu hiyo ya upatanishi ni {ku} kulingana na kitenzi-jina ku-tedha. Uundaji wa kiyeyushi {w} unajitokeza pale vokali /u/ inapopakana na vokali nyengine isiyokuwa /u/, aghalabu, huunda kiyeyusho /w/ katika lahaja hii.

/u/ → /w/ / - /v/

Hapa /v/ inasimamia vokali yoyote nyengine katika Kitikuu, yaani; /a,ε, i ɔ / inaweza kuleta hayo mabadiliko ya uundaji wa kiyeyushi /w/, isipokuwa kwa vokali /u/.

4.4.1.3 Viambishi Rejeshi (Mofimu rejeshi)

Mofimu za urejeshi au viambishi vya urejeshi hurejelea nomino ambayo huwa imetajwa kabla ya kitenzi chenyewe kutajwa. Katika lahaja ya Kitikuu, kama Kiswahili Sanifu kuna mofimu za urejeshi awali na pia tamati. Hapa tutaangalia viambishi awali vya

urejeshi katika kitenzi cha Kitikuu. Mofimu hizi za urejeshi hutegemea ngeli ya nomino inayorejelewa.

Jedwali 7

Viambishi vya Urejeshi katika Kitikuu

| Ngeli | Ngeli ya kimofolojia | Ngeli ya kisintaksia | Mofimu ya urejeshi | Mifano katika sentensi |
|-------|----------------------|----------------------|--------------------|---|
| 1 | n -, mu- | a- | -o- | <i>Mwana a- l-o-umi-a ndo-po-a.</i> (Mtoto aliyeumia amepona) <i>Ndhee a-l-o-anguk-a hakuumia.</i> (Mzee aloanguka hakuumia) |
| 2 | va- | va- | vo- | <i>Vana va-li-vo-umi-a va-ndo-po-a.</i> (Watoto walioumia wamepona). |
| 3 | n-, mu- | u- | -o- | <i>Nchungwa u-lo-kach-w-a ni huu.</i> (Mchungwa uliokatwa ni huu). |
| 4 | mi- | i- | -yo- | <i>Michungwa i-li-yo-kach-w-a ni hii.</i> (Michungwa iliyokatwa ni hii). |
| 5 | i- | li - | -lo- | <i>Iyenyo li-li-lo-tok-a li-ndo-me-a.</i> (Jino lililotoka limemea). |
| 6 | ma- | a- | -yo- | <i>Menyo a-li-yo-tok-a a-ndo-me-a.</i> (Meno yaliyotoka yamemea) |
| 7 | ki- | ki- | -cho- | <i>Kichi ki-li-cho-kach-ik-a ki-tashon-w-a.</i> (Kiti kilichokatika kitashonwa). |
| 8 | dhi- | dhi- | -dho- | <i>Dhichi dhi-li-dho-kach-ik-a dhi-ta-shon-w-a.</i> (Viti viliviyokatika vitashonwa). |
| 9 | n- | i- | -yo- | <i>Nadhi i-li-yo-nunu-liw-a ha-i-fa-i.</i> (Nazi iliyonunuliwa haifai) |
| 10 | n- | dhi- | -dho- | <i>Nadhi dhi-li-dho-nunu-liw-a ha-dhi-fa-i.</i> (Nazi zilizonunuliwa hazifai). |
| 11 | u- | u- | -yo- | <i>Udhi u-li-yo-shon-ew-a ni mweusi.</i> (Uzi ulioshonestwa ni mweusi). |
| 10a | n- | dhi- | -dho- | <i>Nyudhi dhi-li-dho-shon-ew-a ni neusi.</i> (Nyuzi zilizoshonestwa ni nyeusi). |
| 11a | u- | u- | -yo- | <i>Ugonjwa u-li-yo-n-shik-a u-ndo-n-kondr-esh-a.</i> (Ugonjwa uliyomshika umemkondesha.) |
| 6a | ma- | a- | -yo- | <i>Magonjwa yaliyonshika</i> |

| | | | | |
|----|--------|-----|------|--|
| | | | | <i>yandonkondresha.</i> (Magonjwa yaliyomshika yamemkondesha). |
| 14 | u- vu- | u- | -yo- | <i>Udhivu u-li-yo-n-shik-a u-ndo-mu-aib-ish-a.</i> (Uvivu uliyomshika umemuaibisha). <i>Vuyi u-li-yo-pik-w-a undosuka.</i> (Uji uliyopikwa umemwagika). |
| 15 | ku- | Ku | -ko- | <i>Ku-imb-a ku-li-ko-sik-ik-a ku-li-mu-harib-a.</i> |
| 17 | pa- | pa- | -po- | <i>Mahali pa-li-po-saf-ishw-a p'ake.</i> (Mahali paliposafishwa ni pake) |
| 18 | ku- | ku- | -ko- | <i>Mahali ku-li-kosaf-ishw-a kwa'ke.</i> (Mahali kulikosafishwa ni kwake). |

4.4.1.4 Viambishi vya yambwa /Mofimu za yambwa

Kitikuu huweza kuchukua viambishi vya yambwa katika vitenzi vyake. Viambishi vya yambwa vinavyotumiwa hupatikana kama viambishi awali katika vitenzi vya Kitikuu, na vinaweza kuwa ni viambishi vya yambwa tendewa au yambwa tendwa. Yambwa tendwa huwakilisha kitu kinacholipokea tendo fulani, ilihali yambwa tendewa ni mtu/watu au kiumbe/viumbe wanaotendewa jambo fulani.

Vipatanishi hivi vya yambwa hutegemea nafsi na ngeli za nomino zinazorejelewa. Katika viambishi vya nafsi vya yambwa tendwa na tendewa, mofimu za nafsi ndizo zinazotumiwa isipokuwa kwa nafsi ya pili umoja, nafsi ya pili wingi, na nafsi ya tatu umoja kama jedwali hapa chini linavyoonyesha.

Jedwali 8

Viambishi vyta Yambwa Tendwa na Tendewa

| Mofimu za yambwa tendwa | Mifano ya sentensi | Mofimu za yambwa tendewa | Mifano ya sentensi |
|-----------------------------|--|------------------------------|---|
| Nafsi 1 umoja {ni} | <i>Mwalimu a-li-ni-pondr-a yana.</i> (Mwalimu alinipiga jana). | Nafsi 1 umoja {ni} | <i>Mwalimu a-li-ni-som-esh-e-a mwanangu.</i> (Mwalimu alinisomeshea mtoto wangu). |
| Nafsi 1 wingi {chu} | <i>Mwalimu a-li-chu-pondr-a yana.</i> (Mwalimu alitupiga jana.) | Nafsi ya 1 wingi {chu} | <i>Mwalimu a-li-chu-som-esh-e-a vana vechu.</i> (Walimu walitusomeshea watoto wetu.) |
| Nafsi 2 umoja {ku} | <i>Dakitari a-li-ku-dung-a sindano.</i> (Daktari alikudunga sindano.) | Nafsi ya 2 umoja {ku} | <i>Mwanafundi a-li-kw-ech-e-a dhawadi.</i> (Mwanafunzi alikuletea zawadi.) |
| Nafsi ya 2 wingi {va} | <i>Dikitari a-li-va-dung-a sindano.</i> (Daktari aliwadunga sindano.) | Nafsi ya 2 wingi {va} | <i>Mwanafundi a-li-ve-ch-e-a dhawadi.</i> (Mwanafunzi aliwaletea zawadi.) |
| Nafsi 3 umoja {n} | <i>Mwidhi a-li-n-dung-a kisu.</i> (Mwizi alimdunga kisu.) | Nafsi 3 umoja {n} | <i>Ishe a-li-n-nunu-li-a dhawadi ningi.</i> (Babake alimnunulia zawadi nydingi.) |
| Nafsi ya 3 wingi {va} | <i>Mwidhi a-li-va-dung-a dhisu.</i> (Mwizi aliwadunga visu.) | Nafsi ya 3 wingi {va} | <i>Ishe a-li-va-nunu-li-a dhawadi ningi.</i> (Babake aliwanunulia zawadi nydingi.) |

Mofimu za yambwa tendwa na tendewa ni sawa na mofimu za nafsi, isipokuwa kwa nafsi ya pili umoja na wingi, na tatu umoja, kama katika sentensi za hapo juu. Nazo ni:

Nafsi 1 umoja: {ni} pia {na}

Wingi: {chu}

Nafsi 2 umoja: {ku} (badala ya u)

Wingi: {va} (badala ya mu)

Nafsi 3 umoja: {n}, {mu}, {mw} (badala ya a) Wingi: {va}

Nafsi ya kwanza umoja hutumia **{ni}**, lakini pia hutumia **{na}**, kwani ni mfanyiko wa **{ni}** na **{a}** ya njeo iliyopo ikawa **{na}** kwa udondoshi wa vokali ya kwanza.

Nafsi ya tatu umoja ya mofimu {n} ina alomofu {mu} na {mw} katika maneno kama:

nindomwechea (nimemletea), chutamuudhi (tutamuudhi) nk.

Mfano wa nafsi ya pili umoja mofimu {ku} inabadilika na kuwa {kw}, kwa sababu ya mageuko ya uundaji wa kiyeyushi {w};

/u / → /w / / -/ ε/

/ku-ech-ea/ → / kwεchεa/

Katika mfano wa nafsi ya 2 wingi badala ya mofimu {va} inabadilika na kuwa {vε} kwa sababu ya mageuko ya kifonolojia ya kudondosha vokali ya kwanza katika neno hilo;

v → φ / -/v/ /a / → /φ / / -/ε /

a-li-va-ech ea → alivechea

Mofimu za ngeli nyingine za yambwa tendwa huchukua mofimu zake za upatanishi katika viambishi awali vyta kitenzi:

28a) Nkulima a- li - **u** – kach- a nchi. (Mkulima aliukata mti).

| | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|-------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | yambwa tendwa | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|------------------|-------|---------|

Vakulima va- li- i- kach- a michi. (Wakulima waliikata miti.)

| | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|--------|---------|
| Nafsi 3 wingi | njeo iliyopita | yambwa tendwa | mizizi | kiishio |
|------------------|-------------------|------------------|--------|---------|

28b) Mwanafundi a- li- **ki-** vund- a kichi. (Mwanafunzi alikivunja

| | | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|--------|---------|--------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | yambwa tendwa | mizizi | kiishio | kiti). |
|------------------|-------------------|------------------|--------|---------|--------|

Vanafundi va- li- dhi- vund- a dhichi. (Wanafunzi walivivunja

| | | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|-------|---------|--------|
| Nafsi 3 wingi | njeo iliyopita | yambwa tendwa | mzizi | kiishio | viti). |
|------------------|-------------------|------------------|-------|---------|--------|

Ikumbukwe kuwa kwa yambwa tendewa hatuwezi kutumia mofimu za tendewa kwa vitu ambavyo havina uhai, ni kwa viumbe pekee ndiyo tunaoweza kutumia yambwa tendewa.

Vilevile mofimu hizi za yambwa tendwa na tendewa hazipatikani kwa pamoja katika kitenzi kimoja cha Kitikuu, kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu. Mofimu mojawapo itapatikana katika kitenzi husika kama tulivyoona.

4.4.1.5 Mofimu za Jirejea

Mofimu za kujirejelea au kujitendea hupatikana katika sehemu ya viambishi awali katika kitenzi cha Kitikuu. Lahaja ya Kitikuu hutumia mofimu {-i-} katika umoja na wingi kuonyesha kujitendea. Hali ya kujitendea/kujirejelea hupatikana katika viumbe na sio ngeli nyingine zisizoweza kujirejelea.

Nafsi ya kwanza:

29a) *Na- li- i- kach- a kwa kijembe.* (Nilijkata kwa kijembe).

Nafsi 1 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
umoja iliyopita kujitendea

29b) *Chu- li- i- kach - a kwa dhijembe.* (Tulijkata kwa vijembe).

Nafsi ya 1 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
wingi iliyopita kujitendea

Nafsi ya Pili:

29c) *U- li- i- kach - a kwa kisu.* (Ulijikata kwa kisu).

Nafsi ya 2 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
umoja iliyopita kujitendea

29d) *Mu - li- i- kach- a kwa kisu.* (Mlijikata kwa kisu)

Nafsi ya 2 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
wingi iliyopita kujitendea

Nafsi ya tatu

29e) *A- li- i- kach- a kwa kijaya.* (Alijikata kwa kigae).

Nafsi ya 3 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
umoja iliyopita kujitendea

29f) *Va- li- i- kach- a kwa kijaya.* (Walijikata kwa kigae).

Nafsi ya 3 njeo kiambishi cha mzizi kiishio
wingi iliyopita kujitendea

4.4.1.6 Mofimu za Njeo, Hali na Dhamira

Mofimu za njeo hali na dhamira pia zinapatikana kama viambishi awali katika lahaja ya Kitikuu, japo kuna viambishi vya dhamira vinavyopatikana kama viambishi tamati. Mofimu hizo zitajadiliwa kwa kina baadaye katika sura inayofuata kwani ndiyo lengo hasa la utafiti huu, kuchanganua mofimu za njeo, hali na dhamira katika lahaja ya Kitikuu.

4.4.2 Mzizi wa Kitenzi

Mzizi wa kitenzi ni mofimu muhimu na bila mzizi basi hakuna kitenzi. Mzizi wa kitenzi ni sehemu ya kitenzi isiyobadilika, hata tukinyambua kitenzi kwa hali mbalimbali mzizi bado unabaki. Mofimu mbalimbali zinaweza kuwekwa mwanzoni mwa mzizi, kama ambavyo tumeona au baada ya mzizi, ili kuvipa vitenzi maana mbalimbali.

Mara nyingi mizizi ya vitenzi katika lugha za Kibantu, huchukua muundo wa konsonanti, vokali na konsonanti KVK (Kamil, 2002); kuna pia mizizi mingine mbalimbali inayochukuliwa na lahaja ya Kitikuu kama: konsonanti moja au mfuatano wa konsonanti mbili K, KK; vokali na konsonanti VK; vokali, vokali na konsonanti VVK; vokali, konsonanti, konsonanti, vokali na konsonanti VKVK; kama inavyoonyeshwa katika jedwali 9.

Jedwali 9

Muundo wa mzizi wa kitenzi

| | Muundo wa Mzizi | Mifano ya mizizi ya vitenzi | Mifano ya vitenzi (mashina) |
|---|------------------------|---|--|
| A | K, KK | -l-, -p-, -ny-, -nw- | <i>kula, kupa, kunya kunwa</i> (kunywa), |
| b | VK | um-, at- | <i>Uma, ata</i> (wacha) |
| C | KVK | tedh-, pik-, lim-, som-, vak-, viv-nen-, pich- tek- | <i>tedha</i> (cheza), <i>pika</i> , <i>lima</i> , <i>soma</i> , <i>vasa</i> (washa), <i>viva</i> (iva), <i>nena</i> (sema) <i>picha</i> (pita) <i>teka</i> (cheka) |
| d | VKK | imb-, omb-, | <i>imba, ombo</i> |
| E | VK | us-, ag-, os- | <i>usa</i> (rusha), <i>aga</i> , <i>osa</i> (osha) |

| | | | |
|---|-------|-------------------------|---|
| F | VKKVK | anguk-, ambach, - andik | <i>anguka, ambacha (ambata), andika</i> |
| g | VKVK | adhim- | <i>Adhima (azima)</i> |
| h | KV | fu-, va-, vu- | <i>fua, vaa, vua (ua),</i> |

Hiyo ni baadhi tu ya miundo ya mizizi tunayoweza kupata katika Kitikuu yenyе asili ya Kibantu, lakini tunapoongezea mizizi yenyе asili ya kigeni tunaweza kupata orodha ndefu zaidi kama; KVKV- sahau, dharau, sikia; KVKV- tubu, dhuru; KVVKV- fahamu, samehe, fikiri na mengineo.

4.4.3 Viambishi Tamati

Kama tulivyoeleza hapo mbeleni, lahaja ya Kitikuu ina viambishi vya aina mbili, viambishi awali vinavyopatikana kabla ya mzizi wa kitenzi na viambishi tamati vinavyopatikana baada ya mzizi wa kitenzi. Kitikuu kina viambishi tamati vya kitenzi vifuatavyo:

4.4.3.1 Vimalizio vya Kitenzi

Vimalizio vya vitenzi ni viambishi au mofimu zinazowekwa baada ya mzizi wa kitenzi ili kuvikamilisha. Vimalizio katika Kitikuu, kama Kiswahili Sanifu ni viungo vya lazima na hutumika kuonyesha dhamira (Kamil, 2002). Ijapokuwa katika Kitikuu mofimu ya kimalizio ya -e, mbali na kuonyesha dhamira hutumika pia kuonyesha hali timilifu, kama itakavyoolezewa kwa urefu katika hali timilifu, mfano: uiyele (amelala), uchosee (amechoka).

Dhamira arifu na pia dhamira amrishi yakinishi katika umoja huchukua mofimu {-a} kama kimalizio.

Dhamira arifu**Dhamira amrishi**

- 30a) *Amina hu - tedh - a.* (hucheza)
 Hali ya mzizi kiishio
 mazoea
- 30b) *Mwana a - ta - imb- a.*
 Nafsi 3 njeo mzizi kiishio
 umoja ijayo
- 30c) *A - li - pik - a wali.*
 Nafsi 3 njeo mzizi kiishio
 umoja iliyopita
- Tedh - a!* (Cheza!)
- Imb - a!* (Imba!)
- Pik - a!* (Pika!)

Dhamira amrishi katika wingi ina mofimu ya kiishio {-ani}:

- 31a) *Tedh - ani !* (Chezeni!)
- Mzizi kiishio cha wingi
 dhamira amrishi
- 31b) *Imb - ani !* (Imbeni!)
- Mzizi kiishio cha wingi
 dhamira amrishi
- 31c) *Pik - ani !* (Pikeni!)
- Mzizi kiishio cha wingi
 dhamira amrishi

Tofauti na Kiswahili Sanifu, Kitikuu hutumia kiishio **-ani** na Kiswahili Sanifu hutumia kiishio **-eni**, katika wingi wa dhamira amrishi.

Dhamira tegemezi hutumia mofimu {-e}:

- 32a) *Tafadhali m - pek - e sipichali.* (Tafadhali mpeleke hospitali.)
- Nafsi ya mzizi kiishio
 mtendwa
- 32b) *Mu - omb- e - e Mungu a - pow- e haraka.*
- Nafsi ya mzizi kiambishi kiishio
 mtendwa cha mtendwa
- nafsi 3 mzizi kiishio
 umoja
- (Muombee Mungu apone haraka.)

Katika Kitikuu, wakati mwingine kutegemea na kitenzi kinachotumika, mofimu tegemezi huweza kuainishwa na mofimu {-a} badala ya {-e}, tofauti na Kiswahili Sanifu na hii aghalabu hujitokeza kwa nafsi ya kwanza umoja:

- 32c) *Tafadhali nip - a kalamu.* (Tafadhali nipe kalamu.)

Mzizi kiishio

- 32d) *N - ech - e - a nami dhawadi ukirudi.* (Niletee na mimi zawadi ukirudi.)

Nafsi 1 mzizi kiambishi kiishio
umoja cha mtenda

Katika sentensi ya (32d) kitenzi ‘**nechea**’ kimepitia mabadiliko ya kimofofonolojia kwani kitenzi kinatakiwa kiwe ni-ech-e-a, {ni} ikiwa ni mofimu ya nafsi ya kwanza umoja, lakini kwa sababu ya vokali hizo mbili kufuatana (**i** na **e**) na kurahisisha matamshi, vokali ya kwanza {i} hudondoshwa na tunakuwa na kitenzi ‘**nechea**’ badala ya ‘**niechea**’.

Sheria:

/v/ → /ɸ/ / -/v/ /i/ →/ ɸ / - /ɛ/

/ni- etʃ-ɛ-a/ → /netʃea/

4.4.3.2 Mofimu za Ukanushi

Mofimu au viambishi vyta ukanushi vilevile huweza kupatikana kama viambishi tamati katika lahaja ya Kitikuu. Katika njeo iliyopo, njeo ijayo, hali ya mazoea na hali ya kuendelea, Kitikuu hutumia ukanushi wa mofimu {-i} kama kimalizio cha ukanushi wake:

Yakinishi

- 33a) *Amina hu - l - a chakula.*

Hali ya mazoea/ mzizi kiishio
Hali ya kuendelea kanushi

Kanushi

- Amina ha - l - i chakula.*

kiambishi mzizi mofimu kanushi
kanushi ya kiishio

(Amina hula chakula/ Amina anakula chakula). (Amina hali chakula).

- 33b) *Mwana a - tak - a ku - l - a.* *Mwana ha- tak - i ku- l - a.*
- Njeo mzizi kiishio mofimu mzizi kiishio
iliyopo/ ku
nafsi 3umaja
- ukanushi mzizi kiishio mofimu mzizi kiishio
nafsi kanushi ku
- (Mtoto ataka kula). (Mtoto hataki kula).
- 33c) *Maria a - ta- ku- y - a kesho.* *Maria Ha - y - i kesho.*
- Nafsi 3 njeo kiambishi mzizi kiishio
umoja ijayo cha ku
- kiambishi mzizi mofimu kanushi
kanushi ya kiishio
- (Maria atakuja kesho.) (Maria hatakuja kesho.)

Katika ukanushi wa njeo ijayo, Kitikuu hukanusha, nafsi (isipokuwa nafsi ya kwanza umoja) na kuwa {ha} na kiishio huwa {i}, mofimu ya njeo ijayo {ta} haitumiwi, tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo hubakisha mofimu ya njeo {ta} na hukanusha nafsi kwa kutumia {ha}, lakini kiishio hakibadiliki hubaki {a}, kama mfano wa 33c unavyoonyesha. Katika ukanushi wa dhamira mbalimbali pia tunapata mofimu za ukanushi zikibadilika. Kwa mfano, dhamira amrishi na ulizi katika umoja na wingi hubadilika katika ukanushi wake na kuchukua mofimu mbalimbali:

Umoja

- 34a) *Pik - a! / u - si - pik - e!* *Pik- ani! / mu- si- pik- e!*
- Mzizi kiishio nafsi 2 kiambishi mzizi kiishio
umoja kanushi
- mzizi kiishio nafsi 2 kiambishi mzizi kiishio
wingi kanushi
- (Pika / Usipike) (Pikeni / Msipike)

Wingi

- 34b) *Tedh- a! / u- si- tedh- e!* *Tedh- ani! / mu- si- tedh- e!*
- Mzizi kiishio nafsi 2 kiambishi mzizi kiishio
umoja kanushi
- mzizi kiishio nafsi 2 kiambishi mzizi kiishio
wingi kanushi

Dhamira ulizi:

- 34c) *U - ta- ku- l - a eo? / Hu - l - i eo?*
- Nafsi 2 njeo kiambishi mzizi kiishio
umoja ijayo cha ku
- kiambishi kanushi mzizi kiishio
na nafsi 2 umaja
- (Utakula leo? / Huli leo?)

34d) *Mu - ta- imb- a?* / *Ha - mu- imb - i?*

| | |
|----------------------------|---------------------------------|
| Nafsi 2 njeo mzizi kiishio | kiambishi nafsi 2 mzizi kiishio |
| wingi ijayo | kanushi wingi kanushi |

(Mtaimba? / Hamuimbi?)

34e) *A - ta - imb- a?* / *Ha - imb - i?*

| | |
|----------------------------|-------------------------|
| Nafsi 3 njeo mzizi kiishio | kiambishi mzizi kiishio |
| umoja ijayo | kanushi kanushi |

(Ataimba? / Haimbi?)

Katika mfano wa (34c) mofimu {**hu**} katika ukanushi imebeba mofimu ya ukanushi {**ha**} na mofimu ya nafsi ya pili umoja {**u**}, kisha mageuko ya kimofofonolojia yanatokea na kudondosha mofimu ya kwanza {**a**}.

/ha-u-li / → /huli/

4.4.3.3 Mofimu za urejeshi

Mofimu za urejeshi, mbali na kuwa ni viambishi awali vilevile hupatikana kama viambishi tamati, katika lahaja ya Kitikuu. Kutegemea ngeli mbalimbali viambishi vya urejeshi kama tulivyoona katika viambishi awali, huweza pia kutumika mwishoni mwa kitenzi.

35a) *Mwana ni - m- pend - a - e ni huu.* (Mtoto nimpendaye ni huyu).

| |
|-------------------------------------|
| Nafsi 1 mofimu mzizi kiishio mofimu |
| umoja mtendwa rejeshi |

35b) *Nnadhi u - kasi- wa- o ni ulee.* (Mnazi uliokatwa ni ule.)

| |
|-------------------------------|
| Kiambishi mzizi mofimu mofimu |
| ngeli kitendwa rejeshi |

35c) *Dhiachu dhi - a - dhi - mwa - dho ni hidhi.*

| |
|-----------------------------------|
| Kiambishi kiambishi mofimu mofimu |
| ngeli ngeli kitendwa rejeshi |

(Viatu viazimwavyo ni hivi.)

4.4.3.4 Mofimu / Viambishi vya mahali na wakati

Viambishi tamati katika lahaja ya Kitikuu huweza kutumika kuonyesha mahali au wakati katika kitenzi. Mofimu {-ko}, {-po} hutumika kuonyesha mahali katika kitenzi cha Kitikuu, na mofimu {-po} huweza kutumika kuonyesha wakati. Lahaja hii haitumii mofimu {mo} ya mahali, kama tulivyoonyesha katika ngeli za Kitikuu. Kitikuu hakina ngeli ya mahali {mo}.

- 36a) *Hoko ndriko a – tedh- a - ko.* (Huko ndikoachezako).

| | | | |
|---------|-------|---------|-----------|
| Nafsi 3 | mzizi | mofimu | mofimu |
| umoja | | kiishio | ya mahali |

- 36b) *Hapa ndripo a – yal- a - po Halima .* (Hapa ndipo alalapo Halima).

| | | | |
|---------|-------|------------|-----------|
| Nafsi 3 | mzizi | mofimu | mofimu |
| umoja | | ya kiishio | ya mahali |

- 36c) *U - malidh- a- po kadhi nambia.* (Umalizapo kazi niambie).

| | | | |
|---------|-------|---------|--------|
| Nafsi 2 | mzizi | mofimu | mofimu |
| umoja | | kiishio | wakati |

4.4.3.5 Viambishi vya Kauli /Mofimu za Kauli

Hivi ni viambishi vya unyambuaji vya kitenzi. Viambishi vya kauli au vya unyambuaji ni viambishi tamati vinavyopachikwa baada ya mzizi wa kitenzi. Mofimu au viambishi hivi havibadili kategoria ya neno. Kategoria ya neno linabaki kuwa kitenzi. Shina la kitenzi cha Kitikuu, kama ilivyo luga zenyé asili ya Kibantu huishia na vokali {-a} : tedh-a (cheza), imb-a, pik-a, kimbi-a, som-a nk.

Hebu tuangalie kauli mbalimbali za vitenzi vya Kitikuu vyenye asili ya Kibantu :

a) Kauli ya kutendwa

Kauli hii huonyesha mtu/watu au kitu/vitu fulani vimepokea tendo fulani. Alomofu zinazotumika katika kauli hii ni {w}, {iw}, {ew}, {aw} {liw} na {lew}.

37a) *Mwanafundi a - li - pond - w - a na mwalimu wake.*

Nafsi 3 njeo mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendwa

(Mwanafunzi alipigwa na mwalimu wake).

37b) *Maria a - li - kimb- iw- a na inya.* (Maria alikimbiwa na mamake).

Nafsi 3 njeo mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendwa

37c) *Mwalimu Hamisi hu - ch- ew - a na vanafundi vote.*

Hali ya mzizi kauli kiishio
mazoea tendwa

(Mwalimu Hamisi huogopewa na wanafunzi wote.)

38d) *Mbudhi a - li - chombo - lew - a ito yana.*

Nafsi 3 njeo mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendwa

(Mbuzi alitobolewa jicho jana).

b) Kauli ya Kutendea

Katika kauli ya kutendea, tendo huonyesha kufanya kazi kwa maana mbalimbali zikiwemo:

i) Tendo linatendwa kwa manufaa/faida au hasara ya mtu. Mfano:

38a) *Na- li- n- lip- i- a senti dha sukuli ili asikose masomo.*

Nafsi 1 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

(Nilimlipia karo ya shule ili asikose masomo).

A - li- n - su- li - a chakula chote kwa kukosa adabu.

Nafsi 3 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

(Alimmwigia chakula chote kwa kukosa adabu).

ii) Kuonyesha kifaa au ala iliyotumika. Mfano:

38b) Hamisi a - li - kach - i- a nyama kisu kikali.

Nafsi 3 njeo mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

(Hamisi alikatia nyama kisu kikali).

iii) Tendo linatendwa kwa niaba ya mtu mwengine. Mfano:

38c) Amina a - li - n - tuku- li- a mwanavo dhawadi dhake.

Nafsi 3 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

(Amina alimchukulia nduguye zawadi zake).

iv) Tendo linaelekezwa kwa mtu fulani. Mfano:

38d) Maria a - li - mu- us- i- a Hamisi npira

Nafsi 3 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

(Maria alimrushia Hamisi mpira).

v) Tendo kusababishwa na jambo fulani. Mfano:

38e) A - li - n - dhom- e - a alipokosa. (Alimzomea alipokosa).

Nafsi 3 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

vi) Kuonyesha mahali tendo lilipotendeka. Mfano:

38f) Mwidhi a - li - n - jep- e - a garini. (Mwizi alimuibia garini).

Nafsi 3 njeo mtendewa mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita tendea

Alomofu za kauli ya kutenda ni:

- {-i-} kwa vitenzi vyenye mzizi wa a, i, u kama: pik-i-a, us-i-a (rushia), lip-i-a na kadhalika.
- {-e-} kwa vitenzi vyenye mzizi wa e na o kama: pok-e-a, somea, dhom-e-a (zomea), jep-e-a (ibia) na kadhalika.

- {-li-} kwa vitenzi vyenye mzizi unaoishia na vokali, na vokali ya mzizi ni a,i, au u kama kimbi-li-a, tuku-li-a (chukulia), za-lia, va-li-a na kadhalika.
- {-le} kwa vitenzi vyenye mzizi unaoishia na vokali, na vokali ya mzizi ni o au e kama le-lea, poke-le-a, pote-lea, tembe-le na kadhalika.

c) Kauli ya Kutendewa

Katika kauli hii hutumiwa kuonyesha ile hali ya mtu/watu kufanyiwa jambo fulani. Huwa kuna mtu/watu wanaofanya kitendo kwa niaba ya mtu/watu wengine. Anayefanyiwa kitendo huwa ni kwa faida au hasara kwake.

Hapa alomofu mbalimbali hutumiwa kuonyesha kauli hii kama: **{iw}**, **{ew}**, **{liw}** na **{lew}**. Alomofu **{iw}** na **{ew}** hutumika katika vitenzi ambavyo havina mfuatano wa vokali mwisho. Alomofu **{iw}** hutumika pale katika mzizi wa kitenzi hutumia vokali kaze yaani **a**, **i** au **u** kama: **pik-iw-a**, **fany-iw-a**, **fum-iw-a**; na alomofu **{ew}** hutumika katika vitenzi vyenye vokali hafifu kwenye mzizi wake ambazo ni **e** na **o** kama **som-ew-a**, **tek-ew-a** (chekewa), **chom-ew-a**, **tedh-ew-a** (chezewa).

Kwa upande mwingine alomofu **{liw}** na **{lew}** hutumika kwa vitenzi vyenye kuishia na vokali katika mzizi wake wa kitenzi. Iwapo vokali ya mzizi ni **a**, **i**, au **u** basi itachukua alomofu **{liw}** kwa mfano za-liw-a, tuku-liw-a, (chukuliwa), timi-liw-a. Kwa upande mwingine, kama vokali ya mzizi ni **e** au **o** basi itachukua alomofu **{lew}** kwa sababu ya wiano wa vokali, mifano: chobo-lew-a (tobolewa), tembe-lew-a, kombo-lew-a nk.

39a) *Vana va - li - pik - iw - a chakula na jirani.*

| | | | | |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|
| Nafsi 3 wingi | njeo iliyopita | mzizi | kauli tendewa | kiishio |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|

(Watoto walipikiwa chakula na jirani.)

39b) *Hamisi a - li - som - ew - a barua na Amina.*

| | | | | |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mzizi | kauli tendewa | kiishio |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|

39c) *Mwidhi a - li - tuku - liw- a iyu kwa iyu na askari.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendewa | |

(Mwizi alichukuliwa juu kwa juu na askari).

d) Kauli ya Kutendeka

Katika kauli hii ya kutendeka hatuambiwi aliyesababisha kitendo kutendeka, lini tendo hilo lilianza na lini lilimalizika. Alomofu ya kauli hii ni **{ik}** kwa vitenzi vyenye vokali za mzizi **a, i** au **u** kama pik-ik-a, uk-ik-a (rukika) na alomofu **{ek}** kwa vitenzi vyenye vokali za mzizi **e** au **o** kama som-ek-a, tedh-ek-a (chezeka). Kwa vitenzi vinavyoishia na vokali, huchukua alomofu **{lik}** kwa vokali kaze kama **a, i** au **u** mfano: va-lik-a, dha-lik-a, na alomofu **{lek}** kwa mzizi wa kitenzi unaoishia na vokali hafifu; **e** au **o** mfano: tembe-lek-a, chobo-lek-a (toboleka).

40a) *Chakula ki - li - pik - ik - a kwa udhuri.* (Chakula kilipikika kwa uzuri.)

| | | | | |
|------------|-----------|-------|---------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| upatanishi | iliyopita | | tendeka | |

40b) *Hati dhake hu - som - ek - a .* (Hati zake zinasomeka.)

| | | | |
|--------|-------|---------|---------|
| Hali | mzizi | kauli | kiishio |
| mazoea | | tendeka | |

40c) *Mwanambudhi a - li - dha - lik - a bila tabu.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendeka | |

(Mwanambuzi alizalika bila tabu.)

e) Kauli ya Kutendesha

Kauli ya kutendesha huonyesha kuwa tendo limesababishwa na mtu/watu au kitu/vitu fulani. Kitikuu kina alomofu mbalimbali zinazoweza kuonyesha kauli hii nazo ni: {ish}; pik-ish-a

{esh};som-esh-a

{s}: va-s-a (washa)

{dh}: tembe-dh-a (tembeza)

{idh}: lip-idh-a (lipiza)

{edh}: pend-edh-a (pendeza)

{lish}: dha-lish-a (zalisha)

{lesh}: dho-lesh-a.

41a) *Tajiri ake a - li - n - pik - ish - a chakula kingi yana.*

| | | | | |
|--------------|----------|-------|----------|---------|
| Nafsi 3 njeo | mtendewa | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | ilyopita | | tendesha | |

(Tajiri yake alimpikisha chakula kingi jana).

41b) *Mwalimu Ali a - li - som - esh - a kwa udhuri somo la Kiswahili.*

| | | | |
|--------------|----------|----------|---------|
| Nafsi 3 njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | ilyopita | tendesha | |

(Mwalimu Ali alisomesha vizuri somo la Kiswahili).

41c) *Maria a - li - kw - endr - a ku - n - tembe- dh - a mwanavo sokoni.*

| | | | |
|--------------|-----------|---------|------------|
| Nafsi 3 njeo | kiambishi | mzizi | kiishio |
| umoja | ilyopita | kitemzi | tendesha |
| | ku | | kisoukombo |

(Maria alikwenda kumtembeza nduguye sokoni).

41d) *A - li - n - dho - lesh - a chaka dhote.*

| | | | | |
|--------------|----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 njeo | mtendwa | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | ilyopita | | endesha | |

(Alimzolesha taka zote.)

Katika lahaja ya Kitikuu, alomofu {fy} hakuna, kama inavyotumika katika Kiswahili

Sanifu kuonyesha kauli ya kutendesha kama katika neno, **ogo-fy-a**.

f) Kauli ya kutendana

Katika kauli hii huonyesha ile hali ya watu wawili au zaidi kufanyana tendo fulani. Kwamba mtu I anamfanya mtu II tendo, naye mtu II anamfanya mtu I tendo hilo hilo. Mofimu ya kauli hii ni **{an}** haijalishi vokali ya mzizi iwe ni a, e, i, o au u. Vitenzi vyote huchukua kiambishi hicho cha **-an-**:

42a) *Maria na Juma va - pend - an - a sana.* (Maria na Juma wanapendana sana).

| | | | |
|---------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | | tendana | |

42b) *Chu - li - von - an - a yana kwa dakitari.* (Tulionana jana kwa daktari).

| | | | | |
|---------|------|-----------|---------|---------|
| Nafsi 1 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | | iliyopita | tendana | |

42c) *Vana va jirani va - li - chom - an - a kwa mocho.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | | tendana | |

(Watoto wa jirani walichomana kwa moto.)

g) Kauli ya kutendeana

Katika kauli hii huwa wahusika wawili au zaidi wanafanya tendo kwa niaba ya faida au hasara ya mwengine na mwengine naye anamfanya tendo hilo hilo. Yaani tendo linaweza kuwa la faida/zuri au la hasara/ baya. Hivyo wahusika wawili au zaidi wanafanyiana tendo. Alomofu za kauli hii ni **e-an**, **i-an**, **li-an**, **le-an**. Kiambishi **e-an** hutumika kwa vitenzi vyenye mzizi wa vokali **e** au **o**: som-**e-an-a**, tek-**e-an-a** (chekeana) na **i-an** hutumika kwa vitenzi vyenye mzizi wa vokali **a**, **i** na **u**: pik-**i-an-a**, tuk-**i-an-a** (chukiana), kwa mujibu wa wiano wa vokali. Vitenzi vyenye viishio vyakali mbili au zaidi na vokali ya mzizi ni **e** au **o** basi hutumia kiambishi **le-an**: tembe-**le-an-a**, hali kadhalika iwapo vitenzi ni vyakali mbili au zaidi na vokali ya mzizi ni **a**, **i** au **u** basi hutumia alomofu **li-an**: kimbi-**li-an-a**.

43a) *Hassani na Hussenii* *va - li - som - ean - a hadisi.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|----------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendeana | |

(Hassan na Hussein walisomeana hadithi).

43b) *Marafiki* *va - li - pik - ian - a chakula.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|----------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | | tendeana | |

(Marafiki walipikiana chakula).

43c) *Vanafundi* *va - li - tembe - lean - a numbani kwavo.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|----------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | | tendeana | |

(Wanafunzi walitembeleana nyumbani kwao).

h) Kauli ya kutendama

Kauli hii humaanisha vitu au watu huwa katika hali ya kuwa pahali pamoja kwa muda mrefu au tendo kukwama katika hali fulani. Mofimu {-am-} hutumika kuonyesha kauli hii.

44a) *Mwidhi* *a- li- n- gandr- am- a asikari.* (Mwizi alimgandama askari.)

| | | | | | |
|---------|-----------|----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mtendewa | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | | tendama | |

44b) *Machachu* *i- li - sak- am- a kwenye chocho.*

| | | | | |
|------------|-----------|-------|---------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| upatanishi | iliyopita | | tendama | |

(Matatu ilikwama kwenye tope).

44c) *Mato ake* *a - li - fung - am - a baada a ku- pach- a ugonjwa wa mato.*

| | | | | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio | kitenzi | mzizi | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendama | | kisoukomu | | |

(Macho yake yalifungama baada ya kupata ugonjwa wa macho).

i) Kauli ya kutendua

Hii huonyesha kinyume cha tendo lililotajwa. Alomofu {-u-} au {-o-} hutumika kutegemea mzizi wa kitenzi. Iwapo mzizi wa kitenzi una vokali **a, e, i** au **u** basi

kiambishi –**u-** cha ukarusha hutumika na iwapo vokali ya mzizi ni - **o-** basi kiambishi – **o-** ya kinyume hutumika.

45a) *Sungura a - li- cheg - u- a ncatego.* (Sungura alitegua mtego.)

| | | | | |
|------------|-----------|-------|--------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| upatanishi | iliyopita | | tendua | |

45b) *Jumaa a - li- an- u- a nguovo dhote.* (Jumaa alianua nguo zote).

| | | | | |
|---------|-----------|-------|--------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendua | |

45c) *Mwidhi a - li - ki - chom- o- a kisu.* (Mwizi alikichomoa kisu).

| | | | | | |
|---------|-----------|----------|-------|--------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | kitendwa | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | | tendua | |

j) Kauli ya kutenduka

Kauli hii hukaribiana na ya kutendua kwani huonyesha kinyume. Tofauti ni kuwa katika kauli hii haionyeshi mtendaji, tendo hutendeka tu lakini katika kauli ya kutendua bila kuonyesha kusababishwa na kitu au mtu fulani. Kiambishi cha kauli hii ni –**uk-**:

46a) *Nlango wa chumbani u - li- fung- uk- a wenewe.*

| | | | | |
|------------|-----------|-------|-----------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli ya | kiishio |
| upatanishi | iliyopita | | kutenduka | |

(Mlango wa chumbani ulifunguka wenyewe).

46b) *Nchego wa pana u - li - cheg - uk- a.*

| | | | | |
|------------|-----------|-------|-----------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli ya | kiishio |
| upatanishi | iliyopita | | kutenduka | |

(Mtego wa panya uliteguka.)

Hapa ikumbukwe kwamba ni baadhi tu ya vitenzi vinavyoweza kubadilishwa katika kauli ya kutendua na kutenduka. Katika Kitikuu, kama Kiswahili Sanifu si vitenzi vyote vinavyoweza kubadilika katika kauli ya kutendua na kutenduka.

4.4.3.6 Mnyambuliko wa vitenzi vyatya asili ya kigeni

Tumekuwa tukiangalia mnyambuliko wa vitenzi vyenye asili ya Kibantu, na tunaona shina la kitensi lenye asili ya Kibantu lazima liishie na vokali **-a** kama pig-a, imb-a, kimbi-a nk. Vitenzi vyenye asili ya Kigeni au vya mkopo, huweza kuishia kwa vokali nyingine pasi na **-a**, huweza pia kuchukua vokali kama **e**, **i** na **u**. Mifano ni kama ajiri, samehe, fahamu, abudu, hubiri, tubu, jibu, fikiri, adhibu, tumaini, shukuru, kiri, hadhari na sahau. Kuna mifano michache ya vitenzi vya mkopo vinavyoishia na vokali **-a** kama vile: nuia, batiza, hadaa nk.

Mnyambuliko wa vitenzi vyenye asili ya kigeni hazifuati sheria hizo za asili ya Kibantu kwani tunaona vitenzi vingi ni vyenye kuishia na vokali isiyokuwa **-a** na hivyo sio lazima kuchukua alomofu au viambishi sawa na vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Tutatumia baadhi ya mifano ya vitenzi vya mkopo hapo juu tuvinyambue katika kauli mbalimbali.

a) Kauli ya kutendea

Katika kauli ya kutendea vitenzi vya kukopwa huchukua mofimu **{-a}** kama kiishio chake: Ajiri-a, samehe-a, abudi-a, hubiri-a, tubi-a, fikiri-a, adhibi-a.

Kwa vitenzi vyenye vokali mbili au zaidi zinazofuatana basi kiambishi **-li-a** hutumika: sahau-**li-a**, nui-**li-a**, hada-**li-a** nk.

47a) *U - li - mw- ajiri- a nini kama ha - wedh - i kadhi?*

| | | | | | | | |
|------------------|-------------------|---------|-------|----------------------|----------------------|-------|--------------------|
| Nafsi 2 umoja | njeo iliyopita | mtendwa | mzizi | kauli ya kutendea | kiambishi kanushi | mzizi | kiishio kanushi |
|------------------|-------------------|---------|-------|----------------------|----------------------|-------|--------------------|

(Ulimwajiria nini kama hawezikazi?)

47b) *Mwalimu a - li- n- samehe - a mwanaufundi wake.*

| | | | | |
|------------------|-------------------|---------|-------|--------------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mtendwa | mzizi | kauli tendea |
|------------------|-------------------|---------|-------|--------------|

(Mwalimu alimsamehea mwanafunzi wake).

47c) A - li - nui- a kutokula siku ndima. (Alinua kutokula siku nzima).

Nafsi 3 njeo mzizi kauli tendea
umoja iliyopita

Ikumbukwe kwamba vitenzi nya mkopo mara nyingi neno zima huwa ni mzizi wa kitenzi, kwa hivyo vinaponyambuliwa katika kauli ya kutendea huwa vokali **-a** huongezwa mwishoni mwa vitenzi vinavyoishia na vokali **-i** na - e kama ahidi-a, afiki-a, hubiri-a, safiri-a, fariki-a samehe-a, starehe-a nk. Iwapo mzizi wa kitenzi wenyewe asili ya kigeni unaishia na vokali **-u**, basi katika hali ya kutendea, vokali -u hudondoshwa na kuchukua vokali **-i-** na mwisho vokali **-a** ya hali ya kutendea. Hii ni katika mifanyiko ya kifonolojia ili kurahisisha matamshi kutamka vokali tatu kwa pamoja ni shida; shutumuia inakuwa shutumia. Mifano zaidi ni kama shuku-shukia, haribu-haribia, heshimu-heshimia, tubu-tubia, hutubu-hutubia, fahamu-fahamia, shukuru-shukuria, jibujibia, hukumu-hukumia nk.

Sheria hapa tunaweza kuorodhesha kama: /u/ →/ø// - / i+a/

b) Kauli ya kutendwa au kutendewa

Katika vitenzi vyenye asili ya kigeni kauli ya kutendwa na kutendewa huwa ni sawa hakuna tofauti kwani kauli zote mbili huchukua kiambishi **-w-** na **-a-** ya kiishio. Mizizi ya vitenzi vyenye kuishia na /ɛ/ au /i/ huongezwa tu mofimu {-w-} ya kutendwa/kutendewa na baadaye mofimu {-a} ya kiishio. Mifano: ahidi-w-a, hubiri-w-a, samehe-w-a, safiri-w-a, starehe-wa, afiki-w-a, tafiti-w-a, fikiri-w-a.

Katika vitenzi nya kigeni vyenye mzizi unaoishia na **-u** hubadilika ikawa **-i** na kisha kama hapo juu ikachukua mofimu **-w-** na **-a** ya kiishio. Mifano: hukumu-hukumi-w-a, adhibu-adhibi-wa-, heshimu - heshimi-w-a, ruhusu- ruhusi-w-a nk.

Na iwapo mzizi unaishia na vokali zaidi ya moja basi huchukua alomofu {-liw-}; mifano: dharau-dharau-liw-a, sahau-sahau-liw-a, nuia-nui-liw-a.

Kauli ya kutendwa

48a) *Vanafundi va - li- hubiri- w- a na mbunge wavo yana.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|--------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | | tendwa | |

(Wanafunzi walihubiriwa na mbunge wao jana).

48b) *Chu - li- ruhus- i- w- a kungia harusini bila kadi.*

| | | | | | |
|---------|-----------|-------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 1 | njeo | mzizi | kiambishi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | kabla | tendwa | | |

(Tuliruhusiwa kuingia harusini bila kadi).

48) *Mwana a - li - sahau- liw- a na inya.* (Mtoto alisahauliwa na mamake).

| | | | | |
|---------|-----------|-------|--------|---------|
| Nafsi 1 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendwa | |

Kauli ya kutendewa

49a) *Ni- ndo- ahid - iw- a ku- pek- w- a udhunguni na mbunge wechu.*

| | | | | | | | | |
|---------|----------|-------|---------|---------|--------|-------|--------|---------|
| Nafsi 1 | hali | mzizi | kauli | kiishio | mofimu | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | timilifu | | tendewa | | ku- | | tendwa | |

(Nimeahidiwa kupelekwa uzunguni na mbunge wetu).

49b) *A- li- hukum- iw- a kesi ake na jaji nkuu.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | iliyopita | | tendewa | |

(Alihukumiwa kesi yake na jaji mkuu).

49c) *Va- li- salim- iw- a na Raisi Obama wa Merikani.*

| | | | | |
|---------|-----------|-------|---------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| wingi | iliyopita | | tendewa | |

(Walisolimiwa na Rais Obama wa Merikani).

c) Kauli ya kutendeka

Mofimu ya kauli ya kutendeka katika vitenzi vya kigeni ni {k}. Lakini kutegemea kiambishi cha mzizi wa kitende cha huweza kubadilika kwa njia mbalimbali kama tulivyoona hapo juu katika kauli ya kutendewa/kutendwa.

Iwapo mzizi utaishia na vokali **-i-** au **-e-** basi huongezewa mofimu {k} na {a} ya kiishio kama ahidi-k-a, amini-k-a, samehe-k-a, safiri-k-a, shawishi-k-a.

Lakini kama mzizi unaishia na vokali **-u** basi vokali hiyo **-u-** inabadilika na kuwa **-i-**, ikifuatiwa na kiambishi **-k-** na kiishio **-a**. Mifano dhulumu- dhulumika, haribu-haribika, ruhusu-ruhusika, fudhu-fudhika (fuzu-fuzika) nk.

Kwa vitenzi vinavyoishia na vokali zaidi ya moja basi huongezwa alomofu **{lik}** ya kauli ya kutendeka kama sahau-sahaulika, dharau-dharaulika nk.

Mifano ya sentensi katika kauli ya kutendeka:

50a) *Safari a eo i - li- safir- ik- a kwa udhuri.*

| | | | | |
|-----------------------------|-------------------|-------|------------------|---------|
| Kiambishi cha upatanishi | njeo iliyopita | mzizi | kauli tendeka | kiishio |
|-----------------------------|-------------------|-------|------------------|---------|

(Safari ya leo ilisafirika vizuri.)

50b) *Ndhigo wake u - li- sahau- lik- a garini.*

| | | | | |
|-----------------------------|-------------------|-------|------------------|---------|
| Kiambishi cha upatanishi | njeo iliyopita | mzizi | kauli tendeka | kiishio |
|-----------------------------|-------------------|-------|------------------|---------|

(Mzigo wake ulisahaulika garini.)

50c) *Mwene duka a - li- faid- ik- a na magunia a bure a sukari.*

| | | | | |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mzizi | kauli tendeka | kiishio |
|------------------|-------------------|-------|------------------|---------|

(Mwenye duka alifaidika na magunia ya bure ya sukari.)

d) Kauli ya Kutendesha

Katika kauli hii nayo inafuata mfumo huo huo wa vitenzi vyenye asili ya kigeni kama tulivyoona hapo mbeleni. Iwapo mzizi wa kitenzi unaishia na vokali **-i** au **-e** basi kauli ya kutendesha ya mofimu **{sh}** hutumika ikifuatiwa na kiishio **-a**. Kama; faidi-faidi-sh-a, ahidi-ahidi-sh-a, starehe-sh-a, dhidi- dhidi-sh-a (zidisha), adili-adili-sh-a nk.

Kwa mzizi wa kitenzi unaoishia na vokali **-u**, basi vokali hiyo **-u-** hudondoshwa na kuchukua vokali **i** na mofimu **{k}** ikifuatiwa na kiishio **-a**: hesabu-hesab-i-sh-a, jibu-jib-i-sh-a, amuru-amur-i-sh-a, a, starehe-stareh-e-sh-a nk.

Kwa vitenzi vya kigeni vyenye kuishia na vokali zaidi ya moja basi alomofu {lish} hutumika ikifuatiwa na kiishio -**a**: sahau-lish-a, dharau-lish-a nk.

Mifano ya kauli ya kutendesha katika sentensi:

51a) Mwalimu a - li- mu - amur- ish - a mwanafundi a- simam- e.

| | | | | | | | | |
|------------------|-------------------|---------|-------|-------------------|---------|------------------|-------|-------------------------------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mtendwa | mzizi | kauli tendesha | kiishio | nafsi 3 umoja | mzizi | kiishio dhamira amrishi |
|------------------|-------------------|---------|-------|-------------------|---------|------------------|-------|-------------------------------|

(Mwalimu alimuamrisha mwanafunzi asimame).

51b) Askari a - li - mu - adhib - ish - a sana mwidhi.

| | | | | | |
|------------------|-------------------|---------|-------|-------------------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mtendwa | mzizi | kauli tendesha | kiishio |
|------------------|-------------------|---------|-------|-------------------|---------|

(Askari alimuadhibisha sana mwizi).

51c) A- li - i- sahau - lish - a kama ana kadhi a ku - fany - a.

| | | | | | | | | | |
|------------------|-------------------|--------|-------|-------------------|---------|------------------|--------------|-------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | jireja | mzizi | kauli tendesha | kiishio | nafsi 3 umoja | mofimu ku | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|--------|-------|-------------------|---------|------------------|--------------|-------|---------|

(Alijisahaulisha kama ana kazi ya kufanya).

e) Kauli ya kutendana na kutendeana

Vitenzi vyenye asili ya kigeni katika kauli ya kutendana na kutendeana huwa hazonyeshi tofauti kwa mofimu zinazochukua, kama tulivyoona kwa kauli ya kutendwa na kutendewa, huwa sawa.

Mofimu inayotumika ni {an}. Iwapo vitenzi vinaishia na mofimu {i} au{e} basi huongezwa mofimu {an} na mwisho kiishio -**a**. Kama shawishi-an-a, ahidi-an-a, amini-an-a, safiri-an-a, starehe-an-a nk. Kwa mzizi unaoishia na vokali -**u**, sheria ni ileile -**u**- hubadilika na kuchukua vokali -**i**-, ikiongezwa na -**an** ya kutendana/kutendeana na mwisho kiishio -**a**; dhulumu-dhulum-i-an-a, hukumu-hukum-i-an-a, husu-hus-i-an-a, adhibu- adhib-i-an-a nk. Aidha kwa vitenzi vyenye vokali zaidi ya moja ya kiishio alomofu inayotumika ni {lian} : sahau-lian-a, dharau-li-an nk.

Mifano ya kauli ya kutendeana na kutendana katika sentensi:

52a) *Va - li - ahidi- an a ku - lip - an - a deni lavo wiki ijao.*

| | | | | | | | |
|-----------------------|--------------------|-------------------|---------------|-------------------|------------------|-------------------|---------|
| Nafsi 3 njeo wingi | mzizi iliyopita | kauli tendeana | kiishio ku | mofimu tendana | mzizi tendana | kauli tendeana | kiishio |
|-----------------------|--------------------|-------------------|---------------|-------------------|------------------|-------------------|---------|

(Waliahidiana kulipana deni lao wiki ijayo).

52b) *Maria na Alii hu- husi - an - a kidamu.* (Maria na Ali huhusiana kidamu.)

| | | | |
|-------------------|-------------------|-------------------|---------|
| Hali ya mazoea | mzizi tendeana | kauli tendeana | kiishio |
|-------------------|-------------------|-------------------|---------|

52c) *Hassani na Husseni hu - shiriki - an - a kibiashara.*

| | | | |
|-------------------|-------------------|-------------------|---------|
| Hali ya mazoea | mzizi tendeana | kauli tendeana | kiishio |
|-------------------|-------------------|-------------------|---------|

(Hassan na Hussein hushirikiana kibiashara).

52d) *Ndrugu va - li - sahau - lian - a baada a ku - pote- an- a kwa muda nrefu.*

| | | | | | | | |
|-----------------------|--------------------|-------------------|---------------|-------------------|------------------|-------------------|---------|
| Nafsi 3 njeo wingi | mzizi iliyopita | kauli tendeana | kiishio ku | mofimu tendana | mzizi tendana | kauli tendeana | kiishio |
|-----------------------|--------------------|-------------------|---------------|-------------------|------------------|-------------------|---------|

(Ndugu walishauliana baada ya kupoteana kwa muda mrefu).

Ikumbukwe kuwa vitenzi nya kukopwa haviwezi kunyambuliwa katika hali zote kama vilivyo vitenzi vyenye asili ya Kibantu, na ndiyo maana tumeangalia vitenzi hivyo katika zile kauli ambazo zinaweza kunyambuliwa.

4.5 Hitimisho

Sura hii imejikita katika kuangalia kitenzi na mofolojia yake. Kitenzi kimeangaziwa kwa upande wa maana na aina zake mbalimbali. Mofolojia ya kitenzi imehusishwa kwa kuangalia viambishi awali na viambishi tamati vinavyoweza kuambishwa katika kitenzi cha Kitikuu. Viambishi awali ni viambishi vinavyoambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi, katika Kitikuu ni mofimu kama za: njeo, hali, dhamira za masharti, ukanushi, nafsi, viambishi vipatanishi, viambishi nya yambwa, rejeshi nk. Viambishi tamati ni viambishi vinavyoambishwa baada ya mzizi wa kitenzi. Kitikuu huambisha viambishi tamati kama viambishi nya dhamira, viambishi rejeshi, viambishi nya vimalizio, viambishi nya

mnyambuliko na viambishi kanushi. Viambishi au mofimu zote hizo zimeangaziwa katika sura hii. Vilevile muundo wa sentensi za Kitikuu na muundo wa mizizi ya vitenzi vyta Kitikuu pia vimeangaziwa.

SURA YA TANO

UWASILISHAJI WA NA UCHANGANUZI WA DATA

5.0 Kitangulizi

Katika mada iliyotangulia tumeangalia kitenzi cha Kitikuu na mofolojia ya kitenzi hicho kwa kuangazia viambishi awali na tamati katika kitenzi cha Kitikuu. Hapa uchanganuzi wa kina wa njeo, hali na dhamira katika lahaja ya Kitikuu umeainishwa. Kwanza uchanganuzi wa njeo, hali na dhamira za Kitikuu katika sentensi sahili zimewasilishwa, zenyе kuchukua kitenzi kimoja mara nyingi. Baadaye tumeangalia muingiliano wa njeo, hali na dhamira katika sentensi za Kitikuu ambapo vitenzi viwili au hata zaidi vikitumika. Vilevile katika sura hii imeangazia uchanganuzi wa nadharia ya ukaguzi wa sifa inavyofanya kazi katika lahaja hiyo hasa kwa kurejelea hali, njeo na dhamira na muingiliano wake. Kama tulivyoona kitenzi cha Kitikuu kinaweza kubeba mofimu mbalimbali, basi mofimu hizo zinaweza kukaguliwa katika hatua mbalimbali ili kuhakikisha sentensi iko sawa kisarufi katika lahaja hiyo.

5.1 Njeo

Njeo ni kiambishi kinachotoa habari juu ya tendo kufanyika katika muda maalum. Njeo hurejelea wakati tendo linafanyika kwa kurejelea wakati wa uneni /usemi. Lazima kuwe na kirejelezi hicho cha usemi ndipo tuweze kusema kama tendo lilifanywa kabla ya usemi, wakati wa usemi, au baada ya usemi. Ni muhimu kukumbuka kuwa njeo ni dhana ya kisonde, kwa maana ya kuwa tendo huonyeshwa kwa muktadha wa mzungumzi anapozungumza wakati wa sasa. Kulingana na nadharia ya Reichenbach (1947) ya njeo, njeo huonyesha uhusiano wa aina mbili katika mstari wa kiwakati, nazo ni wakati wa usemi na wakati wa tendo.

Payne (1997:236) anafasili njeo, kama kipashio cha kisarufi chenye kuonyesha uhusiano wa muda wa tendo kufanyika na kirejelezi cha wakati fulani, mara nydingi huwa ni wakati wa usemi.'

Comrie (1976:5), naye anazungumzia kuwa njeo ni kategoria ya kisonde, ambayo huonyesha tendo na wakati, kawaida inayohusishwa na wakati wa sasa. Dahl (1985:25) anasema, njeo hakika ni kategoria ya kisonde, kwa kuwa huhusisha wakati wa tendo na wakati wa usemi.

Kwa hivyo sifa ya usonde ya njeo inahusisha wakati wa usemi wa mzungumzaji ambacho ndicho kirejelezi cha uhusiano wa njeo inayohusiana. Wakati wa usemi inakuwa ndio njeo ya sasa au iliyopo, na iwapo ni kabla ya usemi ni njeo iliyopita na kama ni baada ya usemi, basi ni njeo ijayo. Mchoro ufuatao wa wakati unaonyesha uhusiano huo:

Njeo iliyopita

← _____ | _____ →

Njeo ijayo

Kabla

Sasa (wakati wa usemi)

Baada

(Lyons, 1968: 305 na Comrie, 1985:6)

Katika kielelezo hicho cha wakati kinaonyesha ‘sasa’, kama wakati wa usemi na ‘kabla’ ikiwa ni kabla ya usemi na ‘baada’ kwa maana ya baada ya usemi.

Sasa, ndiyo huchukuliwa kuwa kirejelezi cha njeo, na hivyo kitovu cha usonde. Comrie (1985:122) huziita njeo zinazotumia wakati wa sasa au wa usemi kiurejelezi kama njeo halisi. Mbali na njeo halisi, kuna zile zinazojulikana kama njeo rejelezi ambazo ni migawanyo ya njeo inayorejelea pointi ya urejelezi au inayofuatia wakati wa usemi lakini hairejelei kitovu usonde au usemi wa sasa (Givon, 2001:286 na Comrie, 1985: 125). Lakini kwa upande wa njeo rejelezi inakanganya na hali (Dahl, 1985:23-26). Kwa

mintarafu hiyo, kazi hii itaangalia njeo halisi na kuangalia hali kivyake. Muingiliano wa njeo halisi na hali mbalimbali zitaangaziwa katika kazi hii baadaye.

5.1.1 Njeo na Wakati

Wataalam mbalimbali wanachanganya dhana ya njeo na wakati, kwa hivyo ni muhimu tuangalie tofauti kati ya dhana hizi ili tuweze kuzitofautisha na sio kuzitumia kama visawe. Ni muhimu kutofautisha dhana ya njeo kama kategoria ya kisarufi, ilihali dhana ya wakati ni tukio lenyewe la kuashiria wakati (Lindfors, 2003). Kila jamii ina njia zake za kuelezea dhana ya wakati.

Njeo ni kipashio ambishi cha kisarufi kinachopachikwa katika kitenzi, chenye kuonyesha wakati, ikirejelea wakati wa usemi ambaeo ni sasa.

Wakati mara nyingi hujibu swali la **lini** ambalo swali hilo huweza kujibiwa kwa leksika za vielezi kama baada ya, jioni, alfajiri, kesho, juzi, sasa hivi, saa kumi au kutumika pamoja na viambishi vya njeo na hata hali wakati mwingine kama **{na}**, **{li}**, **{ta}**, **{hu}** katika Kiswahili Sanifu.

Kwa hivyo, ni makosa kuchukulia wakati kama kisawe cha njeo kama wanavyofanya wataalam wengine.

5.1.2 Njeo katika Kitikuu

Kila lugha ina njeo zake ambazo zinaweza kutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Kitikuu kina njeo tatu ambazo ni:

- i) Njeo iliyopo
- ii) Njeo iliyopita
- iii) Njeo ijayo

5.1.2.1 Njeo Iliyopo

Njeo iliyopo huwa inazungumzia matukio yanayotukia wakati wa usemi, yaani pale ambapo jambo linapozungumziwa ndilo tendo huwa hutendeka. Iwapo tendo linaendelea kutendeka kwa muda au vipi hayo yanakuwa, ni mambo ya hali.

Kwa hivyo kila mara tukizungumzia juu ya njeo iliyopo, Kitikuu zaidi hutumia hali na sio njeo iliyopo kama tutakavyoona. Wataalam kama Bybee na wenzake (1994) wanaonelea ni bora kutoiita njeo iliyopo bali kuiangalia kama hali mbalimbali.

Wanasema, (Bybee na wenzake, 1994) wakati wa sasa unaweza kudhihirisha :

- a) Hali ya kuendelea au
- b) Hali ya mazoea

Wanadai kuwa wakati wa sasa unaonyeshwa na hali zenye kuonyesha wakati wa sasa usio dhahiri. Besha (1989), naye anakiri kuwa ni shida kukadiria njeo iliyopo, kwani inatakikana iwe sambamba na wakati wa sasa wa usemi, na ndiyo maana si rahisi kuwa na njeo iliyopo bali hali inayoweza kusaidiwa na vielezi mbalimbali vyta wakati kama ‘sasa’.

Bybee na Dahl (1985) wanadai kuwa lugha nyingi za ulimwengu hazitumii viambishi (mofimu) vyta njeo kuonyesha njeo iliyopo.

Kitikuu kwa nadra, huweza kutumia mofimu **{a}** katika kudhihirisha njeo iliyopo, isiyodhahiri na hujitokeza katika nafsi zote, lakini kwa kawaida hujitokeza katika vitenzi visaidizi.

53a) *Jumaa a – a – wedh- a ku - kimbi - a mbio.*

| | | | | | | |
|---------|---------|-------|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kiishio | kitenzi | mzizi | kiishio |
| umoja | iliyopo | | | kisoukomu | | |

(Jumaa aweza kukimbia mbio).

Kina Jumaa va- a- wedh - a ku- kimbi- a mbio.

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio kitenzi mzizi kiishio
wingi iliyopo kisoukomo

(Akina Jumaa waweza kukimbia mbio)

53b) *Mwanae a - a- pend- a ku - l- a bodo kwa isi.*

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
umoja iliyopo kisoukomo

(Mtoto wake apenda kula ugali kwa samaki)

Vanave va - a- pend- a ku- l - a bodo kwa isi.

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
wingi iliyopo kisoukomo

(Watoto wake wapenda kula ugali kwa samaki).

53c) *Ni a- tak- a → nataka ku- fu- a nguvo sasa.*

Nafsi 1 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
umoja iliyopo kisoukomo

(Nataka kufua nguo sasa.)

Chu- a- tak- a → chwataka ku- fu- a nguvo sasa.

Nafsi 1 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
wingi iliyopo kisoukomo

(Twataka kufua nguo sasa.)

Katika sentensi (53a) na (53b) vitenzi **awedha** na **apenda** kuna kudondoshwa kwa vokali {a-} ya kwanza katika mageuko ya kifonolojia, kwani kuna mofimu {a} ya nafsi ya tatu umoja ikifuatiwa na {a} ya hali iliyopo isiyo dhahiri hivyo -a- hizo mbili zikifuatana kuna kudondoshwa kwa vokali {a-} ya kwanza ili kurahisisha matamshi:

Sheria : /a/ → /∅/ /-/a/

Sentensi (53c) kwa umoja, vitenzi **nataka** kuna kudondoshwa kwa mofimu /i/ katika

Kitikuu ili kurahisisha matamshi kwa sababu ya kufuatana kwa vokali hizo mbili za /i/ na /a/ :

Sheria: /i/ → /∅/ /-/a/

/ni-a-tak- a/ → /nataka/

Sentensi (53c) katika wingi, mofimu ya nafsi ya kwanza wingi ni **{chu}** ikifuatiwa na mofimu ya njeo iliyopo **{a}** mageuko ya kimofonolojia ya uundaji wa kiyeyusho hujitokeza:

Sheria : /u/ → /w/ / -/a/

/tʃu- a-tak-a/ → /tʃwataka/

53d) Uwe u - **a** - wedh- a → wawedha ku - imb - a kwa udhuri.
 Nafsi 2 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
 umoja iliyopo kisoukomo

(Wewe waweza kuimba kwa uzuri.)

Ini mu- a - wedh- a → mwawedha ku- imb- a kwa udhuri.
 Nafsi 2 njeo mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
 umoja iliyopo kisoukomo

(Nyinyi mwaweza kuimba vizuri)

Katika sentensi ya (53d), kitenzi -wedha katika umoja na wingi, mageuko yamejitokeza ya uundaji wa kiyeyushi ambapo katika umoja na wingi, vokali **{u}** inapokumbana na vokali **{a}** huunda kiyeyushi **{w}** katika lahaja hii.

Sheria : /u/ → /w/ / -/a/

/u- a- wedh-a / → /wataka/ /mu – a- wedh-a / → /mwawedha/

Kwa upande wa Kiswahili Sanifu, wataalam wengi kama Mgullu (1999), Waihiga (1999), Mohammed (2001) na Polome (1967) wanassema mofimu **{na}** ni mofimu ya njeo iliyopo lakini kwa hakika mofimu **{na}** ni hali zaidi ya kuendelea, kuliko njeo iliyopo:

Mfano: Amina **anacheza densi**.

Fundi **anajenga jumba kubwa**.

Ijapokuwa katika Kiswahili Sanifu tunaweza kupata katika baadhi za sentensi ambapo tunaweza kudai kuwa tendo linatendeka sawia na wakati wa usemi. Mathalan katika matangazo ya michezo kama kandanda, mpira wa kikapu, voliboli nk.

Mfano: Hamisi **anampasia** Ogola mpira.

Mariga **anaelekea** kwenye lango.

Matano ana mpira, **anaenda** nao

Au sentensi zifuatazo:

Maria **anamvalisha** mgeni wa heshima koja.

Mwalimu **anampatia** mwanafunzi bora zawadi.

Sentensi kama hizo zinaweza kuonekana kama tendo linafanyika wakati wa usemi, lakini hatuwezi kusema linafanyika na kukamilika wakati wa usemi, chembilecho Comrie (1985:9) anasema si rahisi kwa tendo kutokea wakati ule ule wa usemi na kukamilika wakati ule ule.

Lahaja ya Kitikuu ni tofauti na Kiswahili Sanifu, kwani lahaja hii haina mofimu {na} ya hali ya kuendelea au kama wengine wanavyodai ya njeo iliyopo bali hutumia mofimu {hu} kuonyesha hali ya kuendelea ambayo pia ni mofimu ya mazoea kama tutakavyoona tutakapoangalia hali.

54a) Baba **hu -** som- a gadheti sasa. (Baba anasoma gazeti sasa).

Hali ya mzizi kiishio
kuendelea

54b) Fatuma **hu-** imb- a wimbo wa taifa.

Hali ya mzizi kiishio
kuendelea

(Fatuma anaimba wimbo wa taifa).

54c) Mwalimu **hu -** som- esh- a vanafundi kwa udhuri.

Hali ya mzizi kauli ya kiishio
kuendelea tendesha

(Mwalimu anasomesha wanafunzi vizuri).


Kulingana na kanuni ya sifa chini ya nadharia ya Uminimalisti sifa za kisarufi hukaguliwa na kusogezwa katika hatua mbalimbali ili kubaini usarufi wa vipashio katika sentensi. Ukaguzi na usogezi hutegemea uimara au udhaifu wa lugha kimofolojia. Kitikuu ni lahaja imara yenyе ukwasi wa kimofolojia kwa kuwa ni lugha ambishibainishi, kwa hivyo tunatarajia kuwe na usogezi wa kukagua sifa mbalimbali. Usogezi huchochewa na sifa za kimofolojia ambazo hupatikana katika kitensi na sifa za kileksika hupatikana katika uhusika. Kitensi ndicho kiungo muhimu katika sentensi yoyote ile, na hivyo sifa zake za kisarufi kama njeo, hali, yambwa, dhamira, kiima na kadhalika husogezwa kwenye vifundo vyake vya uzalishaji. Sifa za uhusika za kiima na yambwa zinazoonekana na kujisimamia husogezwa kwenye spesifaya za kirai cha upatanishi kiima au yambwa ili kukagua sifa za uhusika.

Sentensi 53a) inaweza kuainishwa katika kielelezo matawi kama kifuatavyo:

53a) *Jumaa awedha kukimbia mbio.* (Jumaa aweza kukimbia mbio).

Jumaa a - a - wedh- a → awedha ku - kimbi - a mbio.

| | | | | | | | |
|------------------|-----------------|-------|---------|---------------------|---------|-------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopo | mzizi | kiishio | mofimu kisoukomu | kitenzi | mzizi | kiishio |
|------------------|-----------------|-------|---------|---------------------|---------|-------|---------|



Katika kielelezo matawi hiki kiima ‘*Jumaa*’ kinakaguliwa kutoka spesifaya ya kirai tenzi na kuacha athari kiima (ak), kinahamishwa hadi spesifaya ya kirai upatanishi kiima, na kukagua sifa ya kiima na kubaki hapo. Kitensi kisaidizi ‘*awedha*’ kinasogezwa kutoka kichwa cha kitensi hadi kirai cha upatanishi yambwa kupima yambwa kisha kinasogezwa tena kukagua njeo iliyopo {a} na kuacha athari (at) na hatimaye husogezwa kukagua sifa ya kiima {a} katika UPk ya UPk¹ na kubaki hapo. Mofimu {a} husimamia mofimu ya kiima na vilevile ni ya njeo iliyopo kwa hivyo kuna kudondoshwa kwa mofimu moja kwa sababu ya kurahisisha matamshi. Kitensi kisoukomu ambacho ni kitensi kikuu, ‘*kukimbia*’ kinasogezwa kutoka kitensi (T) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya yambwa, kinasogezwa tena hadi kichwa cha kitensi kisoukomu (KU) kukagua sifa ya kitensi kisoukomu na kusogezwa na kuishia kwenye upatanishi kiima (UPk ya UPk¹).

5.1.2.2 Njeo Iliyopita

Njeo hii huonyesha kuwa tendo lilifanyika wakati uliopita wa nyuma kabla ya usemi. Shopen (1995:204) anadai kuwa njeo iliyopita inatumiwa kwa matukio kabla ya muda wa mazungumzo. Kwa kweli njeo iliyopita ni kabla ya mazungumzo, kabla ya wakati wa sasa. Lahaja ya Kitikuu, kama Kiswahili Sanifu hutumia mofimu {li} katika kuonyesha njeo iliyopita. Katika Kitikuu, mofimu awali za nafsi zikitumiwa na njeo {ta}, hali {ndo}, na dhamira {ka} basi mofimu ya umoja huweza kudondoshwa; lakini kwa njeo iliyopita, Kitikuu hakiwezi kudondosha mofimu ya {li} katika umoja wala wingi. Mifano: *Imi Øtakuya kesho.* (Mimi nitakuja kesho), *Halima Øndokula.* (Halima amekula), *Hamisi alikuya Økakoa, Økala, Økaiyala.* (Hamisi alikuja akaoga, akala, akalala).

Katika ukanushi mofimu {li} haitumiki bali mofimu {ku} huchukua nafasi hiyo ya njeo {li}.

55a) *Hamisi a - li - safiri yana iyoni.* (Hamisi alisafiri jana jioni.)

| | | |
|---------|-----------|-------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi |
| umoja | iliyopita | |

Kan. *Hamisi ha - ku - safiri yana iyoni.* (Mtoto wake hakusafiri jan jioni).

| | | |
|-----------|----------------|-------|
| Kiambishi | ukanushi | mzizi |
| kanushi | njeo iliyopita | |

55b) *Amina na Jumaa va - li- nunu- a dhitabu.*

| | | | |
|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kiishio |
| wingi | iliyopita | | |

(Amina na Jumaa walinunua vitabu).

Kan. *Amina na Jumaa ha - va - ku - nunu - a dhitabu.*

| | | | | |
|-----------|---------|----------------|-------|---------|
| Kiambishi | nafsi 3 | ukanushi | mzizi | kiishio |
| kanushi | wingi | njeo iliyopita | | |

(Amina na Jumaa hawakununua vitabu).

55c) *Nchi u - li - kach - w - a yudhi.* (Mti ulikatwa juzi).

Ngeli ya njeo mzizi kauli kiishio
upatanishi iliyopita

Kan. *Nchi ha - u- ku - kach - w - a yudhi.*

Kiambishi ngeli ya ukarushii mzizi kauli kiishio
kanushi upatanishi njeo iliyopita

(Mti haukukatwa juzi).


Katika Kitikuu, njeo iliyopita haionyeshi tendo limepita kwa muda gani na kama limekamilika au la. Hapa tunaangalia njeo iliyopita kwa Kitikuu katika sentensi sahili tu, baadaye tutaangalia muingiliano wa njeo na hali na hata dhamira katika miktaadha mbalimbali.

Kielelezo matawi cha 55a) ni kama kifuatacho hapo chini:

55a) *Hamisi alisafiri yana iyoni.* (Hamisi alisafiri jana jioni.)

55a) *Hamisi a - li - safiri yana iyoni.*

Nafsi 3 njeo mzizi
umoja iliyopita



Kiima ‘*Hamisi*’ kinasogezwa kutoka spesifaya ya kitenzi kikiacha athari ya kiima hadi spesifaya ya kirai upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi ‘*alisafiri*’ kinasogezwa

kutoka kitenzi (T ya T¹) na kuacha athari ya kitenzi hadi njeo (NJ ya NJ¹) kukagua sifa ya njeo iliyopita {li} na kuacha athari na mwisho kuishia katika upatanishi kiima (UPk ya UPk¹) kukagua sifa ya kiima na kubaki hapo. Vielezi ‘yana iyoni’ vinabaki chini ya kichwa cha kitenzi (T¹) chini ya kielezi (KE) na havisogezwi kwa sababu havina sifa za kimofolojia vya kuweza kusogezwa.

5.1.2.3 Njeo Ijayo

Njeo ijayo huonyesha kutendeka kwa tendo baada ya wakati huu wa usemi. Ni matumaini kuwa jambo fulani litatendeka baada ya muda wa uneni. Kama njeo iliyopita, haielezei kama litatendeka na kukamilika wakati gani katika sentensi sahili. Pengine kwa matumizi ya vielezi zaidi tendo hilo linaweza kupewa sifa zaidi, lakini kwa njeo ijayo haina maelezo mengi. Katika muktadha wa sentensi yenye kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi basi kutakuwa na matumizi ya njeo, hali na hata dhamira mbalimbali basi maelezo zaidi yataweza kupatikana kama tutakavyoona baadaye.

Katika lahaja ya Kitikuu mofimu ya njeo ijayo ni {ta} katika hali yakinishi na katika ukanushi mofimu hiyo haipatikani, tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo mofimu hiyo inapatikana katika ukanushi. Ukanushi wa njeo ijayo katika lahaja ya Kitikuu, inakuwa kama ukanushi katika ile hali ya kuendelea katika Kiswahili Sanifu (**hali –na**).

56a) *Halima a - ta - som - a kitabu cha hadisi.*

| | | | |
|------------------|---------------|-------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo ijayo | mzizi | kiishio |
|------------------|---------------|-------|---------|

(Halima atasoma kitabu cha hadithi).

Kan. *Halima ha - som - i kitabu cha hadisi.*

| | | | |
|----------------------|-------|---------|---------|
| Kiambishi kanushi | mzizi | kiishio | kanushi |
|----------------------|-------|---------|---------|

(Halima **hatasoma** kitabu cha hadithi).

56b) *Iguu lake li - ta - kach - w- a kesho.*

| | | | | |
|---------------|-------|-------|--------|---------|
| Ngeli | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| ya upatanishi | ijayo | | tendwa | |

(Mguu wake utakatwa kesho).

Kan. *Iguu lake ha - li - kach - w - i kesho.*

| | | | | |
|-----------|------------|-------|--------|---------|
| Kiambishi | ngeli ya | mzizi | kauli | kiishio |
| kanushi | upatanishi | | tendwa | kanushi |

(Mguu wake hautakatwa kesho).

56c) *Dhiachu dhi - ta - shon - w - a.* (Viatu vitashonwa).

| | | | | |
|------------|-------|-------|--------|---------|
| Ngeli ya | njeo | mzizi | kauli | kiishio |
| upatanishi | ijayo | | tendwa | |

Kan. *Dhiachu ha - dhi - shon - w - i.* (Viatu havitashonwa).


| | | | | |
|-----------|------------|-------|--------|---------|
| Kiambishi | ngeli ya | mzizi | kauli | kiishio |
| kanushi | upatanishi | | tendwa | kanushi |

Kielezo matawi cha njeo ijayo kitakuwa kama kifuatavyo, kwa mfano wa 56a) :

56a) *Halima atasoma kitabu cha hadisi.* (Halima atasoma kitabu cha hadithi.)

Halima a - ta - som - a kitabu cha hadisi.

| | | | |
|---------|-------|-------|---------|
| Nafsi 3 | njeo | mzizi | kiishio |
| umoja | ijayo | | |



Nomino ‘*Halima*’ imesogezwa kutoka kwa spesifaya ya kirai tenzi na kuacha athari kiima (ak), hadi spesifaya ya kirai upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi ‘atasoma’, kitasogezwa kutoka kichwa cha kitenzi (T ya T¹) hadi upatanishi yambwa (UPy ya UPy¹) kiache athari, tena kisogezwe hadi kwa njeo (NJ ya NJ¹), kiache athari na mwisho kisogezwe kwa upatanishi kiima (UPk ya UPk¹) na kibaki hapo. ‘*Kitabu cha hadisi*’ ni yambwa ambayo itasongezwa kutoka nomino ya kitenzi na kiache athari (ay), na kisogezwe hadi spesifaya ya kirai upatanishi yambwa kupima sifa ya uhusika yambwa na kibaki hapo.


5.2 Hali

Hali kama njeo ni kategoria ya kisarufi inayopatikana katika kitenzi. Lyons (1977), anadai kuwa watoto wanapata hali haraka sana wanapojojifunza lugha yao ya kwanza ikilinganishwa na njeo, akisema kuwa hali ni ya kimsingi zaidi. Anadai kuwa kuna baadhi za lugha ambazo zina hali pekee na hazina njeo. Dholuo, nchini Kenya, kwa mfano ni lugha mojawapo yenyе hali bila njeo katika sarufi yake (Ochola, 2003:77), lugha za Burmese na Dyrbal (Comrie, 1985:51) ni mifano ambayo haina mofimu za njeo katika vitenzi vyake bali ni hali na dhamira pekee.

Lugha mbalimbali huwa na sifa zake kwa upande wa matumizi ya njeo, hali na dhamira. Kuna zile lugha ambazo zina msikiko zaidi wa njeo, nyengine zina msikiko zaidi wa hali na nyingine zina msikiko wa dhamira. Bybee (1985:3) katika utafiti wake wa lugha hamsini alizozifanyia utafiti, aligundua kuwa asilimia 74 ya lugha hizo zilidhirisha, vitenzi vyake kimofolojia zimebeba mofimu za hali, dhamira ilikuwa ya tatu yenyе asilimia 68 na njeo ilikuwa ya saba yenyе asilimia 50. Kwa upande wa Kitikuu, ni lahaja yenyе msikiko zaidi wa hali ikilinganishwa na njeo na dhamira.

Hali hujihusisha na wakati wa tendo bila kurejelea wakati wa usemi. Lyons (1969:315) anaeleza kuwa ‘..... njeo ikiwa ni kategoria ya usonde, inayojihusisha na wakati wa usemi, hali si ya usonde.’ Hali haihusishi na kuangazia tendo na wakati wa usemi au uzungumzi kama ilivyo njeo.

Comrie (1976:3) anatoa fasili ya hali kuwa ni kuangalia jinsi mbalimbali ya kiwakati ya hali husika. Hali inaweza kuangaliwa kama iliyokamilika au isiyokamilika na haiangaliwi kwa kurejelea usemi wa sasa. Comrie anatoa mfano: **John alikuwa anasoma nilipoingia**: hapa kitenzi cha kwanza kinatoa utangulizi wa hali fulani na hali hiyo baadaye inaelezewa na kitenzi cha pili. Hapa John alikuwa anasoma katika hali hiyo ya kuendelea ndio mwalimu akaingia. Comrie (Ibid: 25) amechora mgao wa hali kuonyesha vile inavyoweza kugawanywa kutoka sehemu mbili kuu ya hali timilifu na isiyo timilifu, kwa marekebisho kidogo kukidhi lahaja ya Kitikuu:



5.2.1 Hali katika Kitikuu

Hali katika Kitikuu inaweza kugawanywa kwa ule mgao mkuu ambao ni bia; wa timilifu na iso timilifu. Katika lahaja hii kuna hali timilifu moja na hali zisizo timilifu kadhaa. Hali zisizo timilifu ni hali ya mazoea, hali ya kuendelea, hali ya ki- (ya kuendelea na masharti), hali ya mfululizo na hali ya kurudia rudia.

5.2.1.1 Hali Timilifu

Hali timilifu hudhihirisha kutimilika kwa tendo. Reichenbach (1947) anasema wakati wa tendo huwa umetanguliwa na wakati wa urejelezi. Hii ni kumaanisha kuwa tendo hutendeka na kukamilika na baadaye likaweza kuelezwu katika muktadha wa mazungumzo. Comrie (1976) anasema mara nyingi sifa ya hali timilifu inaonyesha kukamilika kwa tendo. Huonyesha kuwa tendo tayari limetendeka kabla ya kutolewa kwa taarifa na athari zake zinaweza kuwa bado zinaonekana. Kwa mfano: Mtoto ametapika: huonyesha kuwa mtoto ametapika muda mfupi uliopita na athari zake bado zinaonekana.

5.2.1.2 Hali timilifu katika lahaja ya Kitikuu

Kitikuu kina mofimu mbili za hali timilifu ambazo ni {-ndo-} na {-ie}. Mofimu ya kwanza ndiyo inayotumiwa na Watikuu wengi lakini kuna Watikuu kama wa sehemu za Ndaa na Kiwayuu ambao hutumia {-nda-} badala ya {-ndo-}. Kwa mujibu ya kazi hii tutajikita zaidi kwa mofimu {ndo}, kwani ndiyo inayotumiwa na Watikuu wengi na kulingana na data tuliookusanya wametumia mofimu ya {ndo} au {ie} kuonyesha hali timilifu.

Mofimu {ndo} huonyesha tendo limekamilika muda mfupi uliopita, lakini mofimu {ie} huonyesha kuwa tendo limefanyika na kukamilika muda mrefu zaidi ukilinganishwa na wa -ndo-. Hata hivyo, ni muhimu kutaja kuwa muda huo si mrefu sana mpaka kupita siku ya pili, inakuwa ni siku ile ile. Madai haya yanaungwa mkono na Wald (1973), kuwa kiambishi cha kitenzi -ie huonyesha muda uliopita wa siku hiyo hiyo ya kuzungumzwa. Mofimu zote mbili za hali timilifu huonyesha tendo limefanyika na kukamilika, lakini matokeo yake bado yanaonekana yenye umuhimu kwa sasa.

Hali ya kukamilika huweza kutumiwa na njeo iliyopita na ijayo, lakini hayo tutayaangalia baadaye kuonyesha kuingiliana kwa njeo na hali na hali nyingine.

Nurse (1982:116) naye anatilia mkazo swala hili kwa kuonyesha hali timilifu hizi mbili na tofauti yazo kuwa ya **-ndo** ni muda mfupi uliopita na **-ie** ni muda kidogo mrefu uliopita ukilinganishwa na **-ndo-** lakini zote huonyesha kukamilika kwa tendo.

5.2.1.3 Mofimu ya hali timilifu {-ndo-}

Katika lajaja hii tunapotumia mofimu ya hali timilifu ya **{ndo-}** inaweza kutumiwa bila kiambishi cha nafsi, hasa pale nafsi husika iwe imetajwa tayari, na inakuwa katika hali ya umoja, kwani kwa wingi mara nyingi kiambishi cha nafsi wingi huwekwa:

57a) *Jumaa a - ndo - kw- endr- a sokoni. pia Jumaa øndokwendra sokoni.*

Nafsi 3 hali kiambishi mzizi kiishio
umoja timilifu cha ku-

(Jumaa ameenda sokoni)

57b) *Ni - ndo - ku - l - a wali ote.* (Nimekula wali wote.)

Nafsi 1 hali kiambishi mzizi kiishio
umoja timilifu cha ku-

57c) *U - ndo - ku - l - a chakula?* (Umekula chakula?)

Nafsi 2 hali kiambishi mzizi kiishio
umoja timilifu cha ku-

Katika sentensi ya 57a) mofimu/ kiambishi cha nafsi kinaweza kuwekwa au kudondoshwa kwani nomino yenyewe imetajwa; Jumaa, tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo tunaona kiambishi cha nafsi **a-** lazima kiwekwe.

Katika nafsi ya wingi viambishi vya nafsi katika vitenzi havidondoshwi kama inavyofanywa katika umoja:

58a) *Chu - ndo - ku - l - a chakula chote.* (Tumekula chakula chote).

Nafsi 1 hali kiambishi mzizi kiishio
wingi timilifu cha ku-

58b) *Ivo va - ndo - ku - y - a eo.* (Wao wamekuja leo).

Nafsi 3 hali kiambishi mzizi kiishio
wingi timilifu cha ku-

58c) *Mu - ndo - to - a senti dha chama?* (Mumetoa pesa za chama?)

Nafsi 2 hali mzizi kiishio
wingi timilifu

Kwa upande wa ngeli mbalimbali katika umoja kiambishi au mofimu ya umoja inaweza kudondoshwa au ikapatikana, sio lazima lakini katika wingi mofimu ya wingi huwepo:

a) *N'chi u - ndo - kach - w - a.* (*Nchi Øndokachwa*) (Mti umekatwa).

Nge li ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendwa

b) *Michi i - ndo - kach - w - a.* (Miti imekatwa).

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendwa

c) *Iyenyo li - ndo - to - lew - a.* (*Iyenyo Øndotolewa*). (Jino limetolewa).

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendewa

d) *Menyo a - ndo - to - lew - a.* (Meno yametolewa).

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendewa

e) *Kiachu ki - ndo - kach- ik - a.* (*Kiachu Øndokachika*) (Kiatu kimekatika).

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendeka

f) *Dhiachu dhi - ndo - kach - ik - a.* (Viatu vimekatika).

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendeka


Mchoro wa kielelezo matawi cha hali timilifu {ndo} 57a) unaweza kuonyeshwa kama

ifuatavyo:

57a) *Jumaa a - ndo - kw- endr- a sokoni.* Pia: *Juma ḡndokwendra sokoni.*

Nafsi 3 hali kiambishi mzizi kiishio
umoja timilifu cha ku-

(Jumaa ameenda sokoni).



Kiima ‘*Jumaa*’, kinasogezwa kutoka spesifaya ya kirai tenzi hadi spesifaya ya kirai upatanishi kiima (KUPk) kukagua sifa ya uhusika wake na kubaki hapo. Kitenzi ‘*andokwendra*’ kinasogezwa kutoka kifundo cha kitenzi (T ya T¹) hadi kifundo cha hali (HAL ya HAL¹) kukagua sifa ya hali timilifu {ndo}na kuishia katika upatanishi kiima UPk ya UPk¹ ili kukagua sifa ya kiima {a} na kinaishia hapo. ‘*Sokoni*’ kimetumika kama kielezi kwa hivyo hakitasogezwa kwa kutokuwa na sifa za kukaguliwa kitabaki katika E ya T¹.

5.2.1.4 Mofimu ya hali timilifu {-ie}

Katika Kitikuu, iwapo mzizi wa kitenzi una vokali /e/ au /o/ basi huchukua mofimu {ee} ya hali timilifu na iwapo mzizi wa kitenzi una vokali /a/, /i/ au /u/ basi huchukua mofimu {ie} ya hali timilifu. Hali hii ni kulingana na wiano wa vokali ya mifanyiko ya kifonolojia katika lahaja hii, katika juhudhi ya kurahisisha matamshi.

59a) *Ni - l - ie wali ote.* (Nimekula wali wote).

Nafsi 1 mzizi hali
umoja timilifu

59b) *Amini u - gur - ie kwechu.* (Amini amegura kwetu).

Nafsi 1 mzizi hali
umoja timilifu

59c) *Uwe u - som - ee eo?* (Wewe umesoma leo?)

Nafsi 1 mzizi hali
umoja timilifu


59d) *Mwanae u - tuku- dh- ie dhiachu.* (Mtoto wake amechukua viatu).

Nafsi 1 mzizi ngeli ya hali
umoja upatanishi timilifu

Kielelezo matawi cha 59a ni kama kifuatacho:

59a) *Ni - l - ie wali ote.* (Nimekula wali wote).

Nafsi 1 mzizi hali
umoja timilifu



Kielelezo matawi 63a) hakina leksika ya uhusika ya kiima lakini kuna mofimu ya kiima, kwa hivyo haina KUPk lakini kuna UPk ya UPk¹ kupima mofimu ya uhusika **ni-** katika kitenzi ‘niliie’. Kitensi ‘niliie’ kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at), hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya uhusika yambwa na kuacha athari kitensi, husogezwa tena hadi katika HAL ya HAL¹ kupima hali timilifu na kuacha athari kitensi (at), hatimaye kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kupima sifa ya upatanishi kiima ya kitensi hicho na

kubaki hapo. KN ‘*wali ote*’ kinasogezwa pamoja kwani ni kirai nomino, hivyo kitaenda pamoja, kitatoka KN ya T¹ na kuacha athari (ay) kinasogezwa hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.2.1.5 Mofimu –sha

Katika Kiswahili Sanifu mofimu **–sha** huweza kutumika na **–me-** kusisitiza kule kukamilika kwa tendo katika hali timilifu. Kwa hivyo tunaweza kupata sentensi kama wameshalima /wa-mesha-lim-a/. Ikumbukwe kuwa, katika Kiswahili Sanifu huu ni ufupisho ambao unakubalika katika lahaja hii kuwa kutokana na ‘wamekwisha kulima’ tukapata ‘wameshalima’, badala ya kutumia kitenzi kisaidizi kwisha kwa Kiswahili Sanifu huweza kutumia **–me** na **sha-** tukawa na **–mesha-** katika kusisitiza kukamilika kwa tendo fulani. Mifano zaidi ni kama ameshakufa, wameshafika, ameshakwenda.

Kwa upande wa Kitikuu huku kuacha kutumia kwisha na kutumia **–me+sha** pekee hakupatikani. Kwa Kitikuu hatuwezi kusema :

*Vandoshalima, *andoshakufa, *vandoshatedha n.k

Katika Kitikuu hutumika na kitenzi kisaidizi kwisha pamoja na mofimu ya hali timilifu **{-ndo}** kusisitiza kuwa tendo tayari limekamilika.

60a) *Vakulima va - ndo- kw- ish- a ku- lim- a.*
 Nafsi 3 hali kiambishi mzizi kiishio kitenzi mzizi kiishio
 wingi timilifu ku- kisoukomodo

(Wakulima wameshalima)

60b) *Mwalimu ndo - kw - ish- a ku - f - a.*
 Hali kiambishi mzizi kiishio kitenzi mzizi kiishio
 timilifu ku- kisoukomodo

(Mwalimu ameshakufa).

60c) *Vageni va - ndo- kw - ish - a ku - y - a.*
 Nafsi 3 hali kiambishi mzizi kiishio kitenzi mzizi kiishio
 wingi timilifu ku kisoukomodo

(Wageni wameshafika).

60d) *Chu - ndo - kw - ish - a ku - chelew- a.*

| | | | | | | | |
|---------|----------|-----------|-------|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 1 | hali | kiambishi | mzizi | kiishio | kitenzi | mzizi | kiishio |
| wingi | timilifu | ku | | | kisoukomu | | |

(Tumeshachelewa).

Katika ukanushi wa hali timilifu katika lahaja hii hutumia mofimu ya ukanushi {-ya-}, kwa upande wa nafsi, kama katika Kiswahili Sanifu, Kitikuu hutumia mofimu {si} na {ha} kutegemea nafsi husika.

Kiambishi **ku-** hupitia mageuko ya kimofofonolojia na kuwa **kw-** ili kurahisisha matamshi. Shina hapa ni **-isha** yenye maana ya kufikia mwisho, kamilika, maliza, fikia kikomo na kadhalika.


Sheria : /u/ → /w/ / - /i/ /ku-ish-a/ → /kwisha/

Kielelezo cha 60a) kinaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:

60a) *Vakulima va - ndo- kw- ish- a ku- lim- a.*

| | | | | | | | |
|---------|----------|-----------|-------|---------|-----------|-------|---------|
| Nafsi 3 | hali | kiambishi | mzizi | kiishio | kitenzi | mzizi | kiishio |
| wingi | timilifu | ku- | | | kisoukomu | | |

(Wakulima wameshalima)



Nomino ya kiima ‘*vakulima*’, itasogezwa kutoka spesifaya ya kirai tenzi (KT) na kuacha athari (ak) hadi spesifaya ya KUPk kukagua sifa ya uhusika kiima na kinabaki hapo. Kitenzi cha kwanza ‘*vandokwisha*’ kinasogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at) hadi HAL ya HAL¹ na kupima sifa ya hali timilifu, kinasogezwa tena hadi

kifundo cha upatanishi kiima (UPk ya UPk¹) na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*kulima*’ nacho kinasogezwa kutoka kitenzi (T¹) hadi kifundo cha kitenzi kisoukomu (KU) na kupima sifa ya kitenzi hicho na kusogezwa tena hadi upatanishi kiima na kubaki hapo; ijapokuwa hakina mofimu ya kiima lakini kitenzi ‘*kulima*’ ni tendo linaloteklezwa na binadamu na ndio maana husogezwa kwa upatanishi kiima kukagua sifa ya uhusika kiima.


5.2.1.6 Ukanushi wa hali timilifu {ndo}

Katika ukanushi wa hali timilifu **-ndo-** hutumia mofimu **{ya}**, tofauti na Kiswahili Sanifu ambayo hutumia mofimu **{ja}** ya ukanushi wa hali timilifu **{me}**. Mifano ya ukanushi katika ngeli mbalimbali.

61a) Kan. *Amina ha - ya - l- a wali ote.* (Amina hajala wali wote)

Kiambishi ukanushi mzizi kiishio
kanushi hali timilifu

Kielelezo matawi cha ukanushi 61a) kitakuwa:



Katika kielelezo matawi cha 65a) katika ukanushi kinaonyesha kuwa kirai upatanishi kiima kinabeba spesifaya ya uhusika ‘*Amina*’ ambacho kimesogezwa kutoka kwa spesifaya ya kirai tenzi (KT) na kuacha athari (ak). Kitenzi ‘*hayala*’ kinasogezwa kutoka T ya kifundo cha T¹ na kuacha athari (at) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya uhusika yambwa na kuacha athari (ay). Kinasogezwa tena kwa HAL KAN kifundo cha HAL¹ KAN¹ kukagua sifa ya hali ambayo ni katika ukanushi na mwisho kinasogezwa hadi UPk KAN ya UPk¹ KAN¹ na kubaki hapo, kukagua sifa ya uhusika kiima ambacho pia ni katika ukanushi. Kirai nomino ‘*wali ote*’, ambacho pia ni yambwa kinasogezwa kutoka KN ya T¹ na kuacha athari (ay), kinasogezwa tena hadi SPES ya KUPy na kubaki hapo.

61b) *Kiachu ki - ndo - kach - ik - a.* (Kiatu kimekatika.)

Ngeli ya hali mzizi kauli kiishio
upatanishi timilifu tendeka

Kan. *Kiachu ha - ki - ya- kach - ik - a.* (Kiatu hakijakatika.)

Kiambishi ngeli ya ukanushi mzizi kauli kiishio
kanushi upatanishi hali timilifu tendeka

61c) *Maingi a - ndo - vo - a* (Mayai yameoza.)

Ngeli ya hali mzizi kiishio
upatanishi timilifu

Kan. *Maingi ha - ya - ya - vo - a.* (Mayai hayajaoza.)

Kiambishi ngeli ukanushi mzizi kiishio
kanushi ya upatanishi hali timilifu

5.2.1.7 Ukanushi Hali timilifu {-ie}

Katika ukanushi wa hali timilifu ya mofimu {-ie} pia hutumia mofimu {ya} katika ukanushi wake:

62a) *Alii u- l - ie nkache ote.* (Ali amekula mkate wote.)


Nafsi 2 mzizi hali timilifu
umoja

Kan. *Ali ha - ya - l - a nkache ote.* (Ali hajala mkate wote.)

Kiambishi ukunushi mzizi kiishio
kanushi hali timilifu

Kielelezo matawi cha ukunushi katika hali timilifu –**ie** kitakuwa kama kifuatavyo:

Ali ha - ya - l - a nkache ote. (Ali hajala mkate wote.)



Nomino ‘*Alii*’ kitasogezwa kutoka spesifaya ya KT na kuacha athari ya kiima (ak) hadi SPES ya KUPk na kubaki hapo kukagua sifa ya uhusika. Kitenzi ‘*hayala*’ kitasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari ya at, kitasogezwa tena hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at). Kitenzi kitasogezwa tena hadi kifundo cha HAL cha HAL¹ kukagua sifa ya hali timilifu katika ukunushi na hatimaye kifundo cha UPk KAN cha UPk¹ KAN¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima ambacho kipo katika hali ya ukunushi, na kitaishia hapo. Kirai nomino ‘*nkache ote*’ ni yambwa, ambayo inapatikana katika KN cha T¹, kinasogezwa hadi katika SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

62b) *U - to - see changu asubuhi.* (Ametoka tangu asubuhi.)

Nafsi 2 mzizi hali
umaja timilifu

Kan. *Ha-* *ya - tok- a changu asubuhi.* (Hajatoka tangu asubuhi.)

Kiambishi ukanushi mzizi kiishio
kanushi hali timilifu

62c) *Chw - end - ee minadhini ku - tuku - a kuni.*

Nafsi 1 mzizi hali timilifu kitenzi mzizi kiishio
wingi

(Tumeenda minazini (shambani) kuchukua kuni.)

Kan. *Ha - chu- y- endr- a minadhini ku - tuku - a kuni.*

Kiambishi nafsi 1 ukanushi mzizi kiishio mofimu kitenzi mzizi kiishio
kanushi wingi hali timilifu kisoukomo

(Hatujenda minazini kuchukua kuni.)

Katika sentensi ya (iii) hapo juu ‘chu-end-e-e’ kuna uundaji wa kiyeyushi wa pale vokali /u/ inapoungana na vokali nyingine isiyokuwa /u/, huweza kuunda kiyeyushi /w/ ili kurahisisha matamshi.

Sheria: /u/ → /w/ /- /a, ε, i, ɔ/

Vilevile sentensi hiyo hiyo, neno ‘hachuyendra’ lilikuwa ni ‘ha-chu-ya-endra’, kwa sababu ya {ya} ya ukanushi, lakini kwa sababu ya kurahisisha matamshi na mfumo wa silabi pendwa wa KVKV, basi vokali ya kwanza hudondoshwa ili kurahisisha matamshi.

Sheria: /v/ → /ɸ/ /-v/ /a/ → /ɸ/ /- /ε/

/ha-tʃu- ja-ɛndra/ → /hatʃujendra/

5.2.2 Hali Isotimilifu

Hali isotimilifu, kinyume na hali timilifu, huonyesha ile hali kuwa tendo halikukamilika. Hapa kukamilika kwa tendo fulani hakutiliwi maanani. Katika lahaja ya Kitikuu, hali hii hujitokezea kama hali ya mazoea na hali ya kuendelea.

5.2.2.1 Hali ya Mazoea

Comrie (1976:27) anaelezea hali ya mazoea kuwa:

...inaelezea hali ambayo ina sifa ya kuendelea kwa muda mrefu, inaendelea hata ile hali haiangaliwi kama yenye sifa tu ya sasa, bali kama yenye sifa ya kuendelea kwa muda wote. Comrie anatoa mfano kuwa, iwapo mwalimu alikuja darasani na akakohoa siku moja mara kadhaa, hatutaspera hii ni hali ya mazoea, mpaka pale mwalimu anapokuwa darasani huwa anakohoa na hali hii pengine inaendelea kwa mwezi mzima, hapo ndipo tunaweza kusema kwamba, hali hiyo ya mwalimu kukohoakohoa ni ya mazoea.

Beadouin-Lietz (1999-121) naye anaongeza kwa kusema kuwa, hali ya **hu-** katika Kiswahili Sanifu inawakilisha hali ya muda mrefu na ambayo haijihusishi na njeo iliyopita au ijayo. Inaangazia matendo ambayo kwa kawaida yamekuwa yakinendeka, bado yanatendeka na yanaendelea kutendeka. Na kwa sababu ni hali ya mazoea, ndipo mara nyingi hutumika katika methali za Kiswahili, kama wanavyodai kina Ashton (1944) na Maw (1985).

Mifano: Haba na haba **hujaza** kibaba. (*Haba na haba huyadha kibaba*).

Bendera **hufuata** upepo. (*Bendera huandama upepo*).

Hasidi **hana** sababu. (*Hasidi hana sababu*).

Mgaagaa na upwa **hali** wali mkavu. (*Mgaagaa na upwa hali wali nkavu*).

Mti mkuu ukigwa wana wa nyuni **huyumba**. (*Nchi nkuu ukigwa vana va noni huyumba*).

Lindfors (2003:14) anadai kuwa mazoea ni hali inayoelezea matendo yanayotendeka kimazoea au kwa kurudiwarudiwa. Hali hiyo haiangalii tendo katika nyakati maalum, na hivyo basi anamuunga mkono Givon (2001:286) kuwa inakosa ile sifa muhimu ya njeo, kwa hivyo mazoea ni hali na siyo njeo. Kitikuu kinachukua muelekeo huu kuwa hali ya mazoea ni hali na sio njeo.

5.2.2.2 Hali ya Mazoea / kuendelea katika Kitikuu

a) Mofimu {hu-}

Mofimu {hu-} katika Kitikuu hutumika kama hali ya mazoea na hali ya kuendelea, sambamba na ile mofimu {hu-} ya mazoea na {-na-} ya kuendelea katika Kiswahili Sanifu. Kwa mujibu ya kazi hii haitaangazia mofimu {na} ya Kiswahili Sanifu kama njeo, bali kama hali ya kuendelea. Kwa hivyo mofimu {hu} na {na} ya Kiswahili Sanifu ni hali zisotimilifu (Lindfors 2003:34). Kitikuu hakina mofimu {na} na hutumia mofimu {hu} kuwakilisha hali ya mazoea na hali ya kuendelea.

Nurse (1982) anaiita mofimu {hu} ya lahaja ya Kitikuu kama kisawazisho njeo-hali inayosimamia **na na hu** katika Kiswahili Sanifu, yaani husawazisha njeo ya sasa na hali ya mazoea zinatotumika katika Kiswahili Sanifu, na hivyo kumaanisha isiyo ya wakati uliopita wala wakati ujao. Lakini katika Kitikuu tunaangalia hali ya kuendelea na mazoea zote kama hali na sio njeo kama anavyodai Nurse, kuwa ile {na} ya Kiswahili Sanifu ni njeo, ndiyo maana akaiita {hu} ya Kitikuu kisawazisho njeo - hali, kuwa huwakilisha hali ya mazoea na njeo ya sasa.


Hivyo basi mofimu {hu} katika Kitikuu ni ya hali isiyotimilifu na inafanya kazi ya kuwakilisha hali ya mazoea na hali ya kuendelea.

63a) *Vana hu - tedh - a kivandani.*

Hali mazoea mzizi kiishio
na kuendelea

(Watoto wanacheza kiwanjani / watoto hucheza kiwanjani).

Kielelezo matawi 63a)



Kielelezo matawi hapo juu, hata kama hakuna mofimu ya upatanishi kiima katika kitenzi ‘*hutedha*’, katika umbo fonetiki lakini ni dhahiri kuwa katika umbo mantiki mofimu hii ipo. Kwani kulingana na lahaja hii hairuhusu nomino zisizo na uwezo wa kutenda kitendo cha kucheza kutangulia kitendo ‘*hutedha*’, lazima ni kiumbe na ndiyo maana inatanguliwa na kiumbe ‘*vana*’. Nomino ‘*vana*’ husogezwa kutoka SPES ya KT na kuacha athari (ak) hadi SPES ya KUPk na kubaki hapo kukagua sifa ya uhusika kiima. Kitensi ‘*hutedha*’ hukaguliwa kutoka kitensi (T ya T¹) na kuacha athari (at) na kusogezwa hadi HAL ya HAL¹ kukagua hali ya mazoea/kuendelea na kusogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ na kubaki hapo kukagua upatanishi kiima. Kielezi ‘*kivandani*’ hubaki katika kielezi (E ya T¹) kwani hakikaguliwi na kusogezwa kwa sababu hakina sifa za kukaguliwa.

63b) *Noni hu - uk - a iyu kabisa.*

Hali mazoea mzizi kiishio
na kuendelea

(Ndege anaruka juu kabisa / Ndegu huruka juu kabisa.)

63c) *Mwana hu - nw - a madhiva.*

Hali mazoea mzizi kiishio
na kuendelea

(Mtoto anakunywa maziwa / Mtoto hunywa maziwa).

63d) *Amina hu - endr - a → hwendra sokoni kila siku.*

Hali mazoea mzizi kiishio
na kuendelea

(Amina huenda sokoni kila siku / Amina anaenda sokoni kila siku).

Mfano wa (d) hapo juu kuna uyeyushaji ambapo vokali /u/ na na /ɛ/ zinapokutana huunda kiyeyushi /w/ .

/u/ → /w/ / -/ɛ/ /hu-endra/ → /hwendra/

b) Mofimu {- o}


Kitikuu huweza pia kutumia kiishio cha mofimu {-o} katika baadhi ya vitenzi vyake kuonyesha hali ya kuendelea ya sasa kama inavyotumiwa na mofimu {na} katika Kiswahili Sanifu. Vitenzi vinavyoweza kutumia mofimu hii ni viwili pekee: kitenzi cha silabi moja **-y-** na **-endr-**. Vitenzi hivyo katika vitenzi visoukomu ni *ku-y-a* (kuja) na *ku-endra* → *kwendra* (kwenda).

i) Mzizi -y-

64a) *Mwana u - ya - o.* (Mtoto anakuja).

Nafsi 2 mzizi hali ya
umoja kuendelea ya sasa

Kielelezo matawi cha 64a):



Kielelezo matawi cha 64a kinaonyesha kiima ‘mwana’, kinasogezwa kutoka spesifaya ya KT hadi katika SPES ya KUPk kukagua sifa ya uhusika kiima na kubaki hapo. Kitenzi ‘uyao’ kitasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at), hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali ya kuendelea na kuacha athari (at) na kinaishia katika UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi na kubaki hapo.

64b) *Gari li-a-ya-lo* → *le-* *ya - lo.* (Gari linakuja).

Kiambishi mzizi hali ya kuendelea
ngeli upatanishi ya sasa

64c) *Imi /ni-a-ya-o/* → *ne - ya - o.* (Mimi ninakuja).

Nafsi 1 mzizi hali ya kuendelea
umoja ya sasa

ii) **Mzizi -endr-**

65a) *Imi /na-endr-a-o/* → *n - endr - a - o sokoni.* (Mimi ninaenda sokoni).

Nafsi 1 mzizi kiishio hali ya
umoja kuendelea ya sasa

65b) *Amina /a-endr-a-o/* → *endr - a - o kutembea.* (Amina anaenda kutembea).

Mzizi kiishio hali ya
kuendelea ya sasa

Sentensi mbili za kwanza, 65a) na 65b) zina kudondoshwa kwa vokali ya kwanza {a}.

65c) *Isi /chu-endr-a -vo/ → chw – endr – a - vo minadhini.*

Nafsi 1 mzizi kiishio hali ya kuendelea
wingi ya sasa

(Sisi tunaenda minazini / shambani).

Katika sentensi hiyo kuna uundaji wa kiyeyushi -w-, kwani vokali /u/ na /ɛ/ inasababisha uundaji wa kiyeyushi -w-.

Sheria : /u/ → /w/ / /ɛ/

Hapa ikumbukwe kwamba sio kila kitenzi kinaweza kutumika kwa kuishia na vokali -o ya mwisho kuonyesha hali ya sasa ya kuendelea, ni vitenzi viwili tu ambavyo ni vya mzizi wa -y- na endr- kama tulivyoona. Vitenzi vingine vinaweza kuchukua kiambishi – o mwishoni mwa kitenzi lakini kisionyeshe hali hiyo ya sasa ya kuendelea bali kionyeshe urejeshi.

66a) *Mwana a – tedh - a - o kwa hima mbwangu.*

Nafsi 3 mzizi kiishio kirejeshi
umoja

(Mtotoachezaye kwa hima ni wangu).

66b) *Vidhi va - jep - a - o hu – kach - w - a mikono.*

Nafsi 3 mzizi kiishio kirejeshi hali mzizi kauli kiishio
wingi mazoea tendwa

(Wezi waibao hukatwa mikono).

66c) *Michi i - kasi - wa - o nda n'dhee wa nchaa.*

Kiambishi ngeli mzizi kauli kirejeshi
cha upatanishi tendwa

(Miti iliyokatwa ni ya mzee wa mtaa).

5.2.2.3 Ukanushi wa Hali ya Mazoea

Katika ukarusho wa hali ya mazoea na kuendelea {hu-} na mazoea ya kiishio {-o}, mofimu {ha-} hutumiwa mwanzoni na mwisho mofimu {-i} hutumika kuonyesha ukarusho katika Kitikuu, isipokuwa kwa nafsi ya kwanza umoja hutumia {si-}.

67a) *Vana hu - tedh - a kivandani.*

Hali ya mzizi kiishio
mazoea

(Watoto huchenza kiwanjani / Watoto wanacheza kiwanjani).

Kan. *Vana ha - va - tedh - i kivandani.* (Watoto hawachezi kiwanjani).

Kiambishi nafsi 3 mzizi kiishio
kanushi wingi kanushi

67b) *Simba hu - ukauk - a.* (Simba anarukaruka, simba hurukaruka).

Hali ya mzizi-kauli kiishio
mazoea tendatenda

Kan. *Simba ha - ukiuk - i.* (Simba harukiruki.)

kiambishi mzizi-hali kiishio kanushi
kanushi tendatenda kanushi

67c) *Imi hu - kimbi - a kila asubuhi.* (Mimi hukimbia kila asubuhi).

Hali ya mzizi kiishio
mazoea

Kan. *Imi si - kimbi - i kila asubuhi.* (Mimi sikimbii kila asubuhi).

Nafsi 1 mzizi kiishio
kanushi kanushi

67d) *Gari le - ya - lo.* (Gari linakuja).

Kiambishi mzizi hali ya kuendelea
ngeli-upatanishi

Kan. *Gari ha - li - y - i.* (Gari haliji.)

Kiambishi kiambishi mzizi kiishio
kanushi upatanishi kanushi

67e) *Imi ni - endr - ao → nendrao sokoni.* (Mimi ninaenda sokoni).

Nafsi 1 mzizi hali ya
umoja kuendelea

Kan. *Imi si - endr - i → sendri sokoni.* (Mimi siendi sokoni.)


Nafsi 1 umoja mzizi kiishio
kanushi kanushi

Kielelezo matawi cha 67a) kinaweza kuonyeshwa kama kifuatavyo:

67a) *Vana hu - tedh - a kivandani.*

Hali ya mzizi kiishio
mazoea

(Watoto huchenza kiwanjani, watoto wanacheza kiwanjani)



Hapa nomino ‘*kivandani*’ ambayo inafanya kazi kama kielezi kwa kuongezwa mofimu – *ni* hakisogezwi kitabaki hapo kwa kichwa cha kitenzi (T^1) chini ya E (kielezi), kitenzi ‘*hutedha*’ kitasogezwa kutoka T ya T^1 na kuacha athari ya kitenzi (at) hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali, kitasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya kiima na kubaki hapo. Japo kitenzi cha hali hu-tedha, hakibebi mofimu ya kiima, lakini bado ipo kwani kitenzi ‘*hutedha*’ ni tendo la kufanywa na kiumbe na ndio maana lazima tukague sifa ya kiima. Nomino ‘*vana*’ husogezwa kutoka spesifaya ya KT na kuacha athari ya kiima (ak) hadi spesifaya ya KUPk na kubaki hapo kukagua sifa ya kiima.

5.2.2.4 Hali ya Kuendelea {ki}

Mofimu {ki} katika lahaja ya Kitikuu hutumika kuonyesha hali ya kuendelea na pia masharti. Inapotumika kama masharti basi inaonyesha dhamira tegemezi ambayo itaelezewa baadaye.

Mofimu {ki} katika hali ya kuendelea hutokea katika kitenzi kikuu kuonyesha hali, na wakati tendo lilipotendeka huonyeshwa na mofimu za njeo katika kitenzi kisaidizi. Kwa

muktadha huu, hali endezei huwa inaonyeshwa kuwa itakuwa inaendelea katika wakati uliopita ambaa unaonyeshwa na njeo iliyopita au inayoendelea katika wakati ujao kwa kutumia njeo ijayo. Kwa hivyo, hali hii ya kuendelea hutumiwa pamoja na njeo hizo mbili katika Kitikuu, yaani njeo iliyopita au ijayo.

68a) *A - li - ku - v- a a - ki - imb - a usiku kucha.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
umoja iliyopita ku wingi kuendelea

(Alikuwa akiimba usiku kucha).

68b) *Va - li - ku - v- a va - ki - shon - a eo siku ndima.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
wingi iliyopita ku wingi kuendelea

(Walikuwa wakashona leo siku nzima).

68c) *Va - ta - ku - v- a va - ki - som - a wakati wa ntana.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
wingi ijayo ku wingi kuendelea

(Watakuwa wakisoma wakati wa mchana).

68d) *A - ta - ku - v - a a - ki - pik - a chu - ki - endr - a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio nafsi 1 hali ya mzizi kiishio
umoja ijayo ku wingi kuendelea masharti

(Atakuwa akipika sisi tukienda).

Kuna mfanyiko wa kimofonolojia katika sentensi ya 72d) ambapo kitenzi *chukendra*

kuna kudondoshwa kwa vokali /i/ ili kurahisisha matamshi:

/Chu-ki-endra/ → /chukendra/

Sentensi 68a) na 68b) zaonyesha njeo iliyopita {li} katika kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu kimebeba hali ya kuendelea {ki} katika kitenzi kikuu. Sentensi 68c) na 68d) ni za njeo ijayo {ta} katika vitenzi visaidizi na hali ya kuendelea {ki} katika vitenzi vikuu.

Hali hii ya {**ki**} huweza kutumika kuonyesha kuwa kitendo kimeendelea kwa muda kwa kutumia hali timilifu {**ndo**}. Hali timilifu itatumika katika kitenzi kisaidizi na hali ya -**ki**- katika kitenzi kikuu.

68e) *A - ndo - ku - v - a a- ki - tedh- a changu asubuhi.*

Nafsi 3 hali mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
umoja timilifu ku umoja kuendelea

(Amekuwa akicheza tangu asubuhi).

68f) *Chu - ndo - ku - v - a chu - ki - ngoj - a changu meshekuu.*

Nafsi 1 hali mofimu mzizi kiishio nafsi 1 hali ya mzizi kiishio
wingi timilifu ku wingi kuendelea

(Tumekuwa tukingoja tangu alfajiri).

68g) *Valimu va - ndo - ku - v - a va - ki - som - esh - a kwa udhuri.*

Nafsi 3 hali mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kauli ya kiishio
wingi timilifu ku wingi kuendelea tendesha


(Walimu wamekuwa wakisomesha vizuri).

Kielelezo cha 68a) kwa kuzingatia mtazamo wa Uminimalisti kitakuwa:

A - li - ku - v - a a - ki - imb - a usiku kucha.

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
umoja iliyopita ku umoja kuendelea

(Alikuwa akiimba usiku kucha).



Kielelezo matawi hiki kina vitenzi viwili, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu, sentensi ni moja kwa vile ni kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu, ingekuwa ni vitenzi vikuu viwili basi mchoro ungekuwa tofauti. Kitenzi kisaidizi ‘*alikuva*’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo na kuacha athari (at), kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya kiima na kinabaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*akiimba*’ kitasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali, kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya kiima na kubaki hapo. Kielezi ‘*usiku kucha*’ hakisogezwi kwa sababu kulingana na nadharia hii hairuhusu vipashio ambavyo haviwakilishwi kimofolojia kusogezwa ili kukagua sifa.

5.2.2.5 Ukanushi wa mofimu {ki}

Katika ukanushi wa sentensi hizo, utafanywa tu katika vitenzi visaidizi vyenye kubeba njeo na hali timilifu, lakini hali ya kuendelea {ki} inabaki hivyo bila kubadilika.

68a) ***Ha - ku - v - a a - ki - imb - a usiku kucha.***

| | | | | | |
|----------------------|--------------|------------------|------------------|----------------------|------------------|
| Kiambishi kanushi | mofimu ku | mzizi kiishio | nafsi 3 umoja | hali ya kuendelea | mzizi kiishio |
|----------------------|--------------|------------------|------------------|----------------------|------------------|

(Hakuwa akiimba usiku kucha).

68b) ***Ha - va - ku - v - a va - ki - shon - a eo siku ndima.***

| | | | | | | |
|----------------------|------------------|--------------|------------------|------------------|----------------------|------------------|
| Kiambishi kanushi | nafsi 3 wingi | mofimu ku | mzizi kiishio | nafsi 3 wingi | hali ya kuendelea | mzizi kiishio |
|----------------------|------------------|--------------|------------------|------------------|----------------------|------------------|

(Hawakuwa wakishona leo siku nzima).

68c) ***Ha - va - v - i va - ki - som - a wakati wa ntana.***

| | | | | | |
|----------------------|------------------|------------------|--------------------|----------------------|------------------|
| Kiambishi kanushi | nafsi 3 wingi | mzizi kiishio | nafsi 3 kanushi | hali ya kuendelea | mzizi kiishio |
|----------------------|------------------|------------------|--------------------|----------------------|------------------|

(Hawatakuwa wakisoma wakati wa mchana).

68d) ***Ha - v - i a - ki - pik - a chu - ki- endl - a.***

| | | | | | | | | |
|----------------------|------------------|------------------|----------------------|---------------------|------------------|------------------|---------------------|------------------|
| Kiambishi kanushi | mzizi kanushi | kiishio umoja | nafsi 3 kuendelea | hali ya masharti | mzizi kiishio | nafsi 1 wingi | hali ya masharti | mzizi kiishio |
|----------------------|------------------|------------------|----------------------|---------------------|------------------|------------------|---------------------|------------------|

(Hatakuwa akipika tukienda).

Chu-ki-endr- a → chukendra

68e) ***Ha - ya - v - a a - ki - tedh - a changu asubuhi.***

Kiambishi ukanushi hali mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
kanushi ya mazoea umoja kuendelea

(Hajawa akicheza tangu asubuhi).

68f) ***Ha - chu - ya - v - a chu - ki - ngoj - a changu meshekuu.***

Kiambishi nafsi 1 kanushi hali mzizi kiishio nafsi 1 hali ya mzizi kiishio
kanushi umoja mazoea wingi kuendelea

(Hatujakuwa tukingoja tangu alfajiri).

68g) ***Valimu ha - va - ya - v - a va - ki - som- esh - a kwa udhuri.***

Kiambishi nafsi 3 ukanushi mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kauli kiishio
kanushi wingi hali mazoea wingi kuendelea mzizi tendesha

(Walimu hawajawa wakisomesha vizuri).

5.2.2.6 Hali ya Mazoea {ki}

Mofimu {ki} pia huweza kutumika kuonyesha mazoea katika Kitikuu kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu.

69a) ***Mwalimu a - li - ku - v - a a - ki - som - a sana.***

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
umoja iliyopita ku umoja mazoea

(Mwalimu alikuwa akisoma sana.)

69b) ***Vadhadhi va - ta - va - angali - a vana va - ki - tedh - a .***

Nafsi 3 njeo mtendwa mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi ijayo wingi mazoea

(Wazazi watawaangalia watoto wakicheza .)

69c) ***Chu - li - po - kw - endr - a a - li - ku - v - a a - ki - l a.***

Nafsi 1 njeo mofimu mofimu mzizi kiishio nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi iliyopita mahali ku umoja iliyopita ku umoja mazoea

(Tulipokwenda alikuwa akipika.)


chu -li-po-ku-endr-a → chulipokwendra

Kielelezo matawi cha 69a) kinaweza kuonyeshwa kama kifuatavyo:

69a) *Mwalimu a - li - ku - v - a a - ki - som - a sana.*

| | | | | | | |
|------------------|-------------------|----------------------------|------------------|----------------|-------|---------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mofimu ku mzizi kiishio | nafsi 3 umoja | hali mazoea | mzizi | kiishio |
|------------------|-------------------|----------------------------|------------------|----------------|-------|---------|

(*Mwalimu* alikuwa akisoma sana.)



Kielelezo matawi cha 69a) nomino ‘*mwalimu*’ husogezwa kutoka SPES ya KT na kuacha athari (ak) hadi SPES ya KUPk na kubaki hapo. Kitensi kisaidizi ‘*alikuva*’ kutoka T ya T¹ husogezwa hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo iliyopita na kusogezwa tena hadi UPk ya UPK¹ kukagua sifa ya uhusika na kubaki hapo. Kitensi kikuu ‘*akisoma*’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali tena kusogezwa hadi UPk ya UPK¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kielezi ‘*sana*’ hakisogezwi kitabaki kwani hakina sifa za kimofolojia za kusogezwa na kukaguliwa.

5.2.2.7 Ukanushi wa Hali ya Mazoea {Ki}

Katika ukanushi kama ilivyo katika hali ya kuendelea ya {ki}, katika hali ya mazoea ya {ki} pia hukanusha kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu kinaachwa.

69a) *Marehemu ha - ku - v - a a - ki - som - a sana.*

Kiambishi ukanushi mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
kanushi wa njeo li umoja mazoea

(Marehemu hakuwa akisoma sana.)

69b) *Vadhadhi ha - va - va - angali - i vana va - ki - tedh - a.*

Kiambishi nafsi 3 mtendwa mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
kanushi wingi kanushi wingi mazoea

(Wazazi hawatawaangalia watoto wakicheza.)

69c) *Chu- li- po - kw - endr - a ha - ku - v - a a - ki - pik - a.*

Nafsi 1 njeo kiambishi mofimu mzizi kiishio kiambishi ukanushi mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi iliyopita mahali ku kanushi njeo iliyopita umoja mazoea

(Tulipokwenda hakuwa akipika.)

5.2.3 Hali ya Mfululizo

Mofimu {ka} hutumika katika mfululizo wa vitenzi zaidi ya kimoja, ambapo kitenzi chenye {ka} hutanguliwa na kingine kinachowenza kuchukua njeo au hali mbalimbali. Vitenzi nya **ka-** vinaweza vikachukua viishio **-a** au **-e** kwa vitenzi vyenye asili ya kibantu.

70a) *Na - li kw - endr - a sokoni k'a- nunu- a dhiadhi, mboga, machundra, k'a- rud- i.*


Nafsi 1 njeo mofimu mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio
umoja iliyopita ku mfululizo mfululizo

(Nilikwenda sokoni nikanunua viazi, mboga, matunda nikarudi).

Katika sentensi hii Kitikuu hudondosha nafsi ya kwanza umoja ni-, katika vitenzi k'anunua na k'arudi, na {k'a} za mwanzo hutamkwa kwa mpumuo.

Kielelezo matawi cha 70a) ni kama kifuatacho:

Nalikwendra sokoni k'anunua dhiadhi, mboga machundra k'arudi. (Nilikwenda dukani nikanunua mboga, viazi na matunda.)



Katika kielelezo matawi cha 70a), hakina kiima cha kudhahirika bali kuna mofimu katika vitenzi, kwa hivyo hakuna kirai upatanishi kiima (KUPk) bali ni UPk¹ cha kukagua sifa ya upatanishi wa uhusika kiima katika vitenzi. Kitensi ‘nalikwendra’

husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari kitenzi (at₁) hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo iliyopita, baadaye kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kinabaki hapo. Kitensi cha pili cha hali ya mfululizo ‘*k'anunua*’, husogezwa kutoka T ya T¹ cha kitensi cha pili na kuacha athari ya kitensi (at₂), hadi UPy ya UPy¹ kukagua upatanishi wa yambwa, kinasogezwa tena hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali ya mfululizo na kuacha athari, kisha kinasogezwa tena hadi kwa UPk ya UPk¹ ya kitensi cha pili kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kirai nomino chenyeye yambwa tatu, husogezwa kutoka N ya KN na kuacha athari ya yambwa (ay) hadi SPES ya KUPy na kubaki hapo kama nomino tatu; *dhiadhi, mboga na machundra*. Kitensi cha tatu ‘*k'arudi*’ kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari ya kitensi cha tatu (at₃) hadi HAL ya HAL¹ kukagua sifa ya hali ya mfululizo na kuacha athari (at₃), husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Vitenzi viwili *k'anunua* na *k'arudi* japo katika Kitikuu hudondosha mofimu za upatanishi hizo ni katika umbo lake la kifonetiki (UF) tu lakini katika umbo mantiki (US) mofimu hizo zipo, na ndiyo maana wengine wanaitamka na wengi wanaiacha nje katika lajaja hii. Kielezi ‘*sokoni*’ hakisogezwi kinabaki katika E ya T¹ kwa sababu hakina sifa za kukaguliwa.

70b) *Mwalimu a - wedh- a a - ka - va - som - esh - a mpaka usiku.*

| | | | | | | | | |
|------------------|----------------|----------------------|------------------|----------------------|------------------|-------------------|-------------------|---------|
| Nafsi 3 umoja | mzizi umoja | kiishio mfululizo | nafsi 3 umoja | hali ya mfululizo | nafsi 3 umoja | mzizi tendesha | kauli tendesha | kiishio |
|------------------|----------------|----------------------|------------------|----------------------|------------------|-------------------|-------------------|---------|

(Mwalimu anaweza akawasomesha mpaka usiku.)

70c) ‘*Ta- kw- endr- a Mombasa k'a- m- von - e babu angu.*

| | | | | | |
|---------------|--------------|------------------|----------------------|--------------------|----------------------|
| Njeo Ijayo | mofimu ku | mzizi kiishio | hali ya mfululizo | mtendwa dhamira | mzizi kiishio cha |
|---------------|--------------|------------------|----------------------|--------------------|----------------------|

(Nitakwenda Mombasa nikamuone babu yangu.)

Sentensi 70c) viambishi vya kiima (nafsi) vimedondoshwa katika lahaja hii, *t'akwendra, k'amvone* kisha mofimu {ta} na {ka} hutamkwa kwa mpumuo.

Kama ambavyo tumeona vitenzi vinavyobeba mofimu {ka} kuonyesha kufuatana kwa matukio hujitokeza kama kitenzi cha pili na kuendelea.

5.3 Dhamira

Dhamira ni lengo la msemaji/mzungumzaji kuhusu jambo fulani au vile sentensi inavyoolezea. Ni namna tendo au hali ya kitenzi kinavyosawiriwa au kunuiwa.

Hartman (1972:142) anaelezea dhamira kuwa ni ile njia ambayo msemaji anaweza kuwasilisha mtazamo wake katika hali ya mawasiliano.

Naye Bybee (1985:165) anasema,

... dhamira ni kiambishi katika kitenzi kinachoashiria namna msemaji
anavyochagua aina za maneno katika muktadha wa mawasiliano.

Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990) inadai kuwa dhamira ni

Ubainishi wa maumbo ya vitenzi kutegemea lengo la msemaji,
kama vile kuarifu, kuamuru, kusihi, nk.

Kwa hivyo dhamira ni matumizi ya viambishi au mofimu katika vitenzi zinazomruhusu mzungumzaji kuelezea msimamo kuhusu yale anayoyasema. Iwapo anayoyazungumzia ni kwa nia ya kuarifu, kupendekeza jambo, kuamrisha na kadhalika. Wakati mwingine maelezo ya kuonyesha sifa ya dhamira katika sintaksia inaweza kujitokeza katika kirai tenzi chake na sio lazima viambishi katika kitenzi. Lugha nyingi ambishi-bainishi kama vile Kituruki, Kiarabu, lugha za Kibantu, huwa na viambishi au mofimu zinazoambishwa katika kitenzi zinazoonyesha dhamira mbalimbali. Kitikuu kama lahaja ambayo ni ambishi- bainishi hutumia mofimu mbalimbali kudhihirisha dhamira katika

sentensi. Kwa mujibu wa kazi hii vile vile inaangazia zile mofimu zinazoambishwa katika vitenzi zinazodhahirisha dhamira katika Kitikuu.

Kuna aina mbalimbali za dhamira. Kitikuu kina dhamira za aina nne ambazo huwa zinatumika, na ndizo pia zinazotumika katika lugha nyingi.

- i) Dhamira Arifu
- ii) Dhamira Ulizi
- iii) Dhamira Agizi
- iv) Dhamira Tegemezi

5.3.1 Dhamira Arifu

Dhamira arifu ni aina ya dhamira inayozungumzia ukweli dhahiri au ulio wazi, ni maelezo ya kweli. Hapa hakuna fikra ya matamanio, matarajio, kutoa amri au kushuku. Maelezo katika dhamira arifu ni ya kuaminika kwani ni ya ukweli.

Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990), inafasili dhamira arifu kuwa, ‘sifa ya sentensi inayokusudiwa kutoa maelezo ya jambo fulani’.

Dhamira arifu ndiyo aina ya dhamira inayopatikana katika lugha nyingi, na Kitikuu kama Kiswahili Sanifu hutumia dhamira hii kwa kimalizio cha mofimu {-a} katika vitenzi vyenye asili ya Kibantu katika hali yakinishi.

71a) *Mwalimu a - li – androk - a yana ku endr - a → kwendra Udhunguni.*

| | | | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|--------------|----------------|--------------------------|
| Nafsi 3 umoja | njeo iliyopita | mzizi dhamira | kiishio arifu | mofimu ku | mzizi arifu | kiishio dhamira arifu |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|--------------|----------------|--------------------------|

(Mwalimu aliondoka jana kwenda Uzunguni.)

71b) *Mwana hu - l - a wali kwa isi.*

| | | |
|---------------------------------|-------|--------------------------|
| Hali ya kuendelea/ mazoea | mzizi | kiishio dhamira arifu |
|---------------------------------|-------|--------------------------|

(Mtoto anakula wali kwa samaki/mtoto hula wali kwa samaki.)

71c) *Mame ndo - chu - pik - i - a chakula kidhuri eo.*


| | | | | |
|----------|---------|--------|-------|-----------------|
| Hali | nafsi 1 | mzizi | kauli | kiishio dhamira |
| timilifu | wingi | tendea | arifu | |

(Mama ametupikia chakula kizuri leo).

Katika 71(c) mofimu ya kiima {a} hudondoshwa katika Kitikuu kwani kiima chenyewe ‘mame’ kinapatikana kwa hivyo kutumia mofimu ya kiima {a-} ni kama marudio kulingana na Kitikuu, tofauti na sentensi ya kwanza ambapo kiima ‘mwalimu’ ametajwa na mofimu ya kiima {a} inapatikana. Hii ni kwa sababu kwa njeo iliyopita {li} Kitikuu hakidondoshi mofimu ya kiima. Katika Kitikuu vitenzi katika nafsi ya umoja vyta kutumia hali timilifu {ndo} na njeo ijayo {ta} ndiyo Mara nyingi huweza kudondoshwa. Lakini kudondoshwa huku ni katika umbo nje tu lakini umbo ndani mofimu hiyo ipo na ndiyo maana wakati mwingine hudondoshwa na Mara nyingine hutumiwa.

Kielelezo matawi cha sentensi 71a) kulingana na nadharia ni kama kifuatacho:

71a) *Mwalimu a - li - androk - a yana ku - endr - a → kwenda Udhunguni.*



Nomino ‘*mwalimu*’ inasogezwa kutoka spesifaya ya KT na kuacha athari ya kiima (ak) hadi SPES ya KUPk kukagua sifa ya uhusika kiima na kinabaki hapo. Hapa kuna vitenzi viwili; ‘*aliandroka*’, kinasogezwa kutoka T ya T¹ ya kitenzi cha kwanza (1) na kuacha athari (at) hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo iliyopita, baadaye kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kinabaki hapo. Kitensi cha pili ni kitensi kisoukomu, ‘*kwendra*’ kinasogezwa kutoka T ya T¹ ya kitensi cha pili (2) na kuacha athari (at₂), hadi KU ya KU¹ kukagua sifa ya kitensi kisoukomu, kinaacha athari hapo (at₂) na mwisho kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kuna vielezi viwili ambavyo vitabaki katika E ya T¹ kitensi cha kwanza (1) ni ‘*yana*’ na E ya T¹ ya kitensi cha pili (2) ni ‘*udhunguni*’.

5.3.1.2 Ukanushi

Katika ukanushi wa dhamira arifu, njeo iliyopita na hali timilifu hutumia mofimu {a} lakini kwa njeo ijayo na hali ya mazoea/kuendelea hutumia mofimu {i} kama viishio.

71a) *Mwalimu ha - ku - androk - a yana kw - endr - a Udhunguni.*

| | | | | | | |
|-------------------|--------------|-------|---------|--------------|-------|---------------|
| Mofimu kanushi | mofimu ku | mzizi | kiishio | mofimu ku | mzizi | kiishio |
| | | | | | | dhamira arifu |

(Mwalimu hakuondoka jana kwenda Uzunguni).

71b) *Mwana ha - l - i wali kwa isi.* (Mtoto hali wali kwa samaki).

| | | | |
|-------------------|-------|---------|---------|
| Mofimu kanushi | mzizi | kiishio | kanushi |
| | | | |

72c) *Mame ha - ya - chu - pik - i - a chakula kidhuri eo.*

| | | | | | |
|-------------------|---------------------------|------------------|-------|-------|---------------|
| Mofimu kanushi | ukanushi hali timilifu | nafsi 1 wingi | mzizi | kauli | kiishio |
| | | | | | dhamira arifu |

(Mama hajatupikia chakula kizuri leo).

5.3.2 Dhamira Ulizi

Ni aina ya dhamira ambayo huwa ni ya kuuliza maswali na tunatarajia kupata maelezo au tendo fulani kufanyika. Sentensi zenyenye dhamira ulizi lazima ziishie na alama ya kiulizio (?). Mofimu za dhamira ulizi ni sawa na dhamira arifu katika hali yakinishi na hali ulizi, na hii ndiyo sababu mara nyingi dhamira ulizi huwekwa pamoja na dhamira arifu.

72a) *Uwe wa - i - pend - a mwenewe?* (Wewe wajipenda mwenyewe?)

Nafsi 2 jirejea mzizi kiishio
umoja

72b) *Vageni va - ta - ku - y - a kesho?* (Wageni watakuja kesho?)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio
wingi ijayo ku

72c) *Ni nyanyi a - ta - andik - a ubavoni?* (Ni nani ataandika ubaoni?)

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio
umoja ijayo

Katika sentensi mbili za kwanza 72a) na 72b) jibu linahitajika, lakini sentensi ya mwisho (72c) sio lazima kutoa jibu, tendo linaweza kufanya ili kujibu swali hilo, yaani (72c) mwanafunzi anaweza kwenda kuandika ubaoni.

Katika ukanushi mofimu zinazotumika ni kama katika dhamira arifu:

72a) Uwe wa- i - pend - a mwenewe? (Wewe wajipenda mwenyewe?)

Nafsi 2 jirejea mzizi kiishio
umoja

Kan. Uwe hu - i - pend - i mwenewe? (Wewe hujipendi mwenyewe?)

Nafsi jirejea mzizi kiishio
Kanushi

72b) *Vageni va - ta - ku - y - a kesho?* (Wageni watakuja kesho?)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio
wingi ijayo ku

Kan. Vageni ha - va - y - i kesho? (Wageni hawaji kesho?)

mofimu nafsi 3 mzizi kiishio
kanushi wingi

72c) Ni nyanyi a - ta - andik - a ubavoni? (Ni nani ataandika ubavoni?)

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio
umoja ijayo


Kan. Ni nyanyi ha - andik - i ubavoni? (Ni nyanyi haandiki ubavoni?)

Mofimu mzizi kiishio
kanushi kanushi

Kielelezo matawi cha 72a) kitaonyeshwa kama kifuatavyo kulingana na nadharia ya ukaguzi wa sifa:

72a) Uwe wa - i - pend - a mwenewe? (Wewe wajipenda mwenyewe?)

Nafsi 2 jirejea mzizi kiishio
umoja



Katika mchoro huo kulingana na nadharia ya ukaguzi wa sifa, kiima 'uwe' kinasogezwa kutoka SPES ya KT hadi SPES ya KUPk kukagua sifa ya uhusika na kubaki hapo.

Kitenzi 'waipenda' ni kitenzi chenyé mofimu ya kujirejelea {i}, kwa hivyo kitasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari ya kitenzi (at) hadi J ya J¹ kukagua sifa ya kujirejea na kuacha athari ya kitenzi (at). Kinasogezwa tena katika UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi na kinabaki hapo. Kivumishi cha pekee cha aina ya '-

enyewe' urejezi husogezwa kutoka V ya T¹ na kuacha athari hadi SPES ya kirai jirejea , (KJ) na kubaki hapo.

5.3.3 Dhamira Agizi

Aina ya pili ya dhamira ni dhamira agizi ambayo hutoa amri, ombi na hata pendekezo. Hapa huonyesha msemaji katika usemajii wake ataka hatua ichukuliwe na anayezungumziwa kama atatoa kama amri, pendekezo au ombi.

Kamusi Sanifu ya Isimu na Luga inatoa maelezo ya dhamira agizi kuwa:

Ni aina ya tungo yenye kuonyesha amri, ombi, pendekezo, nk.

Kulingana na Wikipedia,

Dhamira agizi ni aina ya dhamira inayotoa amri, ombi na pia makatazo, ruhusa au aina yoyote ya nasaha au ushauri.

Kulingana na fasili ya Wikipedia dhamira agizi inavuka mipaka ya kutoa amri, pendekezo au ombi, bali pia inaangazia mambo ya kutoa makatazo, ruhusa, nasaha, au ushauri katika sentensi.

Dhamira agizi kwa hivyo inaweza kutoa maagizo kwa njia ya amri au ikatoa maagizo kwa njia ya pendekezo au nasaha, ambayo hii ya pili huingiliana na dhamira tegemezi kama tutakavyoona.

Kwa hivyo tunaweza kugawanya dhamira agizi mara mbili:

- a) Dhamira agizi ya amri
- b) Dhamira agizi isiyo ya amri

5.3.3.1 Dhamira agizi ya amri

Dhamira agizi ya amri katika Kitikuu kama ilivyo katika lugha nyingi hulenga nafsi ya pili katika umoja na wingi (wewe na nyinyi).

Katika Kitikuu mofimu ya dhamira agizi inayoonyesha amri kwa vitenzi vyenye asili ya Kibantu ni mofimu tamati {-a} kwa hali yakinishi, na mofimu {si-} na {-e} kwa ukarusha. Katika wingi hali yakinishi hutumia mofimu {-ani} na ukarusha hutumia mofimu {si} mwanzoni na {-e} mwishoni. Ikumbukwe kwamba katika aina hii ya dhamira agizi mofimu ya kiima katika hali yakinishi hudondoshwa na kwa umoja tunabaki na shina tu la kitenzi (pika, imba), kwa wingi huongezwa -ni kwa shina hili la kitenzi **pikani**, **imbani** nk.

Katika ukarusha mofimu za kiima huwekwa (**usipike**, **usiimbe**, **musipike**, **musiimbe**).

Kwa vitenzi vyenye asili ya kigeni huweza kuishia na vokali isiyokuwa -a, kama vile **fikiri**, **jaribu**, **sahau**, **dhulumu**, **ajiri**, **tubu** na kadhalika na huachwa hivyo hivyo kwa umoja lakini kwa wingi huongezea mofimu {-ni} mwishoni: **fikirini**, **jaribuni**, **dhulumuni**, **ajirini**.

Vilevile sentensi za dhamira agizi za amri humalizia na alama ya mshtuo (!) lakini kwa dhamira agizi zisizoonyesha amri sio lazima ziishie na alama ya mshtuo.

Umoja

73a) *Simam - a!*

Mzizi kiishio dhamira
 agizi

Wingi

Simam- ani! (Simameni!)

mzizi kiishio dhamira
 agizi wingi

73b) *Imb - a!*

Mzizi kiishio dhamira
 agizi

Imb - ani! (Imbeni!)

mzizi kiishio dhamira
 agizi wingi

73c) *Kimbi - a!*

Mzizi kiishio dhamira
 agizi


Kimbi - ani! (Kimbieni!)

mzizi kiishio dhamira
 agizi wingi

Ikumbukwe hapa kuwa katika Kitikuu tofauti na Kiswahili Sanifu mofimu ya wingi kuonyesha dhamira agizi amrishi ni {-ani} lakini kwa Kiswahili Sanifu ni {-eni} kwa vitenzi vyenye asili ya Kibantu, kama mifano hapo juu inavyoonyesha.

Kielelezo matawi cha dhamira agizi ni kama kifuatacho:

73a) Simama



Sentensi 73a) ‘Simama’ kimesogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua dhamira agizi ya amri au amrishi na kinaishia hapo.

Kwa vitenzi nya silabi moja, Kitikuu huonyesha dhamira agizi ya amri kiambishi **ku-** cha kitenzi kisoukomu hakitumiki, kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu, Kitikuu hutumia mofimu {i} mwanzoni kuonyesha ile hali ya kuamrisha.

Umoja

Wingi

74a) **I - l - a!** (Kula!) **I - l - ani!** (Kuleni!)

| | | | | | |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|
| mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi umoja | mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi wingi |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|

74b) **I- nw - a!** (Kunywa!) **I - nw - ani!** (Kunywani!)

| | | | | | |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|
| mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi umoja | mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi wingi |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|

74c) **I - f - a!** (Kufa !) **I - f - ani!** (Kufeni!)

| | | | | | |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|
| mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi umoja | mofimu amrishi | mzizi | kiishio dhamira agizi wingi |
|-------------------|-------|--------------------------------|-------------------|-------|--------------------------------|

Ukanushi wa dhamira agizi ya amri hutumia mofimu kanushi {si} na kiishio {e} katika umoja na wingi:


Umoja**Wingi**

| | | |
|----|---|---|
| a) | <i>U - si - simam - e</i> | <i>Mu - si - simam - e!</i> |
| | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira umoja kanushi agizi kanushi | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira wingi kanushi agizi |
| b) | <i>U - si - imb - e!</i> | <i>Mu - si - imb - e!</i> |
| | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira umoja kanushi agizi kanushi | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira wingi kanushi agizi |
| c) | <i>U - si - kimbi - e!</i> | <i>Mu - si - kimbi - e!</i> |
| | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira umoja kanushi agizi kanushi | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira wingi kanushi agizi |
| d) | <i>U - si - l - e!</i> | <i>Mu - si - l - e!</i> |
| | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira umoja kanushi agizi kanushi | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira wingi kanushi agizi |

Ikumbukwe kwamba dhamira agizi ya amri huwa ni ya nafsi ya pili umoja na wingi pekee, lakini kwa dhamira agizi isiyo ya amri inaweza kujitokeza kwa nafsi zote.

Kielelezo matawi cha ukarusha cha dhamira agizi ya amri kitaonyeshwa kama kifuatavyo:

| | |
|----|---|
| a) | <i>U - si - simam - e!</i> |
| | nafsi 2 mofimu mzizi kiishio dhamira umoja kanushi agizi kanushi |



Katika ukarusha kitenzi cha dhamira agizi ya amri ‘*usisimame*’ kielelezo matawi chake kitakuwa tofauti na kile cha hali yakinishi. Kitenzi ‘*usisimame*’ kitasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari ya kitenzi (at) hadi kwa dhamira (DHAM) kukagua sifa ya dhamira agizi na kuacha athari, kitasogezwa tena hadi kichwa cha KAN ya KAN¹ kukagua sifa ya ukarusha na kuacha athari; hatimaye husogezwa katika kichwa cha UPk kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo.

5.3.3.2 Dhamira Agizi isiyo ya Amri

Dhamira agizi isiyo ya amri ni ya kuonyesha upole, ombi au pendekezo katika sentensi, ambayo pia hujitokeza kama dhamira tegemezi. Dhamira ya aina hii huhusisha kuomba na hivyo, neno tafadhali, huweza kutumika katika sentensi. Tafadhali, ni neno lenye asili ya Kiarabu, nacho Kitikuu pia hutumia neno hilo. Hutumika zaidi, kwa nafsi ya pili umoja na wingi. Hapa kiambishi cha nafsi ya pili katika umoja ni {u-} na wingi {mu}.

75a) *U - pik - e chakula vana va - l - e.* (Upike chakula watoto wale).

| | | | | | |
|------------------|-------|-------------------------|------------------|-------|------------------|
| Nafsi 2 umoja | mzizi | mofimu dhamira agizi | nafsi 3 wingi | mzizi | dhamira agizi |
|------------------|-------|-------------------------|------------------|-------|------------------|

Mu - pik - e chakula vana va - l - e. (Mpike chakula watoto wale.)

| | | | | | |
|------------------|-------|-------------------------|------------------|-------|------------------|
| Nafsi 2 wingi | mzizi | mofimu dhamira agizi | nafsi 3 wingi | mzizi | dhamira agizi |
|------------------|-------|-------------------------|------------------|-------|------------------|

75b) *U - som - e dhitaru dhote eo.* (Usome vitabu vyote leo.)

| | | |
|------------------|-------|-------------------------|
| Nafsi 2 umoja | mzizi | mofimu dhamira agizi |
|------------------|-------|-------------------------|

Mu - som - e dhitaru dhote eo. (Msome vitabu vyote leo.)

| | | |
|------------------|-------|-------------------------|
| Nafsi 2 wingi | mzizi | mofimu dhamira agizi |
|------------------|-------|-------------------------|

75c) *Tafadhali i - nw- a dawa u - si - sahau.*

| | | | | | |
|-------------------|-------|---------|------------------|-------------------|-------|
| Mofimu nafsi 2 | mzizi | kiishio | nafsi 2 umoja | mofimu kanushi | mzizi |
|-------------------|-------|---------|------------------|-------------------|-------|

(Tafadhali kunywa dawa usisahau.)

Tafadhali i - nw - ani dawa mu - si - sahau.

| | | | | | |
|-------------------|------------------------|------------------|---------|-------------------|-------|
| Mofimu nafsi 2 | mzizi dhamira agizi | kiishio wingi | nafsi 2 | mofimu kanushi | mzizi |
|-------------------|------------------------|------------------|---------|-------------------|-------|


(Tafadhali kunyweni dawa msisahau.)

Katika Kitikuu, kwa dhamira agizi isiyo ya amri vitenzi vyake katika umoja na wingi huchukua mofimu {e} mwishoni badala ya {a} lakini inapotumiwa na neno, tafadhali, katika nafsi ya pili, basi inaweza kuishia na vokali ya {a} (Taz.75c).

Kielelezo matawi cha 75a) kinaweza kuainishwa kama:

75a) *U - pik - e chakula vana va- l - e.* (Upike chakula watoto wale).

| | | | | | |
|------------------|------------------------|-----------------|------------------|----------------|-------|
| Nafsi 2 umoja | mzizi dhamira agizi | mofimu agizi | nafsi 3 wingi | mzizi agizi | dhama |
|------------------|------------------------|-----------------|------------------|----------------|-------|



Katika sentensi ‘*Upike chakula vana vale*’, ni kama sentensi mbili katika sentensi moja, kwani ina vitenzi vikuu viwili vya dhamira agizi; *upike* na *vale*, kwa hivyo katika kuonyesha katika kielelezo matawi itaonyeshwa kama sentensi mbili lakini ziko kwa moja. Mchoro utakuwa mmoja wenyewe vichwa vya vitenzi viwili. Sentensi inaanza kwa kitenzi cha kwanza ‘*upike*’ kinachokaguliwa sehemu mbalimbali, kwanza kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi UPy ya UPy¹ kupima sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (ay), tena kinasogezwa hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira agizi, kisha kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kuishia hapo. Yambwa ‘*chakula*’ kinasogezwa kutoka N ya T¹ na kuacha athari (ay) hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo. Sentensi ya pili kitenzi ‘*vale*’ husogezwa kutoka T ya T¹ hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira agizi, kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kiima ‘*vana*’ husogezwa kutoka SPES ya KT na kuacha athari (ak) hadi SPES ya KUPk kukagua sifa ya uhusika kiima na kubaki hapo.

5.3.3.3 Ukanushi

Katika ukanushi wa dhamira agizi isiyo ya amri, kama ilivyo katika dhamira agizi ya amri hutumia mofimu kanushi {si} baada ya nafsi na kiishio {e}

75a) *U - si - pik - e chakula vana va - si- l - e.*

| | | | | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|------------------|-------------------|------------------|------------------|
| Nafsi 2 umoja | mofimu kanushi | mzizi dhamira | kiishio agizi | nafsi 3 wingi | mofimu kanushi | mzizi dhamira | dhamira agizi |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|------------------|-------------------|------------------|------------------|

(Usipike chakula watoto wasile).

Mu - si - pik - e chakula vana va- si- l - e.

| | | | | | | | |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|------------------|-------------------|------------------|------------------|
| Nafsi 2 wingi | mofimu kanushi | mzizi dhamira | kiishio agizi | nafsi 3 wingi | mofimu kanushi | mzizi dhamira | dhamira agizi |
|------------------|-------------------|------------------|------------------|------------------|-------------------|------------------|------------------|

(Msipike chakula watoto wasile).

75b) *U - si - som - e dhitabu dhote eo.* (Usisome vitabu vyote leo.)

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio
umoja kanushi dhamira agizi

Mu - si - som - e dhitabu dhote eo. (Msisome vitabu vyote leo.)

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio
wingi kanushi dhamira agizi

75c) *Tafadhali u - si nw - e dawa u - si - sahau.*

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio nafsi 2 mofimu mzizi
umoja kanushi dhamira agizi umoja kanushi

(Tafadhali usinywe dawa usisahau.)

Tafadhali mu - si- nw - e dawa mu - si - sahau.

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio nafsi 2 mofimu mzizi
wingi kanushi dhamira agizi wingi kanushi

(Tafadhali msinywe dawa msisahau.)

Sentensi 75a) na 75c) katika ukarusha zina vitenzi viwili, ambapo wakati mwingine tukikanusha vitenzi vyote viwili maana hupotea. Kwa sentensi 75a), *Usipike chakula vana vasile* inawezekana, kwa mfano mama anapomwambia mpishi, usipike chakula watoto wasile, pengine watoto wamefanya makosa fulani, basi kwa kuwaadhibu leo kusipikwe chakula ndio wasipate kula. Vilevile kwa sentensi 75c) mtoto alikuwa akitumia dawa fulani, labda muda wake umeisha au haikufanya kazi kama ilivyotarajiwa, sasa mama anamkumbusha kuwa, ‘tafadhalii usinywe dawa, usisahau.

5.3.4 Dhamira tegemezi

Ni aina ya dhamira inayoonyesha matumainio, hali ya kufikirika, matarajio ambayo mara nyingi hayapatikani.

Kulingana na Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (1990) inafasili dhamira tegemezi kuwa:

Dhamira ambayo kwa kawaida huonyesha matumainio ambayo aghalabu hayapatikani.

Dhamira tegemezi huwa ni kinyume cha dhamira elezi, kwani dhamira elezi hutoa maelezo ya kweli na kuaminika lakini dhamira tegemezi hutoa maelezo yasioaminika au yakutarajiwa tu na sio ya uhakika.

Dhamira tegemezi inamruhusu mzungumzaji kutunga sentensi zinazoonyesha matarajio, maombi, mapendekezo, amri, malengo, masharti na makisio ambayo ni kinyume na uhakika wa mambo wakati wa usemi.

Dhamira tegemezi huweza kutumika kutekeleza hayo mambo mbalimbali kama ambavyo yametajwa hapo juu. Matumizi yake ni kama yafuatayo:

5.3.4.1 Hutumika kama dhamira agizi isiyo ya amri.

Hapa ni kama matumizi ya dhamira agizi isiyo ya amri, kama nilivytangulia kusema kuwa dhamira agizi isiyo ya amri hutumika pia kama dhamira tegemezi. Hii hutokea kwa nafsi ya pili umoja na wingi katika lahaja hii.

76a) *U - l - e wali ote ni - lo - ku - chi- li - a.*
 Nafsi 2 mzizi dhamira agizi/
 umoja tegemezi nafsi 1 kirejeshi yambwa mzizi kauli kiishio
 tendea

(Ule wali wote niliokutilia.)

Mu - l - e wali ote ni - lo - va - chi - li - a.
 Nafsi 2 mzizi dhamira agizi/
 wingi tegemezi nafsi 1 kirejeshi yambwa mzizi kauli kiishio
 tendea

(Mle wali wote niliowatilia.)

76b) *U - imb - e wimbo wa taifa kesho. (Uimbe wimbo wa taifa kesho).*

Nafsi 2 mzizi dhamira agizi/
 umoja tegemezi

Mu - imb - e wimbo wa taifa kesho. (Muimbe wimbo wa taifa kesho).

Nafsi 2 mzizi dhamira agizi/
 wingi tegemezi

76c) *Tafadhali m - pek - e mwanao kwa dakitari.*

Njeo 1 mzizi dhamira agizi/
umoja tegemezi

(Tafadhali mpeleke mtoto wako kwa daktari.)

Tafadhali va - pek - e vana venyu kwa dakitari.

Njeo 2 mzizi dhamira agizi/
wingi tegemezi



(Tafadhali wapeleke watoto wenu kwa daktari.)

Kielelezo matawi cha 76a) kitakuwa kama kifuatacho:

76a) *U - l - e wali ote ni - lo - ku - chi- li - a.*

Nafsi 2 mzizi dhamira agizi/
umoja tegemezi nafsi 1 kirejeshi yambwa mzizi kauli kiishio
 umoja mtenda tendea

(Ule wali wote niliokutilia).



Sentensi hii ina vitenzi viwili vikuu, kwa hivyo tunaweza kuiangalia kama sentensi moja yenye virai tenzi viwili katika kielelezo matawi. Kirai tenzi cha kwanza huonyesha kitenzi ‘ule’ kikihamishwa kutoka kirai tenzi cha T¹ na kuacha athari (at) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa, kinahamishwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kisha kinahamishwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kirai nomino ‘wali ote’ kinahamishwa kutoka KN ya KT na kuacha athari (ay) hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo. Kirai tenzi cha pili, ‘nilokuchilia’ kinahamishwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi kichwa cha kauli ya kutenda (IA ya IA¹) na kuacha athari ya kitenzi, kinahamishwa tena hadi RE ya RE¹ kukagua sifa ya mofimu ya mtenda ya urejelezi na kuacha athari, kinahamishwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukugua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo.

5.3.4.2 Ukanushi

Hapa kama dhamira agizi isiyo ya amri hutumia mofimu ya ukashu {si} baada ya nafsi na kiishio {e}:

| | | | | | | | | | | | | |
|------|------------------|-------------------|-------------------|----------------------------|-------------|------------|------------------|---------------------|-----------------|----------------|-------------------|-----------|
| 76a) | <i>U-</i> | <i>si -</i> | <i>l -</i> | <i>e</i> | <i>wali</i> | <i>ote</i> | <i>ni -</i> | <i>lo-</i> | <i>ku -</i> | <i>chi -</i> | <i>li -</i> | <i>a.</i> |
| | Nafsi 2 umoja | mofimu kanushi | mzizi tegemezi | dhamira agizi/ tegemezi | | | nafsi 1 umoja | kirejeshi mtenda | mtenda mzizi | kauli kauli | kiishio tendea | |

(Usile wali wote niliokutilia.)

| | | | | | | | | | | | |
|------------------|-------------------|-------------------|----------------------------|------|-----|------------------|---------------------|-----------------|----------------|-------------------|----|
| Mu - | si - | l - | e | wali | ote | ni - | lo - | va - | chi - | li - | a. |
| Nafsi 2 wingi | mofimu kanushi | mzizi tegemezi | dhamira agizi/ tegemezi | | | nafsi 1 umoja | kirejeshi mtenda | mtenda mzizi | kauli kauli | kiishio tendea | |

(Msile wali wote niliowatilia.)

| | | | | | |
|------|------------------|-------------------|-------------------|----------------------------|------------------------------|
| 76b) | <i>U -</i> | <i>si -</i> | <i>imb -</i> | <i>e</i> | <i>wimbo wa taifa kesho.</i> |
| | Nafsi 2 umoja | mofimu kanushi | mzizi temezezi | dhamira agizi/ tegemezi | |

(Usiimbe wimbo wa taifa kesho.)

Mu - si - imb - e wimbo wa taifa kesho.

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira agizi/
umoja kanushi temezezi

(Msiimbe wimbo wa taifa kesho.)

5.3.4.3 Mapendekezo, matamanio, matakwa (ombi)

Hutumika kwa nafsi zote tatu.

77a) *A - dhungumudh - e Kiswahili ni - sik- i- e.*

Nafsi 3 mzizi dhamira nafsi 1 mzizi kauli dhamira
umoja tegemezi tendea tegemezi

(Azungumze Kiswahili nisikie.)

Va - dhungumudh - e Kiswahili chu - sik - i - e.

Nafsi 3 mzizi dhamira nafsi 1 mzizi kauli dhamira
wingi tegemezi tendea tegemezi

(Wazungumze Kiswahili tusikie.)

77b) *Mambo haa na - ya - ish- e → nayashe hapa hapa.*

Ngeli mzizi kauli dhamira
upatanishi tendesha tegemezi

(Mambo haya nayaish hapa hapa.)

77c) *Tafadhali m - pek- e mwanao kwa dakitari.*

Nafsi 2 mzizi dhamira
umoja tegemezi

(Tafadhali mpeleke mtoto wako kwa daktari.)

Tafadhali va - pek - eni vana venyu kwa dakitari.

Nafsi 2 mzizi dhamira
wingi tegemezi wingi


(Tafadhali wapelekeni watoto wenu kwa dakitari.)

Katika mfano 77b) neno ‘nayaish’ katika Kitikuu mzizi ni {ya} lakini kwa sababu ya mfuatano wa vokali ya chini {a} na ya juu {i} kuna mvutano wa vokali hizo, na hatimaye uundaji wa vokali ya kati {ε}, kwa hivyo mageuko ya kimofofonolojia yanatokea. Katika Kiswahili Sanifu japo kuna mfuatano huo wa vokali hakuna mageuko yanayotokea neno linabaki /nayaish/.

/na-ya-ish-e/ → / nayeshe/

Kielelezo matawi cha 77a ni kama kifuatacho:

77a) A - dhungumudh - e Kiswahili ni - sik- i- e.
 Nafsi 3 mzizi dhamira nafsi 1 mzizi kauli dhamira
 umoja tegemezi tendea tegemezi
 (Azungumze Kiswahili nisikie.)



Kielelezo cha hapo juu kinaonyesha kina vitenzi vikuviwili kwa hivyo huonyeshwa kwa virai tenzi viwili. Kwanza kirai tenzi cha kwanza ‘adhungumudhe’ huonyeshwa kitenzi husogezwa kutoka T ya T¹ hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa katika kitenzi na kuacha athari (at₁), husogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira na kuacha athari (at₁), na hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya uhusika na kubaki hapo. Nomino ya yambwa ‘Kiswahili’ husogezwa kutoka N ya T¹ na kuacha athari yambwa (ay) hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya

uhusika yambwa na kubaki hapo. Kitensi cha pili ‘nisikie’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at₂), hadi DHAM ya DHAM¹ na kuacha athari (at₂), kukagua sifa ya dhamira, husogezwa tena hadi IA ya IA¹ kukagua sifa ya kauli ya kutendea, hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitensi na kubaki hapo.

5.3.4.4 Ukanushi

77a) A - dhungumudh - e Kiswahili ni - si- sik - i- e.

| | | | | | | | |
|------------------|----------|-------|------------------|--------|--------|----------|---------|
| Ngeli 1 umoja | mzizi | dhama | nafsi 1 umoja | mofimu | mzizi | kauli | dhamira |
| | tegemezi | | kanushi | | tendea | tegemezi | |

(Azungumze Kiswahili nisisikie.)

Va - dhungumudh - e Kiswahili chu - si - sik - i - e.

| | | | | | | | |
|------------------|----------|-------|------------------|--------|--------|----------|---------|
| Ngeli 2 wingi | mzizi | dhama | nafsi 1 wingi | mofimu | mzizi | kauli | dhamira |
| | tegemezi | | kanushi | | tendea | tegemezi | |

(Wazungumze Kiswahili tuisikie.)

77b) Mambo haa na - ya - si - ish - e → nayasiishe hapa hapa.

| | | | | |
|----------------------|-------|-------------------|----------|---------|
| Mofimu upatanishi | mzizi | mofimu kanushi | kauli | dhamira |
| | | tendesa | tegemezi | |

(Mambo haya nayasiishe hapa hapa.)

77c) Tafadhali u- si - m - pek - e mwanao kwa daktari.

| | | | | |
|------------------|---------|---------|----------|---------|
| nafsi 2 umoja | mofimu | mtendwa | mzizi | dhamira |
| | kanushi | | tegemezi | |

(Tafadhali usimpeleke mtoto wako kwa daktari.)

Tafadhali mu - si - va - pek - e vana venyu kwa daktari.

| | | | | |
|------------------|-------------------|----------|----------|---------|
| nafsi 2 wingi | mofimu kanushi | watendwa | mzizi | dhamira |
| | | | tegemezi | |

(Tafadhali musiwaapeleke watoto wenu kwa daktari.)

Mfano 77b) ya ukunushi kuna kudondoshwa kwa vokali ya kwanza kwani kuna vokali mbili zinazofanana zimefuatana /yasiishe/. Katika Kitikuu vokali ya kwanza /i/ hudondoshwa kurahisisha matamshi:

/na- ya-si-ish-e/ → / na-ya- s- ish- e/.

Tofauti na Kiswahili Sanifu vokali /i/ haidondoshwi na hubaki nayasiishe.

5.3.4.5 Amri isiyo dhahiri, isiyo ya moja kwa moja.

78a) *Ndoo u- l - e nami.* (Njoo ule na mimi.)

mzizi nafsi 2 mzizi dhamira
umoja tegemezi

Ndoo - ni mu - l - e nasi. (Njooni mle na sisi.)

Mzizi mofimu nafsi 2 mzizi dhamira
wingi wingi tegemezi

78b) *Pok - e - a kitabu chako u - som - e.*

Mzizi kauli kiishio nafsi 2 mzizi dhamira
tendea dhamira arifu umoja tegemezi

Pok - e - ani dhitabu dhenyu mu - som - e.

Mzizi kauli kiishio cha nafsi 2 mzizi dhamira
tendea wingi wingi tegemezi

(Pokeeni vitabu vyenu musome)

78c) *Sikidh - a kisha u - jib - u maswali.* (Sikiliza kisha ujibu maswali.)

Mzizi kiishio nafsi 2 mzizi dhamira
dhamira arifu umoja tegemezi


Sikidh - ani kisha mu- jib - u maswali. (Sikilizeni kisha mjibu maswali).

Mzizi mofimu wingi nafsi 2 mzizi dhamira
dhamira arifu wingi tegemezi

Kielelezo matawi cha 78a) kinaweza kuainishwa kama kifuatavyo:

78a) *Ndoo u- l - e nami.* (Njoo ule na mimi.)

mzizi nafsi 2 mzizi dhamira
umoja tegemezi



Kielelezo matawi hiki kina vitenzi vikuu viwili; ‘*ndoo na ule*’. Kitenzi ‘*ndoo*’ japo hakina mofimu ya upatanishi kiima lakini katika Kiswahili na lahaja ya Kitikuu kinamaanisha anaambiwa mtu wa nafsi ya pili umoja (wewe), kwa hivyo kichwa cha UPk kimewekwa kwa ajili ya kukagua sifa hiyo ya kiima. Kitenzi ‘*ndoo*’, kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi cha pili ‘*ule*’ kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa katika kitenzi hicho na kuacha athari (at), kinasogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira na kuacha athari (at), hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi hicho na kubaki hapo. Nomino ‘*nami*’ husogezwa kutoka N ya T¹ na kuacha athari (ay) hadi spesifaya ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.3.4.6 Ukanushi

78a) *U - si - y - e ku - l - a nami.* (Usije kula na mimi.)

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira mofimu mzizi kiishio
umoja kanushi tegemezi ku dhamira arifu

Mu - si - y - e ku - l - a . (Msije kula na sisi.)

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira mofimu mzizi kiishio
wingi kanushi tegemezi ku dhamira arifu

78b) *U - si - poke - e kitabu chako ku - som - a.*

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira mofimu mzizi kiishio
umoja kanushi tegemezi ku dhamira arifu

Mu - si - poke - e dhitabu dhenyu ku - som - a.

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira mofimu mzizi kiishio
wingi kanushi tegemezi ku dhamira arifu

(Msipokee vitabu vyenu kusoma.)

78c) *U - si - sikidh - e kisha u - si - jib - u maswali.*

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira nafsi 2 mofimu mzizi kiishio
umoja kanushi tegemezi umoja kanushi dhamira arifu

(Usisikilize kisha usijibu maswali.)

Mu - si - sikidh - e kisha mu - si - jib - u maswali.

Nafsi 2 mofimu mzizi dhamira nafsi 2 mofimu mzizi kiishio
wingi kanushi tegemezi wingi kanushi dhamira arifu

(Msisikilize kisha mjibu maswali.)

5.3.4.7 Enye kutumia semi zenye maneno kama: **lazima, heri, sharti, yabidi, afadhali, bora, yafaa na yapasa**

Dhamira tegemezi huweza pia kutumika kwa kutumia semi kama hizi katika sentensi.

79a) *Ladhima u - endr - e → wendre sipichali kesho.*

Nafsi 2 mzizi kiishio
umoja cha dhamira

(Lazima uende hospitali kesho.)

Ladhima mu - endr - e → wendre sipichali kesho.

Nafsi 2 mzizi kiishio
wingi cha dhamira

(Lazima mwende hospitali kesho.)

- 79b) *Heri u - endr - e* → *wendre kadhini.* (Heri uende kazini.)
 Nafsi 2 mzizi kiishio cha
 umoja dhamira
- Heri mu - endr - e* → *mwendre kadhini.* (Heri mwende kazini.)
 Nafsi 2 mzizi kiishio cha
 wingi dhamira
- 79c) *Bora u - nyuk - e meshekuu.* (Bora uamke alfajiri.)
 Nafsi 2 mzizi kiishio
 umoja cha dhamira
- Bora mu - nyuk - e meshekuu.* (Bora muamke alfajiri.)
 Nafsi 2 mzizi kiishio
 wingi cha dhamira

Katika mifano hiyo hapo juu 79a) na 79b) kuna mifanyiko ya kimofofonolojia ya uundaji wa kiyeyushi /w/ kutoka kwa vokali /u/.


/u/ → /w/ / /ε/ /mu-endre/ → /mwendre/

Kielelezo matawi cha 79a) kinaoyeshwa kama kifuatavyo:

- 79a) *Ladhima u - endr - e* → *wendre sipichali kesho.*

Nafsi 2 mzizi kiishio
 umoja cha dhamira

(Lazima uende hospitali kesho.)



Katika kielelezo matawi hiki neno ‘*ladhima*’ mwanzo wa sentensi hufanya kazi ya fokasi kwa hivyo kimewekwa kwenye kichwa cha fokasi na kukaguliwa na kubaki hapo ili kuwe na mpangilio sahihi wa maneno. Kitenzi ‘*wendre*’ kutoka kichwa cha T cha T¹ husogezwa hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishwa yambwa na kuacha athari, husogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua dhamira tegemezi na kuacha athari kitensi (at), mwisho kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima kwenye kitensi na kubaki hapo. Nomino ya yambwa ‘*sipichali*’ kutoka N ya KN husogezwa hadi SPES ya KUPy na kubaki hapo. Kivumishi ‘*kesho*’ hakisogezwi kutoka V ya KN, kinabaki hapo kwa sababu hakina sifa za kimofolojia za kusogezwa.

5.3.4.8 Ukanushi

80a) *Si ladhima u - endr - e → wendre sipichali kesho.*

| | | |
|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mzizi | kiishio cha |
| umoja | | dhamira |

(Sio lazima wende hospitali kesho.)

Si ladhima mu - endr - e → mwendre sipichali kesho.

| | | |
|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mzizi | kiishio cha |
| wingi | | dhamira |

(Sio lazima mwende hospitali kesho).

80b) *Heri u - si - endr - e → usendre kadhini.* (Heri usiende kazini.)

| | | | |
|---------|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio cha |
| umoja | kanushi | | dhamira |

Heri mu - si - endr - e → musendre kadhini. (Heri musiende kazini.)

| | | | |
|---------|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio cha |
| wingi | kanushi | | dhamira |

80c) *Bora u - si - nyuk - e meshekuu.* (Bora usiamke alfajiri.)

| | | | |
|---------|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio cha |
| umoja | kanushi | | dhamira |

Bora mu - si - nyuk - e meshekuu. (Bora musiamke alfajiri.)

| | | | |
|---------|---------|-------|-------------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio cha |
| wingi | kanushi | | dhamira |

Katika sentensi ya 80b), kuna mfanyiko wa kimofofonolojia katika Kitikuu ambapo mofimu **{si}** ya ukarusha inapakanana na vokali ya kitenzi **{e}** kwa hivyo kuna kudondoshwa kwa vokali ya kwanza **{i}** ili kurahisisha matamshi, badala ya kusema usiendre, inakuwa usendre, pia musendre badala ya musiendre. Tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo inabaki usiende na msiente mtawalia.

/v/ → /ɸ/ / - /v/

/u-si-endr-e/ → /u-s-endr-e/ /mu-si-endr-e/ → /musendre/

5.3.4.9 Dhamira tegemezi huweza kutumika na kiambishi ‘Ka’

Kitendo katika sentensi hutumia kiambishi ‘ka’ kuonyesha sasa tendo litendeke lakini mahali pengine tofauti na mahali pa uzungumzi. Katika Kitikuu katika nafsi ya kwanza na pili umoja kiambishi cha nafsi hudondoshwa lakini katika wingi huwepo. Hiyo ‘ka’ hutamkwa kwa mpumuo katika nafsi ya kwanza umoja.

- 81a) *Ngoj- a k'a - l - e wali.* (Ngoja nikale wali.)
mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio
 sasa cha dhamira
- Ngoja - ni chu - ka - l - e wali.* (Ngojeni tukale wali.)
mzizi mofimu nafsi 1 hali ya mzizi kiishio cha
 ya wingi wingi sasa dhamira
- 81b) *E- nendr - a ka - nunu - e ndridhi.* (Nenda kanunue ndizi.)
Nafsi 2 mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio cha
 sasa dhamira
- E- nendr - ani mu - ka - nunu - e ndridhi.* (Nendeni mkanunue ndizi.)
Nafsi 2 mzizi kiishio cha nafsi 2 hali ya mzizi kiishio cha
 dham.wingi wingi sasa dhamira
- 81c) *Mu - at - e → mwate a - ka - vas - e taa ni usiku.*
Mofimu mzizi kiishio cha nafsi 3 hali ya mzizi kiishio cha
 ngeli 1 umoja sasa dhamira
- (Mwache akawashe taa ni usiku.)

Va - at - e va - ka - vas - e taa ni usiku.


Mofimu mzizi kiishio cha nafsi 3 hali ya mzizi kiishio cha
Ngeli 2 dhamira wingi sasa dhamira

(Waache wakawashe taa ni usiku.)

Kielelezo matawi cha 81a) katika ukaguzi wa sifa kinaweza kuainishwa ifuatavyo:

81a) Ngoj- a k'a - l - e wali. (Ngoja nikale wali).

mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio
sasa cha dhamira



Katika kielelezo hiki vitenzi vikuu ni viwili ‘ngaja’ na ‘k’ale’ kwa hivyo kutakuwa na KT viwili katika sentensi moja. Kitenzi ‘kale’ huhamishwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at₁) hadi upatanishi kiima UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Japo kitenzi ‘ngaja’ hakina mofimu ya kiima lakini huwakilisha nafsi ya kwanza umoja, kwa hivyo badala ya kusema ‘ningaja’ inaweza kufupishwa ikawa ‘ngaja’, mofimu {ni} imedondoshwa, japo katika umbo mantiki (US) huwa ipo ni katika umbo la kifonetiki ndio hudondoshwa (UF). Kitenzi cha pili ‘k’ale’ kimesogezwa

kutoka T ya T¹ na kuacha athari kitenzi hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at₂), kinasogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira tegemezi na kuacha athari ya kitenzi (at₂). Hatimaye husogezwa kwenye kifundo cha UPk cha UPk¹ kukagua sifa ya uhusika kiima na kubaki hapo. Japo katika umbo fonetiki, mofimu ya uhusika haipo katika kitenzi hiko katika umbo mantiki mofimu hiyo ipo, hudondoshwa tu katika lahaja hii kwa hivyo haina budi kukagua sifa hiyo ya UPk. Kwa hivyo badala ya kusema ‘ningoja’ inaweza kufupishwa ikawa ‘nganja’. Yambwa ‘wali’ husogezwa kutoka N ya KT na kuacha athari (ay) hadi kwa spesifaya ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kinabaki hapo.

5.3.4.10 Ukanushi

81a) *U - si - ni - ngoj - e ku - l - a wali.* (Usiningoje kula wali.)

| | | | | | | | |
|---------|---------|---------|-------|-------------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | nafsi 1 | mzizi | kiishio cha | mofimu | mzizi | kiishio |
| umoja | kanushi | umoja | | dhamira | ku | | |

Mu- si - tu - ngoj - e ku- l - ani wali. (Msiningoje kuleni wali.)

| | | | | | | | |
|---------|---------|---------|-------|-------------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | nafsi 1 | mzizi | kiishio cha | mofimu | mzizi | kiishio |
| wingi | kanushi | wingi | | dhamira | ku | | wingi |

81b) *U - si - endr - e → usendre ku - nunu - a ndridhi.*

| | | | | | | |
|---------|---------|-------|-------------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio | mofimu | mzizi | kiishio |
| umoja | kanushi | | cha dhamira | ku | | |

(Usiende kununua ndizi)

Mu - si - endr - e ku - nunu - a → musendre kununua ndridhi.

| | | | | | | |
|---------|---------|-------|-------------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | mzizi | kiishio | mofimu | mzizi | kiishio |
| wingi | kanushi | | cha dhamira | ku | | |

(Msiende kununua ndizi.)

81c) *U - si - mu - at - e ku - vas - a taa ni usiku.*

| | | | | | | | |
|---------|---------|---------|-------|---------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | mofimu | mzizi | kiishio | mofimu | mzizi | kiishio |
| umoja | kanushi | mtendwa | | dhamira | ku | | |

(Usimuache kuwasha taa ni usiku.)

Mu - si - va - at- e ku - vas - a taa ni usiku.

Nafsi 2 mofimu mofimu mzizi kiishio mofimu mzizi kiishio
wingi kanushi mtendwa dhamira ku wingi

(Msiwaache kuwasha taa ni usiku.)

5.3.4.11 Kuonyesha azma au nia kwa kutumia au kutotumia maneno kama ‘ili’ au ‘kusudi’

82a) *A - li - som - a ili a - pach - e kadhi.* (Alisoma ili apate kazi.)

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio nafsi 3 mzizi dhamira
umoja iliyopita umoja tegemezi

Va - li - som - a ili va - pach - e kadhi. (Walisoma ili wapate kazi.)

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio nafsi 3 mzizi dhamira
wingi iliyopita wingi tegemezi

82b) *Hu - fany - a kadhi kusudi ni - pach - e chakula.*

Hali mzizi kiishio nafsi 1 mzizi dhamira
mazoea wingi tegemezi

(Hufanya kazi kususdi nipate chakula.)

Hu - fany - a kadhi kusudi chu - pach - e chakula.

Hali mzizi kiishio nafsi 1 mzizi dhamira
mazoea wingi tegemezi


(Hufanya kazi kusudi tupate chakula.)

Kielelezo matawi cha 82a) ni kama kifuatacho:

82a) *Alisoma ili apache kadhi.*

A - li - som - a ili a - pach - e kadhi. (Alisoma ili apate kazi.)

Nafsi 3 njeo mzizi kiishio nafsi 3 mzizi dhamira
umoja iliyopita umoja tegemezi



Kitenzi kikuu cha kwanza, ‘*alisoma*’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at₁) hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo iliyopita kisha husogezwa kwenye UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Neno ‘*ili*’ hufanya kazi kama fokasi hapo, na hivyo husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at₁) hadi FOK ya FOK¹ kukagua sifa ya fokasi na kubaki hapo. Kitenzi cha pili ‘*apache*’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at₂), kisha husogezwa hadi kifundo cha DHAM kukagua sifa ya dhamira tegemezi na kuacha athari (at₂), hatimaye husogezwa hadi kifundo cha UPk cha UPk¹

kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Nomino ‘*kadhi*’ hukaguliwa kutoka N ya KT na kuacha athari (ay), inasogezwa kutoka hapo hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.3.4.12 Matumizi ya Dhamira za Masharti: {ngali} na {ki}

Katika Kitikuu mofimu {ngali} na {ki} hutumika kuonyesha dhamira ya masharti katika sentensi. Kitikuu hakitumii mofimu ya {nge} na {ngeli} kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu kuonyesha masharti. Matumizi ya mofimu hizi zina matumizi zaidi lakini kwa ajili ya dhamira inaangazia tu pale inapotumiwa kama sharti.

Beaudoin (1999:135) anasema kuwa viambishi vya –nge- na –ngali- mara nyingi huchukuliwa kama viambishi vya njeo na hali, lakini haziingiliani na uchambuzi wa njeo na hali.

Vilevile Contini-Morava (1989), na Mohlig na Heine (1995) katika tasnifu ya Beaudoin (1999:137) wanadai kuwa tofauti kati ya matumizi ya –nge- na –ngali- hayaonyeshi tofauti ya njeo bali huonyesha kama kuna uwezekano wa sharti fulani kutimizika au la.

Vilevile matumizi haya pia hayaonyeshi hali kwa namna matumizi yake yanavyoingiliana katika sentensi ambatano, kama tutakavyoona baadaye. Na ndiyo maana mofimu zinazoonyesha masharti zinasimamia dhamira. (Beaudoin: 138).

Nakubaliana na maoni ya Beaudoin kuwa mofimu za masharti husimamia dhamira na sio njeo au hali, na katika fasili ya dhamira tegemezi hapo mwanzo, maelezo yanaonyesha pia kuwa ni masharti ambayo yanaweza kutimizika au la. Kwa hivyo, pale sentensi zenye mofimu hizi (-ngali- na -ki-) zitakopotumika kuonyesha masharti, basi zinakuwa zinawakilisha dhamira na sio njeo wala hali.

5.3.4.12.1 Matumizi ya Dhamira ya Masharti {-ngali-}

83a) *U - ngali - ku - y- a mapema u - ngali - pach - a mapeni ako.*

| | | | |
|------------------------|----------------------------|------------------------|---------------|
| Nafsi 2 dham. umoja | mofimu mzizi kiishio ku | nafsi 2 dham. umoja | mzizi kiishio |
|------------------------|----------------------------|------------------------|---------------|

(Ungekuja mapema ungepata pesa zako.)

Mu - ngali - ku - y- a mapema mu - ngali - pach - a mapeni enyu.

| | | | |
|------------------------|----------------------------|------------------------|---------------------------|
| Nafsi 2 dham. wingi | mofimu mzizi kiishio ku | nafsi 2 dham. wingi | mzizi kiishio masharti |
|------------------------|----------------------------|------------------------|---------------------------|

(Mungekuja mapema mungepata pesa zenu.)

83b) *Ni - ngali - iv - a mapema si - ngali - ku - endr - a → singalikwendra*

| | | | |
|------------------------|---------------|-------------------------|----------------------------|
| Nafsi 1 dham. umoja | mzizi kiishio | mofimu dham. kanushi | mofimu mzizi kiishio ku |
|------------------------|---------------|-------------------------|----------------------------|

(Ningejua mapema nisingekwenda.)

Chu - ngali - iv - a mapema ha - chu - ngali - ku - endr - a → hachungalikwendra

| | | | |
|------------------------|---------------|---------------------------------------|-------------------------------------|
| Nafsi 1 dham. wingi | mzizi kiishio | mofimu nafsi 1 dham. kanushi wingi | mofimu mzizi kiishio masharti ku |
|------------------------|---------------|---------------------------------------|-------------------------------------|

(Tungejua mapema hutungekwenda.)

83c) *Numba hii i - ngali - ni - anguk - i - a i - ngali - ni - vu - a.*

| | | | |
|--|---|-------------------|--------------------------------|
| Mofimu njeo dham. upatanishi masharti | nafsi 1 mzizi kauli kiishio njeo umoja tendea upatanishi | dham. masharti | nafsi 1 mzizi kiishio umoja |
|--|---|-------------------|--------------------------------|

(Nyumba hii ingelinangukia ingelinua.)

Numba hidhi dhi - ngali - chu - anguk - i - a dhi - ngali - chu - vu - a.

| | | | |
|--|---|-------------------|--------------------------------|
| Mofimu ya dham. upatanishi masharti | nafsi 1 mzizi kauli kiishio njeo wingi tendea upatanishi | dham. masharti | nafsi 1 mzizi kiishio wingi |
|--|---|-------------------|--------------------------------|


(Nyumba hizi zingalituangukia zingalituua.)

Kielelezo matawi cha 83a) ni kama kifuatacho:

U - ngali - ku - y- a mapema u - ngali - pach - a mapeni ako.

| | | | |
|------------------------|----------------------------|-----------------------|---------------|
| Nafsi 2 dham. umoja | mofimu mzizi kiishio ku | nafsi 2 hali umoja | mzizi kiishio |
|------------------------|----------------------------|-----------------------|---------------|

(Ungekuja mapema ungepata pesa zako.)



Kitenzi cha kwanza ‘*ungalikuya*’ huhamishwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at) hadi NJ ya NJ¹ kukagua njeo iliyopita, na kuacha athari (at₁) kisha husogezwa hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira ya masharti na kuacha athari (at₁) na hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kivumishi ‘*mapema*’ hakisogezwi kinabaki katika V ya KN kwa sababu hakina sifa za kimofolojia hivyo hakina sifa ya kusogezwa na kukaguliwa. Kitenzi cha pili ‘*ungalipacha*’ husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at₂) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at₂), kisha kinasogezwa tena hadi NJ ya NJ¹ kukagua sifa ya njeo iliyopita na baadaye husogezwa katika kifundo cha DHAM ya DHAM¹ kukagua dhamira ya masharti na kuacha athari (at₂), hatimaye

husogezwa katika UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo.

Nomino ‘mapeni ako’ husogezwa kutoka KN ya T¹ hadi SPES ya KUPy kupima sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.3.4.12.2 Matumizi ya Dhamira ya masharti {ki}

Mofimu {ki} imeangaziwa mbeleni kama mofimu ya hali katika kazi hii, lakini inapotumika kama mofimu ya masharti basi inakuwa ni dhamira tegemezi. Kama katika mofimu ya {ngali}, mofimu ya {ki} huonyesha kuwa mambo yangekuwa tofauti iwapo tendo fulani lingefanyika. Kwa hivyo ni sharti kwa jambo fulani lifanyike ndipo lingine liweze kuwa. Lazima vitenzi viwe viwili kama katika dhamira tegemezi ya -ngali-

84a) *U - ki - ni - lip - a 'ta - kw - ech - e - a dhichi dhako.*

| | | | | | | | | |
|---------------------------------|------------------|----------------|-------------------|---------------|------------------|-----------------|-----------------|---------|
| Nafsi 2 dham. umoja masharti | kiamb. yambwa | mzizi ijayo | kiishio yambwa | njeo ijayo | kiamb. yambwa | mzizi tendea | kauli tendea | kiishio |
|---------------------------------|------------------|----------------|-------------------|---------------|------------------|-----------------|-----------------|---------|

(Ukinilipa nitakuletea viti vyako.)

Mu - ki - chu - lip - a chu - ta - va - ech - e - a dhichi dhenyu.

| | | | | | | | | | |
|---------------------------------|------------------|----------------|------------------|------------------|---------------|------------------|-----------------|-----------------|---------|
| Nafsi 2 dham. wingi masharti | kiamb. yambwa | mzizi wingi | kiishio wingi | nafsi 1 ijayo | njeo ijayo | kiamb. yambwa | mzizi tendea | kauli tendea | kiishio |
|---------------------------------|------------------|----------------|------------------|------------------|---------------|------------------|-----------------|-----------------|---------|

(Mukitulipa tutawaletea viti vyenu.)

84b) *U - ki - li - a 'ta - ku - pondr - a .* (Ukilia nitakupiga.)

| | | | | | | |
|---------------------------------|-------------------|----------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|
| Nafsi 2 dham. umoja masharti | njeo iliyopita | kiishio iliyopita | njeo ijayo | kiamb. yambwa | mzizi yambwa | kiishio |
|---------------------------------|-------------------|----------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|

Mu - ki - li - a chu - ta - va - pondr - a. (Mkilia tutawapiga.)

| | | | | | | | |
|---------------------------------|-------------------|------------------|------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|
| Nafsi 2 dham. wingi masharti | njeo iliyopita | kiishio wingi | nafsi 1 ijayo | njeo ijayo | kiamb. yambwa | mzizi yambwa | kiishio |
|---------------------------------|-------------------|------------------|------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|

84c) *A - ki - ni - said - i - a kadhi 'ta - n - lip - a.*

| | | | | | | | | |
|---------------------------------|------------------|-----------------|-----------------|-------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|
| Nafsi 3 dham. umoja masharti | kiamb. yambwa | mzizi tendea | kauli tendea | kiishio yambwa | njeo ijayo | kiamb. yambwa | mzizi yambwa | kiishio |
|---------------------------------|------------------|-----------------|-----------------|-------------------|---------------|------------------|-----------------|---------|

(Akinisaidia kazi nitamlipa.)


Va - ***ki*** - *chu* - *said* - *i* - *a* *kadhi* *chu* - *ta* - *va* - *lip* - *a*.

| | | | | | | | | | | |
|---------|----------|--------|--------|-------|---------|---------|-------|--------|-------|---------|
| Nafsi 3 | dham. | kiamb. | mzizi | kauli | kiishio | nafsi 3 | njeo | kiamb. | mzizi | kiishio |
| wingi | masharti | yambwa | tendea | | | wingi | ijayo | yambwa | | |

(Wakitusadia kazi tutawalipa.)

Kielelezo matawi cha 84a ni kama kifuatacho kulingana na ukaguzi wa sifa:

84a) *Ukinilipa 'takwechea dhichi dhako.* (Ukinilipa nitakuletea viti vyako).



Kitenzi cha kwanza cha KT (1) ‘*ukinilipa*’ katika sentensi hii kinasogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at_s) hadi TEW ya TEW¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa tendwa na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira ya masharti, hatimaye husogezwa katika UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi cha pili cha KT (2) ‘*takwechea*’ hukaguliwa kutoka T ya T’ na kuacha athari hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at_{kuu}), kisha kinasogezwa hadi IA ya IA¹ kukagua sifa ya kauli ya kutenda na kuacha athari (at_{kuu}) kisha kusogezwa katika NJ ya NJ¹ kukagua njeo ijayo na kuacha athari (at_{kuu}), hatimaye kinasogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Ijapokuwa mofimu ya kiima hapo imedondoshwa, ni katika umbo fonetiki (UF) tu lakini katika umbo matinki (US) mofimu hiyo ya {ni} ipo. KN ya ‘*dhichi dhako*’ husogezwa pamoja kutoka KN ya T¹ hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.3.4.13 Ukanushi

Katika ukanushi wa mofimu {ki} ya masharti, mofimu {sipo} hutumika katika Kitikuu kama ilivyo katika Kiswahili Sanifu.

84a) *U - sipo - ni - lip - a si - kw - eche - i - dhichi dhako.*

| | | | | | | | | |
|---------|---------|--------|-------|---------|---------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | kiamb. | mzizi | kiishio | mofimu | kiamb. | mzizi | kiishio |
| umoja | kanushi | yambwa | | | kanushi | yambwa | | kanushi |

(Usiponilipa sikuletei viti vyako.)

Mu - sipo - ni - lip - a si - va - eche - i dhichi dhenyu.

| | | | | | | | | |
|---------|---------|--------|-------|---------|---------|--------|-------|---------|
| Nafsi 2 | mofimu | kiamb. | mzizi | kiishio | mofimu | kiamb. | mzizi | kiishio |
| wingi | kanushi | yambwa | | | kanushi | yambwa | | kanushi |

(Msiponilipa siwaletei viti vyenu.)

84b) *U - sipo - li - a si - ku - pondr - i.* (Usipolia sikupigi.)

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio mofimu kiamb. mzizi kiishio
umoja kanushi kanushi yambwa kanushi

Mu - sipo - li - a si - va - pondr - i. (Msipolia siwapigi.)

Nafsi 2 mofimu mzizi kiishio mofimu kiamb. mzizi kiishio
wingi kanushi kanushi yambwa kanushi

84c) *A - sipo - ni - saidi - a kadhi si - n - lip - i.*

Nafsi 3 mofimu kiamb. mzizi kiishio mofimu kiamb. mzizi kiishio
umoja kanushi yambwa kanushi yambwa kanushi

(Asiponissaidia kazi simlipi.)

Va - sipo - chu - saidi - a kadhi ha - chu - va - lip - i.

Nafsi 3 mofimu kiamb. mzizi kiishio mofimu nafsi 3 kiamb. mzizi kiishio
wingi kanushi yambwa kanushi wingi yambwa kanushi

(Wasipotusaidia kazi hatuwalipi)

5.4 Muingiliano wa Njeo, Hali na Dhamira katika Sentensi Ambatano

Baada ya kuangalia njeo, hali na dhamira, hapa inaendelea kuchanganua mofimu hizo za njeo, hali na dhamira katika maingiliano yake kama yanavyojitokeza katika sentensi ambatano. Sentensi ambatano hizo zina muundo wa kitenzi kisaidizi cha **kuwa** au **kuwa na** na kitenzi cha pili, ambacho ni kitenzi kikuu. Vitenzi hivyo vitabeba mofimu za njeo, hali na dhamira katika muundo wake wa sentensi ambatano. Katika miundo hiyo ya sentensi za Kitikuu, sio kila mofimu za njeo, hali na dhamira zinaweza kuchukuliwa tu na kubandikwa mahali popote, bali kuna baadhi za njeo au hali ambazo haziwezi kupatikana katika muingiliano huo .

Kwa kawaida, mofimu za njeo kama vile {ta} na {li} hazipatikani katika vitenzi vikuu, bali hupatikana katika vitenzi visaidizi katika sentensi ambatano zenyenye vitenzi vya - **kuwa**. Mofimu za hali za aina mbalimbali hujitokeza katika vitenzi vikuu. Kitikuu kama vile Kiswahili Sanifu, njeo inayozungumzia juu ya tendo fulani huonyeshwa kwanza

kabla ya hali inayozungumziwa, (Beaudoin 1999,14). Mfano: **Tulikuwa tumelala**, ambapo mofimu ya njeo {li} inajitokeza kisha ya hali timilifu {me} katika sentensi hiyo. Katika Kitikuu itakuwa: *Chwaliko chundoiyala*. Katika Kitikuu kitenzi *chwalikuva* (tulikuwa) kinaweza kufupishwa na kuwa *chwaliko*. Mofimu {li} ni ya njeo iliyopita na mofimu {ndo} **ni** ya hali timilifu. Mofimu za dhamira tegemezi kama {ki} na {ngali} pia zitatumika mahali hapo pa njeo au hali katika sentensi ambatano. Hapa mofimu za njeo, hali na dhamira zitaangaziwa zinavyoingiliana katika sentensi mseto wa sentensi ambatano.

5.4.1 Mofimu {-ta-} katika sentensi ambatano

Njeo **-ta-** inayoonyesha njeo ijayo, katika Kitikuu huonyesha matumizi yake katika kitenzi kisaidizi kwa sentensi ambatano. Mofimu hii hutumika pamoja na mofimu za hali zifuatazo zinazoambishwa katika vitenzi vikuu:

- a) Mofimu - ndo
 - b) Mofimu – hu
 - c) Mofimu – ki
 - d) Mofimu - ndo+sha
- 85a) *Mwana a- ta - ku - v - a ndo - iyal - a .* (Mtoto atakuwa amelala.)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja ijayo ku timilifu

- 85b) *Va - ta - ku- v - a hu - pik - a kesho.* (Watakuwa wanapika kesho.)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio
wingi ijayo ku kuendelea

- 85c) *Chu- ta - ku - v - a chu - ki - imb - a va - ki - y - a.*

Nafsi 1 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 1 hali ya mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi ijayo ku wingi mazoea wingi mazoea

(Tutakuwa tukiimba wakija.)

85d) *A- ta- ku- v- a ndo - kw - ish -a ku- l - a a- ki- y- a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mofimu mzizi kiishio kitenzi mzizi kiishio nafsi3 hali mzizi kiishio wingi iliyopita ku timilifu ku kisoukomo umoja mazoea

(Atakuwa ameshakula akija.)


Ikumbukwe kuwa mofimu {**hu**}- hapa ya (85b) ni ile ya kuendelea, kwa Kiswahili Sanifu inatumia mofimu {**na**}.

Sentensi 86a) katika kitenzi chake cha pili, mofimu ya upatanishi kiima {**a**} imedondoshwa ili kurahisisisha matamshi, lakini katika umbo mantiki (US), mofimu hiyo ipo japo haidhihiriki katika umbo fonetiki (UF). Hata kitenzi cha kwanza mofimu hiyo {**a**} katika umbo fonetiki huweza kudondoshwa lakini katika umbo mantiki huwa ipo. Vilevile katika kitenzi cha pili sentensi 85d) ‘ndokuya’ badala ya ‘andokuya’.

Kielelezo matawi cha 85a) *Mwana atakuva ndoiyala.*

Mwana a- ta - ku - v - a ndo - iyal - a (Mtoto atakuwa amelala.)

Nafsi 3 njeo mofimu ku mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja Ijayo timilifu



Nomino ‘*Mwana*’ husogezwa kutoka SPES ya KT na kuacha athari (ak) hadi SPES ya KUPk kukagua uhusika wa kiima na kubaki hapo. Sentensi hiyo ina vitenzi viwili, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Kitensi kisaidizi ‘*atakuva*’, husogezwa kutoka T ya T¹ hadi NJ ya NJ¹ kukagua njeo ijayo na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitensi kikuu ‘*ndoiyala*’, husogezwa kutoka T ya T¹ na kuacha athari (at_{kuu}) hadi HAL ya HAL¹ kukagua hali timilifu na kuacha athari (at_{kuu}), kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitensi na kubaki hapo.

5.4.2 Mofimu {-li-} katika sentensi ambatano

Mofimu ya njeo {li} hupatikana katika vitenzi visaidizi kwa sentensi ambatano kama vile katika matumizi ya njeo –ta- hapo mwanzoni. Katika kitensi kikuu cha sentensi hizo ambatano zitatumia mofimu za hali zifuatazo katika Kitikuu:

- a) Mofimu – ndo
 - b) Mofimu – ki
 - c) Mofimu – hu
 - d) Mofimu – ndo+sha
- 86a) *A - li - ku - v - a ndo - kachik- a sana.* (Alikuwa amekatika sana.)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja iliyopita ku timilifu

- 86b) *Chu- li - ku - v - a chu - ki - pend - a ku - imb - a.*

Nafsi 1 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 1 hali ya mzizi kiishio kitensi mzizi kiishio
wingi iliyopita ku wingi mazoea kisoukomu

(Tulikuwa tukipenda kuimba.)

- 86c) *Juma a - li - ku - v - a hu - uk- a a - ka - anguk - a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio nafsi 3 hali ya mzizi kiishio
umoja iliyopita ku mazoea umoja mfululizo


(Juma alikuwa anaruka akaanguka.)

Sentensi 86a) kitenzi cha pili ‘**ndokuva**’ huweza kudondosha mofimu ya nafsi ya ‘a’ lakini hii ni katika tu umbo fonetiki, katika umbo mantiki mofimu hiyo ipo kama tulivvyotangulia kusema. Katika Kitikuu ni kupunguza urudiaji wa nafsi ‘a’ ambayo tayari ipo katika kitenzi kisaidizi ‘**alikuva**’.

Mchoro matawi wa 86a) unaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:

86a) *A - li - ku - v - a ndo - kachik- a sana.* (Alikuwa amekatika sana.)

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umaja iliyopita ku mazoea



Sentensi ina vitenzi viwili, kitenzi kikuu na kitenzi kisaidizi. Kitenzi kisaidizi ‘*alikuva*’ kinahamishwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (*atₛ*) hadi NJ ya NJ¹ kukagua njeo iliyopita, kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*ndokachika*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (*atₖᵣᵣ*) hadi kifundo cha HAL kukagua hali timilifu na kuacha athari (*atₖᵣᵣ*), kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kielezi ‘*sana*’ hakisogezwi kitabaki katika kifundo cha kitenzi chini ya kielezi (E) kwani hakina sifa za kimofolojia kukiwezesha kusogezwa na kukaguliwa.

5.4.3 Mofimu {-ndo-}

Hali timilifu ya **-ndo-** pia hutumika katika sentensi ambatano na hutumika katika kitenzi kikuu katika sentensi hizo. Mofimu hii hutumika pamoja na mofimu zifuatazo:

- a) Mofimu –li-
- b) Mofimu –ta-
- c) Mofimu –ki-
- d) Mofimu –ngali-
- e) Mofimu –ka-
- f) Mofimu –hu-

Mifano ya matumizi yake katika sentensi kwa kutumia kitenzi kisaidizi cha kuwa:

87a) *Vanave va - li - ku - v - a va - ndo - dham - a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi iliyopita ku wingi timilifu

(Watoto wake walikuwa wamezama.)

87b) *A - ta - ku - v - a ndo - ku - y - a kesho.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mofimu mzizi kiishio
umoja ijayo ku timilifu ku

(Atakuwa amekuja kesho.)

87c) *A - ki - v - a ndo - ku - y - a n - samehe.*

Nafsi 3 dham. mzizi kiishio hali mofimu mzizi kiishio mtendwa mzizi
umoja masharti timilifu ku

(Akiwa amekuja msamehe.)

87d) *Mu - ngali - ku - v - a mu - ndo - po - a mu - ngali - safir - i.*

Nafsi 2 dham. mofimu mzizi kiishio nafsi 2 hali mzizi kiishio nafsi 2 dham. mzizi kiishio
wingi masharti ku wingi timilifu wingi masharti

(Mngelikuwa mumepona mngeesafiri).

87e) *Mwidhi a - li - ku - v - a ndo - kimb - a a - ka - shik - w - a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kauli kiishio
umoja iliyopita ku timilifu umoja mfululizo tendwa

(Mwizi alikuwa amekimbia akashikwa.)

87f) *Hu - v - a ni - ndo - iyal - a saa hidhi.*

Hali mzizi kiishio nafsi 1 hali mzizi kiishio
mazoea umoja timilifu


(Huwa nimelala saa hizi.)

Kielelezo matawi cha 87a) kwa ukaguzi wa sifa kinaweza kuonyeshwa katika mchoro ufuatao:

87a) *Vanave va - li - ku - v - a va - ndo - dham - a.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
wingi iliyopita ku wingi timilifu

(Watoto wake walikuwa wamezama.)



Nomino ‘vanave’ husogezwa kutoka SPES ya kirai tenzi (KT) na kuacha athari (ak), hadi SPES ya KUPk kukagua uhusika kiima na kubaki hapo. Kitenzi kisaidizi ‘valikuva’

husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at_s) hadi kifundo cha njeo (NJ ya NJ¹) kukagua njeo iliyopita na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitensi kikuu ‘*vandodhama*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at_{kuu}) hadi kifundo cha HAL kukagua sifa ya hali timilifu na kuacha athari (at_{kuu}). Kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitensi na kubaki hapo.

5.4.4 Mofimu {Ki}

Mofimu {ki} nayo inatumika katika kitensi kikuu kikitanguliwa na kitensi kisaidizi cha **kuwa**. Mofimu hii huweza kutumika na mofimu zifuatazo katika sentensi:

- a) Mofimu –li-
- b) Mofimu –ta-
- c) Mofimu –ndo
- d) Mofimu –ka-
- e) Mofimu –hu-
- f) Mofimu -ngali-

Matumizi yake katika sentensi ni kama ifuatavyo:

| | | | | | | | | |
|------|------------------|-------------------|--------------|------------------|-------------------|------------------|--------------|-----------|
| 88a) | <i>Na-</i> | <i>li -</i> | <i>ku -</i> | <i>v -</i> | <i>a</i> | <i>ki -</i> | <i>som -</i> | <i>a.</i> |
| | Nafsi 1 umoja | njeo iliyopita | mofimu ku | mzizi kiishio | hali ya mazoea | mzizi kiishio | | |

(Nilikuwa nikisoma.)

| | | | | | | | | | | |
|------|------------------|---------------|--------------|------------------|------------------|-------------------|------------------|--------------|----------|-------------------|
| 88b) | <i>Va-</i> | <i>ta -</i> | <i>ku -</i> | <i>v -</i> | <i>a</i> | <i>va -</i> | <i>ki -</i> | <i>imb -</i> | <i>a</i> | <i>siku hiyo.</i> |
| | Nafsi 3 wingi | njeo ijayo | mofimu ku | mzizi kiishio | nafsi 3 wingi | hali ya mazoea | mzizi kiishio | | | |

(Watakuwa wakiimba siku hiyo.)

| | | | | | | | | | | | | |
|------|------------------|------------------|--------------|------------------|------------------|------------------|------------------|-----------------|---------------|------------|----------|----------------------|
| 88c) | <i>Va-</i> | <i>ndo-</i> | <i>ku -</i> | <i>v -</i> | <i>a</i> | <i>va -</i> | <i>ki -</i> | <i>i -</i> | <i>fany -</i> | <i>i -</i> | <i>a</i> | <i>tu mambo avo.</i> |
| | Nafsi 3 wingi | hali timilifu | mofimu ku | mzizi kiishio | nafsi 3 wingi | mtenda mazoea | mzizi kiishio | kauli tendea | | | | |

(Wamekuwa wakijifanya tu mambo yao.)

- 88d) *A - ka - v - a a - ki - angali- a hana la ku - nen - a.*
 Nafsi 3 hali mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio mofimu ku mzizi kiishio
 umoja mfulullizo umoja mazoea

(Akawa akiangalia hana la kusema.)

- 88e) *Hu - v - a va - ki - som - a wakati huu.*
 Hali mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio
 mazoea wingi mazoea

(Huwa wakisoma wakati huu.)


- 88f) *A - ngali - ku - v - a a - ki - som - a a- ngali - ku- v - a mbali.*
 Nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio
 umoja masharti ku umoja masharti umoja masharti ku

(Angekuwa akisoma angekuwa mbali.)

Mchoro matawi wa 88a) kulingana na Uminimalisti unaweza kuonyeshwa kama ifuatavyo:

- 88a) *Nalikuva kisoma.* (Nilikuwa nikisoma.)

- 88a) *Na- li - ku - v - a ki - som - a.*
 Nafsi 1 njeo mofimu mzizi kiishio hali ya mzizi kiishio
 umoja iliyopita ku mazoea



Katika kielelezo hicho, kitenzi kisaidizi ‘nalikuva’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at_s) hadi kifundo cha njeo (NJ ya NJ¹) kukagua njeo iliyopita

na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi hicho na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*kisoma*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at_{kuu}) hadi kifundo cha hali, kukagua hali ya mazoea na kuacha athari (at_{kuu}), kinasogezwa tena hadi kifundo cha upatanishi kiima (UPk ya UPk¹) kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo.

Mofimu {ki} pia inapotumika kama dhamira tegemezi kuonyesha masharti, huweza kutumika katika kitenzi kisaidizi. Huweza kutumika pamoja na:

a) Mofimu {hu}

b) Mofimu {ta}

c) Mofimu {ndo}

89a) *U - ki - v - a n - shindran- i hu - um - i - a.*

| | | | | | | | | | | |
|---------------|----------|---------|--------|-------|---------|------|--------|-------|-------|---------|
| Nafsi 2 dham. | mzizi | kiishio | kiamb. | mzizi | kiishio | hali | mazoea | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | masharti | | yambwa | | tendea | | | | | |

(Ukiwa mshindani hummia.)

89b) *Mu - ki - v - a barabarani mapema mu - ta - pach - a gari.*

| | | | | | |
|---------------|----------|---------|--------------|-------|---------|
| Nafsi 2 dham. | mzizi | kiishio | nafsi 2 njeo | mzizi | kiishio |
| wingi | masharti | | wingi | ijayo | |

(Mkiwa barabarani mapema mtapata gari.)

89c) *A - ki - v - a ndo - anguk - a m - pek - e sipichali.*

| | | | | | | | | |
|---------------|----------|---------|----------|-------|---------|---------|-------|----------|
| Nafsi 1 dham. | mzizi | kiishio | hali | mzizi | kiishio | mtendwa | mzizi | dhama |
| umoja | masharti | | timilifu | | | | | tegemezi |


(Akiwa ameanguka mpeleke hospitali.)

Kielelezo matawi cha 89a) kinaweza kuainishwa kama kifuatavyo:

89a) *Ukiva nshindrani hummia.* (Ukiwa mshindani hummia.)

U - ki - v - a n - shindran- i hu um - i - a

| | | | | | | | | | |
|---------------|----------|---------|--------|-------|---------|------|-------|-------|---------|
| Nafsi 2 dham. | mzizi | kiishio | kiamb. | mzizi | kiishio | hali | mzizi | kauli | kiishio |
| umoja | masharti | | yambwa | | tendea | | | | |



Kitenzi kisaidizi ‘*ukiva*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (*at_s*) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (*at_s*), husogezwa tena hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua dhamira ya masharti na kuacha athari (*at_s*), hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*huumia*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (*at_{kuu}*) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (*at_{kuu}*), kinasogezwa tena hadi kifundo cha hali (HAL) kukagua hali ya mazoea na kuacha athari (*at_{kuu}*), hatimaye husogezwa katika kifundo cha UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Nomino ‘*nshindrani*’ husogezwa kutoka N ya T¹ hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

5.4.5 Mofimu { hu-}

Mofimu huu huambishwa katika kitenzi kisaidizi cha kuwa kama viambishi vingine vya hali. Katika Kitikuu, kama tulivyoelezea hapo mbeleni, mofimu {hu} husimamia

mofimu -**na-** ya hali ya sasa ya kuendelea, na **hu-** ya mazoea katika Kiswahili Sanifu.

Mofimu {**hu**} katika Kitikuu huweza kuambishwa mofimu zifuatazo:

- a) Mofimu {ta}
- b) Mofimu {li}
- c) Mofimu {ki}
- d) Mofimu {me}
- e) Mofimu {ka}
- f) Mofimu {ndo} + {sha}

Matumizi ya mofimu hizo katika miktadha ya sentensi:

90a) *A - ta - ku - v - a hu - som - a wakati hoo.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja ijayo ku mazoea

(Atakuwa anasoma wakati huo.)

90b) *A - li - ku - v - a hu - imb - a chu - ki - endr - a → chukendra.*

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio nafsi 1 hali mzizi kiishio
umoja iliyopita ku mazoea wingi mazoea

(Alikuwa anaimba tukienda.)

90c) *U - ki - v - a ndhivu hu - iyal - a na ndaa.*

Nafsi 2 dham. mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja masharti mazoea

(Ukiwa mvivu hulala na njaa.)

90d) *Ndo - ku - v - a hu - iyal - a tu.*

Hali mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
timilifu ku mazoea

(Amekuwa analala tu / Amekuwa hulala tu.)

90e) *Chu - li - po - kw - endr - a a - ka - v - a hu - rud- i.*

Nafsi 1 njeo mofimu mofimu mzizi kiishio nafsi 3 hali mzizi kiishio hali mzizi kiishio
wingi iliyopita wakati ku umuja mfululizo kuendelea

(Tulipokwenda akawa anarudi.)

90f) *Ndo - kw - ish - a ku - v - a hu - jep - a tu maisha ake.*

Hali mofimu mzizi kiishio mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
timilifu ku ku mazoea


(Ameshakuwa huiba tu maisha yake.)

Kielelezo matawi cha 90a) katika ukaguzi wa sifa ni kama kifuatacho;

90a) *Atakuva husoma wakati hoo.* (Atakuwa husoma wakati huo)

A - ta - ku - v - a hu - som - a wakati hoo.

Nafsi 3 njeo mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja ijayo ku mazoea



Kitenzi kisaidizi ‘*atakuva*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi (T ya T¹) na kuacha athari (atₙ) hadi kifundo cha njeo kukagua sifa ya njeo ijayo, husogezwa tena hadi kifundo cha upatanishi kiima kukagua sifa ya uhusika kiima katika kitenzi hicho na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*husoma*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (atₖuu) hadi kifundo cha HAL kukagua hali ya mazoea na kuacha athari (atₖuu), kisha kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kielezi ‘*wakati hoo*’ hakisogezwi kwani hakina sifa za kimofolojia za kufanya kisogezwe.

5.4.6 Mofimu {ngali}

Mofimu {ngali} ya dhamira tegemezi ya kuonyesha masharti au matamanio ambayo hayakuweza kufikiwa. Mofimu hii hutumika pamoja na kitenzi kisaidizi katika sentensi ambatano na kuchukua mofimu nyingine mbalimbali katika kitenzi kikuu. Zinaweza kuchukua mofimu zifuatazo:

- a) Mofimu {ngali}
- b) Mofimu {ndo}
- c) Mofimu {ki}
- d) Mofimu {hu}

91a) *U - ngali - ku - v - a na bidii u - ngali - pich - a ntihani.*

Nafsi 2 dham. mofimu mzizi kiishio
umoja masharti ku nafsi 2 dham. mzizi kiishio
umoja masharti

(Ungekuwa na bidii ungepita mtihani.)

91b) *Si - ngali - ku - v - a ni - ndo - chok - a ni - ngali - kw - endr - a.*

Mofimu dham. mofimu mzizi kiishio nafsi 1 hali mzizi kiishio nafsi 1 dham. mofimu mzizi kiishio
kanushi masharti ku umoja timilifu umoja masharti ku

(Singalikuwa nimechoka ningalikwenda.)

91c) *A- ngali - ku - v - a a - ki- som- a a - si - ngali - anguk - a ntihani.*

Nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio nafsi 3 dham. mzizi kiishio nafsi 3 mofimu dham. mzizi kiishio
umoja masharti ku umoja masharti umoja kanushi masharti

(Angekuwa akisoma asingeanguka mtihani.)

91d) *Chu - ngali - ku - v - a hu - pich - a mwichuni sasa.*

Nafsi 1 dham. mofimu mzizi kiishio hali mzizi kiishio
umoja masharti ku kuendelea


(Tungekuwa tunapita msituni sasa).

Kielelezo matawi cha 91a) kinawenza kuonyeshwa kama kifuatavyo:

91a) *Ungalikuva na bidii ungalipicha nithani.* (Ungekuwa na bidii ungepita mtihani.)

91a) *U - ngali - ku - v - a na bidii u - ngali - pich - a ntihani.*

Nafsi 2 dham. mofimu mzizi kiishio nafsi 2 dham. mzizi kiishio
umoja masharti ku umoja masharti



Katika kielelezo hicho kitenzi kisaidizi, ‘*ungalikuva*’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari hadi kifundo cha UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya uhusika yambwa na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi kifundo cha dhamira kukagua sifa ya dhamira ya masharti na kuacha athari (at_s), husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Kitenzi kikuu ‘*ungalipicha*’ kinasogezwa kutoka kifundo cha kitenzi na kuacha athari (at_{kuu}) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at_{kuu}). Husogezwa tena hadi kifundo cha dhamira kukagua dhamira ya masharti na kuacha athari (at_{kuu}). Hatimaye husogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima na kubaki hapo. Nomino ‘*bidii na ntihani*’ husogezwa kutoka N ya T¹ hadi SPES ya KUPy kukagua sifa za uhusika kiima na vinabaki hapo.

Hata hivyo, mofimu ya {ngali} kwa kuwa si ya njeo wala hali bali ni ya dhamira tegemezi kama vile mofimu {ki}, huweza kutumika pia katika kitenzi kikuu katika sentensi na sio katika kitenzi kisaidizi pekee.

92a *A - ngali - kw - endr - a hondreni a - ngali - pach - a mahembe tuu.*

| | |
|---|---|
| Nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio | nafsi 3 dhami. mzizi kiishio |
| umoja masharti ku | umoja masharti |

(Angelikwenda shmbani angelipata maembe mengi.)

92b *A - ngali - tedh - a kwa bidii a - ngali - chudh - w - a sana.*

| | | |
|---------------------------------------|---|--------|
| Nafsi 3 dham. mzizi kiishio | nafsi 3 dham. mzizi kauli kiishio | |
| umoja masharti | umoja masharti | tendwa |

(Angelicheza kwa bidii angelituzwa sana.)

92c *Va - ngali - ku - y - a kwechu chu - ngali - va - karib - ish - a .*

| | | |
|---|--|----------|
| Nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio | nafsi 1 dham. kiambi. mzizi kauli kiishio | |
| wingi masharti ku | wingi masharti yambwa | tendesha |

(Wangalikuja kwetu tungeliwakaribisha.)


Mchoro matawi wa 92a kulingana na nadharia ya ukaguzi wa sifa ni kama ufuatao:

92a) *Angalikwenda hondreni angalipacha mahembe tuu.*

(Angelikwenda shambani angelipata maembe mengi.)

92a) *A - ngali - kw - endr - a hondreni a - ngali - pach - a mahembe tuu.*

| | |
|---|--|
| Nafsi 3 dham. mofimu mzizi kiishio | nafsi 3 dhamira mzizi kiishio |
| umoja masharti ku | umoja masharti |



Kulingana na kielelezo hapo, kuna vitenzi vikuu viwili, kwa hivyo kutakuwa na virai tenzi viwili kuonyesha kama sentensi ni mbili kwenye moja. Kitenzi cha kwanza ‘angalikwendra’ husogezwa kutoka kifundo cha kitenzi, T ya T¹ na kuacha athari (at₁) hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua dhamira ya masharti na kuacha athari (at₁), kinasogezwa tena hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi hicho na kubaki hapo. ‘Hondreni’ ni kielezi na kitabaki bila ya kusogezwa kwa sababu hakina sifa za kimofolojia za kufanya kisogezwe. Kitenzi cha pili ‘angalipacha’, kitasogezwa kutoka kifundo cha kitenzi (T ya T¹) na kuacha athari (at₂) hadi UPy ya UPy¹ kukagua sifa ya upatanishi yambwa na kuacha athari (at₂); kisha husogezwa tena

hadi DHAM ya DHAM¹ kukagua sifa ya dhamira ya masharti na kuacha athari (at₂), hatimaye husogezwa hadi UPk ya UPk¹ kukagua sifa ya upatanishi kiima katika kitenzi na kubaki hapo. Kirai nomino ‘mahembe tuu’ kitasogezwa pamoja kutoka KN ya T¹ na kuacha athari yambwa (ay) hadi SPES ya KUPy kukagua sifa ya uhusika yambwa na kubaki hapo.

Mifano ya sentensi ya 92 hapo inadhihirisha kuwa mofimu ya {ngali} ni ya dhamira na sio hali wala njeo, na ndiyo maana mofimu hizo zinatumika katika sentensi moja kama vitenzi vikuu vyote viwili.

5.5 Hitimisho

Sura hii ni uchanganuzi na uwasilishaji wa data juu ya njeo, hali na dhamira katika Kitikuu. Imebainika kuwa kitenzi ni kategoria ya maneno yenye uwezo mkubwa wa kuweza kuambishwa viambishi au mofimu mbalimbali. Mofimu za njeo, hali na dhamira ni baadhi tu ya mofimu zinazoambishwa katika kitenzi. Mofimu hizo mbalimbali ni kama za njeo ni {a}, {li} na {ta}. Mofimu za hali ni {hu}, {ka}, {ki} {ndo} na {ie}. Mofimu za dhamira ni pamoja na {ngali}, {ki}, {a} na {e}. Hatimaye uchanganuzi wa mofimu hizo huonyeshwa kupitia ukaguzi wa sifa katika nadharia ya Uminimalisti.

Sura hii mwishoni imeonyesha mwingiliano kati ya njeo, hali na dhamira katika sentensi ambatano. Katika uchanganuzi wa awali, mofimu za njeo, hali na dhamira zilijitokeza kivyake katika sentensi sahili, bila kutumika kwa pamoja katika sentensi. Baadaye imeangazia jinsi mofimu hizo za njeo, hali na dhamira zinavyoweza kutumiwa pamoja katika miktadha ya sentensi ambatano na uchanganuzi wake kupitia ukaguzi wa sifa.

SURA YA SITA

MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

6.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia matokeo ya utafiti kwa muhtasari, juu ya kazi za njeo, hali na dhamira chini ya nadharia ya ukaguzi wa sifa ya Uminimalisti. Hitimisho na mapendekezo vilevile yameshughulikiwa katika sura hii.

6.1 Muhtasari wa Matokeo

Kwa muhtasari, hapa tutaonyesha matokeo ya utafiti kwa kuonyesha vipi malengo ya utafiti yaliweza kuafikiwa.

Lahaja ya Kitikuu ina matumizi ya viambishi /mofimu za njeo, hali na dhamira katika vitenzi vyake. Kwa upande wa njeo Kitikuu kinatumia njeo mbili kuu, ambazo ni njeo za kuonyesha wakati uliopita na ujao. Kwa kiwango kidogo, Kitikuu hutumia njeo iliyopo ya {a}, na inakuwa si dhahiri kwani mara nyingi huwa inadondoshwa katika umbo la fonolojia, ijapokuwa katika umbo mantiki huwa ipo, (Kwa nadharia ya Umilikifu na Masharti ni umbo la nje na ndani mtawalia). Kwa mfano: *Ataka kulima*; kitenzi ataka ni *a-a-tak-a : {a}* ya kwanza ni ya nafsi na {a} ya pili ni ya njeo iliyopo, lakini haidhahiriki, kwani kuna kudondoshwa kwa {a} ya kwanza katika mfanyiko wa kimofonolojia. Ikumbukwe vilevile {a} hutumika tu kwa kitenzi kisaidizi katika sentensi na sio kitenzi kikuu. Kuna wanaodai mofimu {na} ya Kiswahili Sanifu ni mofimu ya njeo iliyopo, lakini utafiti wetu unaonyesha kuwa hiyo ni hali ya kuendelea na siyo njeo. Kitikuu hakitumii mofimu {na} ya hali ya kuendelea bali hutumia mofimu {hu}, kuonyesha hali ya kuendelea badala ya {na}. Katika Kitikuu kuna kuingiliana kwa mofimu ya {hu}, kama hali ya kuendelea na hali ya mazoea.

Njeo mbili kuu zinazotumika zaidi ni: kwanza, njeo iliyopita, Kitikuu kama Kiswahili Sanifu hutumia mofimu {li} na pili ni njeo ijayo, Kitikuu hutumia mofimu {ta}, kama ya Kiswahili Sanifu, lakini, /t/ ya Kitikuu ni ya kutamkiwa menoni na ya Kiswahili Sanifu ni ya ufizi. Njeo iliyopita hutumika kwa tendo ambalo limetendeka kabla ya usemi na huonyeshwa kwa mofimu {li} na katika ukarusha mofimu {li} hubadilika na kuchukua mofimu {ku}: *Alipika chakula. Kan. Hakupika chakula.*

Kwa upande wa njeo ijayo, tendo hutendeka baada ya usemi. Mofimu {ta} ndiyo inayotumika kuonyesha ni baada ya usemi. Ukarusha wa njeo ijayo, Kitikuu hudondosha mofimu ya njeo {ta} na kuishia na mofimu kanushi ya {i}. Tofauti na Kiswahili Sanifu ambapo mofimu ya njeo iliyopo {ta} hubakishwa na kitenzi kinaishia na mofimu {a} na siyo {i} kama katika Kitikuu. Mfano: *Mwidhi atafungwa miaka mivili. Kan. Mwidhi haOfungwi* miaka mivili. (Mwizi atafungwa miaka miwili. Kan. Mwizi *hatafungwa* miaka miwili).

Hali ni sehemu ya pili muhimu ya kazi hii. Hali huonyesha wakati wa tendo bila kurejelea wakati wa usemi. Kama anavyodai Lyons (1969) kuwa, njeo ni kategoria ya usonde ambapo hali si ya usonde. Usonde hapa kumaanisha kurejelea wakati wa usemi ambaa ni sasa. Kitikuu, kama lugha nyinginezo hugawanya hali katika hali timilifu na isiyo timilifu. Hali timilifu katika Kitikuu zipo za aina mbili: hali timilifu ya mofimu {ndo} na {ie}. Mofimu {ndo} huonyesha tendo limekamilika muda mfupi uliopita. Mofimu {ie} huonyesha tendo limefanyika na kukamilika muda mrefu zaidi ukilinganishwa na –ndo-, lakini ya siku hiyo hiyo. Zote ni hali timilifu kwa sababu tendo limefanyika na kukamilika kwani matokeo yake bado yanaonekana.

Hali ya pili ni hali ya mazoea. Hali ya mazoea huonyesha hali ya kuendelea kwa muda mrefu, au muda wote hata imekuwa ni hali ya kawa, kufanyika kwa tendo hilo. Kitikuu kama Kiswahili Sanifu hutumia mofimu {hu} kama hali ya mazoea. Ikumbukwe

hana kuwa, Kitikuu vilevile hutumia mofimu {hu} kwa hali ya kuendelea, sawia na mofimu {na} kwa Kiswahili Sanifu. Kwa hivyo Kitikuu hutumia kiambishi **hu-** cha hali, kama hali ya mazoea na hali ya kuendelea. Kazi hii inaangalia mofimu {hu} ya hali ya kuendelea kama hali na siyo njeo kama wanavyodai wataalam wengine, kuwa mofimu {na} ya Kiswahili Sanifu ni ya njeo iliyopo. Mfano: *Amina hunwa madhiva.* (Amina anakunywa maziwa). *Paka hula nama.* (Paka **hula** nyama). Kitikuu pia huonyesha hali ya kuendelea kwa kutumia mofimu {o} ya kiishio kwa baadhi ya vitenzi vyake. Vitenzi viwili tu, huweza kutumika kwa Kitikuu kuonyesha hali ya kuendelea, sawia na mofimu {na} ya Kiswahili Sanifu. Vitenzi hivyo ni *kuya {y}* na *endra{endr}* yaani, kuja na kwenda. Mfano: *Ntonyi uya na isi.* (Mvuvi **anakuja** na samaki). *Nendrao kununua sukari na mayani a chai.* (Ninaenda kununua sukari na majani ya chai).

Kitikuu hutumia hali ya mfululizo, kwa kutumia mofimu {ka}. Hali ya mfululizo huonyesha kuwa kuna mfuatano wa vitenzi, yaani zaidi ya kimoja. Kitenzi cha kwanza hutumia mofimu za njeo au hali na vitenzi vinavyofuata hutumia hali ya **-ka-**. Mfano: *Nalikwendra dukani kanunua ntee, kundre, munu, nlonje, na dhichunguu, karudi kapika vana vakala.* (Nilikwenda dukani nikanunua mchele, kunde, nyanya na vitunguu, nikarudi nikapika watoto wakala). Kwa vitenzi vyenye kubeba mofimu {ka} ya mfululizo, Kitikuu hudondosha mofimu ya nafsi, kwani tayari mofimu hiyo ipo katika kitenzi cha kwanza kwa hivyo haina haja ya kurudia, tofauti na Kiswahili Sanifu.

Dhamira ni sehemu ya tatu muhimu iliyoshughulikiwa katika kazi hii. Kitikuu kina dhamira nne. Dhamira ya kwanza ni dhamira arifu, ambayo huhusika na maelezo ya kweli au dhahiri. Hutoa maelezo juu ya jambo fulani. Dhamira arifu hutumia mofimu {a} kama kiishio katika vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Mfano: *Amina alikula wali na isi.* (Amina alikula wali na samaki). Dhamira ya pili ni dhamira ulizi. Hapa maswali huulizwa na tunatarajia kupata jibu au tendo kufanyika. Dhamira ulizi

hutumia mofimu {a} ya kiishio kama dhamira arifu, kwa vitenzi vyenye asili ya Kibantu.

Mfano: *Vanafundi vatakwenda safari kesho?* (Je, Wanafunzi watakwenda safari kesho?). Kwa vitenzi vyta kigeni hutegemea mwisho wa kitenzi hicho na huweza kubadilika, ikawa e, a, i, au u. Mfano: *Mwalimu atasahau kadhi alochupa?* (Je, mwalimu atasahau kazi alotupatia?).

Dhamira aina ya tatu ni dhamira agizi. Dhamira agizi hugawanywa mara mbili; kama dhamira agizi ya amri, ambayo huhusika na kutoa amri, na dhamira agizi isiyo ya amri inayohusika na kutoa pendekezo au maoni. Dhamira agizi ya amri huchukua mofimu {a} kama kiishio katika hali ya umoja, na kwa wingi huchukua kiishio {ani}. Dhamira agizi ya amri kwa sababu huhusika na kutoa amri basi humalizia na alama ya mshtuo. Mfano: *Imba! Imbani!* (Imba!- Imbeni!). Kwa upande wa vitenzi vyta silabi moja, Kitikuu huchukua mfumo tofauti na Kiswahili Sanifu. Kitikuu huanza na mofimu {i} kuonyesha dhamira agizi ya amri, katika umoja na wingi. Mfano: *Ila! –Ilani!* (Kula! - Kuleni!), Inwa!- Inwani! (Kunywa!- Kunyweni!). Kwa upande wa dhamira agizi isiyo ya amri, hufanya kazi kama dhamira tegemezi, ya kuonyesha upole, kutoa pendekezo au ombi. Dhamira hii hutumika kwa nafsi ya pili, umoja na wingi. Mofimu inayotumiwa ni mofimu {e} mwishoni mwa kitenzi. Mifano: *Usome kwa bidii - Musome kwa bidii. Upike chakula cha usiku. – Mupike chakula cha usiku.* Dhamira hii huweza kutumiwa pamoja na neno ‘tafadhalii’, Mfano: *Tafadhali enendra sipichali eo - Tafadhali enendrani sipichali eo.* (Tafadhali nenda hospitali leo.- Tafadhali nendeni hospitali leo).

Dhamira ya nne ni dhamira tegemezi. Dhamira tegemezi ni aina inayoonyesha matumainio, matarajio ambayo mara nyingi hayapatikani. Ni dhamira pia inayotoa maombi, mapendekezo, masharti na makisio ambayo ni kinyume na uhakika. Mofimu mbalimbali hutumika katika dhamira hii. Hutumika kama dhamira isiyo ya amri kwa kutumia mofimu {e}. Mfano: *Mpeke mwana kwa dakitari.* (Mpeleke mtoto kwa

daktari). Dhamira tegemezi hutumika kuonyesha masharti, Kitikuu hutumia mofimu *{ki}* na *{ngali}*. Mifano: *Ukipicha ntihani takununulia dhawadi.* (Ukipita mtihani nitakununulia zawadi). *Ningalikuva tajiri ningalijenga ijumba ikuru.* (Ninge kuwa tajiri ningejenga jumba kubwa).

Mofimu za njeo, hali na dhamira huweza kutumiwa katika sentensi kwa pamoja katika sentensi zenyenye kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Muingiliano huo huonyesha mofimu za njeo huweza kuingiliana na za hali na pia za dhamira, vilevile za hali kuingiliana na za njeo na dhamira. Lakini ikumbukwe kwamba sio njeo zote zinaweza kuingiliana na mofimu za hali na dhamira zote, huwa kuna baadhi tu ambazo zinaweza kutumika kwa pamoja.

Kazi hii imeonyesha kuwa, kwa vile Kitikuu ni lugha ambishi-bainishi, basi imeweza kufanya kazi vizuri sana kupitia mtazamo wa Uminimalisti, chini ya ukaguzi wa sifa. Mofimu za njeo, hali na dhamira zinasogezwa na kukaguliwa katika hatua mbalimbali ili kudhihirisha ukubaliano wa kisarufi.

6.2 Hitimisho

Kazi hii ya utafiti imechanganua mofosintaksia ya njeo, hali na dhamira kwa mkabala wa Uminimalisti, chini ya ukaguzi wa sifa katika Kitikuu. Kitenzi cha Kitikuu kinaambishwa mofimu za njeo, hali na dhamira ambazo zinasogezwa na kukaguliwa katika hatua mbalimbali kubaini usarufi wa sentensi. Maneno ambayo hayana sifa za kimofolojia huwa hayasogezwi kwa sababu ya kukosa sifa za kimofolojia zinazosababisha usogezi na ukaguzi.

Kitikuu, kama tulivyoona kina njeo mbili kuu, njeo iliyopita na njeo ijayo. Njeo iliyopita hutumia mofimu {**li**} na njeo ijayo hutumia mofimu {**ta**} kama katika Kiswahili Sanifu. Kwa upande wa hali, Kitikuu hutumia hali nyingi kuliko njeo. Kitikuu kinagawanya hali mara mbili: timilifu na isiyotimilifu. Katika hali timilifu Kitikuu kinatumia mofimu mbili kuu {**ndo**} na {**ie**}. Hii ni tofauti kabisa na Kiswahili Sanifu ambapo tuna mofimu {me} tu ya hali timilifu. Kitikuu kinatofautisha hali timilifu ya hivi karibuni {**ndo**} na ya muda mrefu kidogo lakini ya siku hiyo hiyo {**ie**}.

Kwa upande wa aina ya hali zisotimilifu, kuna hali ya kuendelea, hali ya mazoea na hali ya mfululizo. Kitikuu hutumia mofimu {**hu**} kwa maana mbili, tofauti na Kiswahili Sanifu ambayo ni ya mazoea tu; Mofimu {**hu**} ina maana ya hali ya mazoea na hali ya kuendelea kulingana na inavyotumika katika sentensi. Kitikuu hakina mofimu {**na**} kama Kiswahili Sanifu ya hali ya kuendelea bali hutumia mofimu {**hu**}. Kwa mfano: *Mwana hula wali*; kwa maana, Mtoto anakula wali; kuonyesha anakula sasa na anaendelea kula na sio mazoea. Mbali na mofimu ya mazoea {**hu**}, Kitikuu pia hutumia mofimu {**ki**} ambayo husimamia hali ya mazoea, kama Kiswahili Sanifu. Hapa huwa kuna mwingiliano; mofimu {**hu**} hutumika kwa hali hizo mbili tofauti, yaani hali ya kuendelea na hali ya mazoea. Vilevile mofimu {**ki**} hutumika kwa hali ya mazoea na dhamira ya masharti.

Kitikuu pia hutumia hali ya mfululizo ya mofimu {**ka**} kama Kiswahili Sanifu. Hata hivyo, Kitikuu mara nyingi kinapotumia mofimu hii ya {**ka**} pamoja na mofimu za kiima {**a**} na {**na**}, basi huweza kudondosha mofimu za kiima {**a**} na {**na**}; na sauti k'ikatolewa kwa mpumuo. Mfano: *Mwana k'aya, k'ala, k'atedha kisha k'aiyala*. (Mtoto akaja, akala, akacheza kisha akalala). Imi k'aya, k'ala, k'atedha kisha k'aiyala. (Mimi nikaja, nikala, nikacheza kisha nikalala).

Kwa mintarafu hiyo basi, ndiyo tukasema Kitikuu kina msikiko zaidi kwa upande wa hali ikilinganishwa na njeo na dhamira. Kwa sbababu Kitikuu hutumia hali zaidi kuliko njeo na dhamira na ndiyo hata mofimu za hali ni nyingi zaidi zikilinganishwa na njeo na dhamira. Tofauti na Kiswahili Sanifu, kama anavyodai Rieger (2011) kuwa Kiswahili Sanifu kina msikiko zaidi wa njeo kuliko hali na dhamira. Kutokana na utafiti huu ni dhahiri kuwa lahaja ya Kitikuu ina msikiko zaidi wa hali kulingana na migao ya kiwango cha matumizi ya kisarufi anayotupatia Bhat (1999) kuliko njeo na dhamira. Bhat anadai kuwa lugha huwa ina msikiko zaidi wa njeo, hali au dhamira kulingana na migao na matumizi yake ya kisarufi. Ndiyo nikaonelea kuwa Kitikuu kina msikiko zaidi wa hali kuliko njeo na dhamira.

Kwa upande wa dhamira, mara nyingi ni mofimu za viishio zinazohusika, japo pia kuna dhamira za masharti zinazotumia mofimu **{ki}** na **{ngali}**. Kitikuu kama Kiswahili Sanifu hutumia mofimu **{a}** kwa dhamira arifu na **{e}** kwa dhamira agizi na tegemezi. Tofauti na Kiswahili Sanifu, dhamira agizi katika umoja, Kiswahili Sanifu hutumia mofimu **{ku}** kwa vitenzi vya silabi moja, Kitikuu hakitumii mofimu **{ku}** bali hutumia mofimu **{i}** mwanzoni; mfano, Kula! Kufa! Kunywa! ; Kitikuu: *Ila! Ifa! Inwa!*. Kitikuu hutumia dhamira ya masharti kwa kutumia mofimu **{ki}** na **{ngali}**. Kitikuu tofauti na Kiswahili Sanifu hakitumii **{nge}** na **{ngeli}** ya masharti bali hutumia mofimu **{ngali}** pekee kuonyesha masharti.

Mwisho, mwingiliano wa njeo, hali na dhamira umeonyeshwa katika sentensi ambatano, yaani ni vipi mofimu hizi huingiliana katika sentensi ambatano na ni wapi haziwezi kupatikana kwa pamoja katika lahaja ya Kitikuu.

Kazi hii kwa kiasi kikubwa imeweza kuonyesha tofauti za njeo, hali na dhamira na mofimu zake mbalimbali, ndiyo zisiende zikichanganywa changanywa kama kazi za

awali zilivyofanya. Vilevile utafiti huu umweza kuonyesha matumizi ya nadharia ya Uminimalisti inavyofanya kazi, hasa kwa mfano wa lugha imara zenye ukwasi wa mofolojia, kama Kitikuu.

6.3 Mapendekezo

Kazi hii imetoa mchango mkubwa kwanza, kwa vipashio vyta kisarufi vya njeo, hali na dhamira ili viweze kufahamika na vitumiwe ipasavyo. Dhana hizi zimetumiwa kwa njia inayokanganya na baadhi ya waandishi, kwa hivyo tumejaribu kutoa mwanga ili ziweze kueleweka na kutumiwa ipasavyo.

Kwa upande wa pili, kazi hii ni kielelezo cha kufuatwa hasa kwa wanafunzi wa uzamili na uzamifu wa lugha ya Kiswahili, wanaotaka kutumia nadharia ya Uminimalisti. Utafiti huu ni uchanganuzi wa kimofosintaksia wa njeo, hali na dhamira chini ya nadharia ya Uminimalisti ya kanuni ya ukaguzi wa sifa. Kanuni hii inafanya kazi vyema katika lahaja ya Kitikuu, ambayo ni lugha ambishi bainishi. Kwa mintarafu hiyo basi, mofimu za njeo, hali na dhamira zinakuwa na vichwa vyake na husogezwa na kukaguliwa katika hatua mbalimbali ili ziweze kuonyesha usarufi wake katika sentensi, na hakuna kuacha au kuongeza chochote, kama inavyotetewa na kanuni ya iktisadi.

Kitikuu hutumia baadhi za mofimu za njeo, hali na dhamira tofauti na za Kiswahili sanifu. Kuna haja ya tafiti nyingine za lahaja kufanywa kuona kama kuna tofauti za mofimu hizo au la. Kazi za lahaja ni muhimu na kuna umuhimu kwa lahaja hizi mbalimbali za Kiswahili kufanyiwa utafiti wa kina kiisimu. Kazi hii imeangazia tu lahaja ya Kitikuu na nadharia ya Uminimalisti ambayo imefanya kazi vizuri sana kwa lahaja hii. Kuna haja ya kufanya tafiti lahaja nyingine za Kiswahili kwa misingi ya kimofosintaksia, hasa Uminimalisti kuona kama inatenda kazi kwa namna gani.

Japo lahaja sanifu ya Kiswahili imeshughulikiwa kwa kiwango fulani, kuna umuhimu kuifanya uchunguzi wa kinadharia kama Uminimalisti na kwa nadharia ya karibu zaidi ambayo ilasisiwa na Chomsky mwaka wa 2000, Unyambuzi kwa hatua (Derivation by Phase) zitumike kuchanganulia kazi hizo.

Mwisho napendekeza mbali na njeo, hali na dhamira mofu nyinginezo katika vitenzi ziweze kuchanganuliwa kwa kutumia nadharia hizo na kuhusisha sentensi changamano, kwani kazi yangu imeangazia sentensi sahili na ambatano zaidi. Kazi za lahaja za Kiswahili mbalimbali zichanganuliwe kiisimu kupitia nadharia anuwai za kiisimu, Uminimalisti ikiwa ni mojawapo.

MAREJELEO

- Ashton, E. (1944). *Swahili Grammar*. Harlow: Longman Group.
- Baker, M. (1988). *Incorporation: A theory of Grammatical Function Changing*. Chicago: The University of Chicago Press.
- Bakari, M. (1982). The Morphophonology of the Kenyan Swahili Dialect. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Beaudoin-Lietz, C. (1999). Formatives of Tense , Aspect, Mood and Negation in the Verbal Construction of Standard Swahili. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Memorial Newfoundland.(Haijachapishwa).
- Besha, R. (1989). *A Study of Tense and Aspect in Shambala*. Berlin: Dietrich Reimer.
- Bybee, J. , Revere, P. & William, P.(1999). *The Evolution of Grammar: Tense, Aspect and Modality in the Languages of the World*. Chicago: University of Chicago Press.
- Bybee, J. & Dahl, O. (1989). 'The Creation of Tense and Aspect in the Languages of the World'. In *The Studies in Language Journal*. Amsterdam and Philadelphia: John Benjamins Publishing Company. Vol.13 pp 51-103.
- Chiraghdin, S. & Mnyapala, M.(1997). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press
- Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, Mass: MIT Press

Chomsky, N. (1993). ‘The Minimalist Program for Linguistic Theory’ In occasional paper in Linguistic in Hale, K. & Keyser, S (eds). *The view from Building 20 Essays in Linguistics in Honor of Syirain Bromberger*. Cambridge, Mass: MIT Press.

Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program*. Cambridge, Mass: The MIT press.

Comrie, B. (1976). *Aspect: An Introduction to the Study of Verbal Aspect and Related Problems*. Cambridge: Cambridge University Press.

Comrie, B. (1985). *Tense*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cook, V. & Newson, M. (1996). *Chomsky's Universal Grammar: An Introduction*. Oxford : Blackwell.

Crystal, D. (1991). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics 3rd Ed*. Oxford: Basil Blackwell.

Dahl, O. (1985). *Tense and Aspect Systems*. Oxford: Basil Blackwell.

Der Houssikian, H. (1969). Noun class and Concords in Kimombasa. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Texas. (Haijachapishwa).

Guthrie, M. (1948). *The Classification of Bantu languages*. Gregg: Oxford.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Haegeman, L. (1994). *Introduction to Government and Binding Theory. 2nd ed*. Oxford: Blackwell.

- Hillewaert, S. (2011). ‘The Ideological Motivations for Language Change: The Loss of Dialectical Variation and Identity among the Swahili Speaking People of the Kenya Coast’. In Chimera, R.(ed). *Kiswahili Research and Development in Eastern Africa*. Mombasa: Jor’s Publishers. Vol.1. pp 131-153.
- Hornstein, N. Nunes, J. & Grohmann, K. (2005). *Understanding Minimalism*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Horrocks, G. (1987). *Generative Grammar*. London: Longman.
- Jerono, P. (2012). Tugen Word Order : A Minimalist Approach. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Lindfors, A. (2003). Tense and Aspect in Swahili. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Uppsala. (Haijachapishwa).
- Lyons, J. (1968). *Introduction to Theoretical Linguistics*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Marantz, A. (1995). *Government and Binding Theory and the Minimalist Program: Principles and Parameters in Syntactic Theory*. Blackwell: Oxford Gert Webelhuth.
- Massamba, D. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lughha*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Mdee, J. (1986). *Kiswahili Muundo na Matumizi yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers.
- Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

- Mohamed, M. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi : East African Educational Publishers.
- Mohlig, W. (1985). *Swahili -Dialekte*. In Miehe, G. & Mohlig, W. (1995). *Swahili – Handbuch*. Cologne: Rudiger Koppe. pp 41-62.
- Mukwana, A. & Obuchi, S. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Myachina, E. (1981). *The Swahili Language : A Descriptive Grammar*. London : Oxford University Press.
- Nzioka, A. (2007). A Minimalist Analysis of Kikamba Tense and Aspect. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Nurse, D. (1982). ‘The Swahili Dialects of Somalia and the Northern Kenya Coast’. In *Etudes sur le Bantu Oriental*, ed. M-F Rombi. Paris: SELAF. pp. 73-146.
- Nurse, D. (1994). ‘Historical Texts from the Swahili Coast.’ In *Swahili Forum 1*. Institut fur Afrikanistik. Cologne: Universitat zu Koln. 50923.
- Nurse, D. & Hinnebusch, T. (1993). *Swahili and Sabaki. A linguistic History*. London: University of California Publishers.
- Nurse, D. & Muzale, H. (1999). ‘Tense and Aspect in Great Lakes Bantu Languages’. In Hombert, J. & Hyman, M. (Eds.) *Bantu Historical Linguistics: Theoretical and Empirical Perspectives*. Stanford, California: Centre for the Study of Language and Information Publications. pp. 515-544.
- Ochola, E. (2003). A Morpho-syntactic Analysis of Dholuo Verb System. Tasnifu ya Uzamili : Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

- Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington D.C.: Centre for Applied Linguistics.
- Radford, A. (1997a). *Syntactic Theory and the Structure of English: A Minimalist Approach*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Radford, A. (1997b). *Syntax: A Minimalist Introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Reichenbach, H. (1947). *Elements of Symbolic Logic*. New York: Macmillan.
- Schroeder, H. (2008). *Word Order in Toposa: An Aspect of Multiple Feature-Checking*. Sil: Sil International.
- Stigand, C. (1915). *A Grammar of Dialectic Changes in the Kiswahili Language*. London: Cambridge University Press.
- Swaleh, R. (2005). Mofosintaksia ya Kishazi cha Kitikuu: Mtazamo wa Uminimalisti. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Vitale, A. (1981). *Swahili Syntax*. Dordrecht-Holland/Cinnamison, USA: Foris Publications.
- Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Kampala: Longman Publishers Ltd.
- Walker, J. (2013). Comparative Tense and Aspect in the Mara Bantu Languages: Towards a Linguistic History. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Trinity Western. (Haijachapishwa).

KIAMBATISHO A**IDHINI YA KIMAADILI YA KUFANYA UTAFITI**

Anwani: Njeo, Hali na Dhamira katika Kitenzi cha Kitikuu: Nadharia ya Uminimalisti
UTANGULIZI

Madhumuni ya waraka huu ni kukualika na kukunasihi kushiriki na kuchangia katika utafiti kuhusu mada ya njeo, hali na dhamira katika lahaja ya Kitikuu. Bi. Rukiya H. Swaleh ni mwanafunzi wa Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Pwani Idara ya Isimu, Lugha na Fasihi na ndiye atakayeendesha utafiti huu.

Mshiriki anapokubali kuchangia katika utafiti huu atahitajika kujaza hojaji atakazopewa na kama ana shida ya kusoma na kuandika basi atasomewa sentensi naye atatoa kisawe chake katika lahaja ya Kitikuu. Mshiriki ana uhuru wa kutojijulisha jina lake lakini ni muhimu kutujulisha umri wake. Washiriki hawatalazimishwa kushiriki katika utafiti huu bali ni wale waliokubali kwa hiari yao.

Tunawakikishia watakaoshiriki katika zoezi hili kuwa habari zote zitakazopatikana kutoka kwao zitahifadhiwa vyema na zitatumika katika kazi hii pekee.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na mtafiti:

Bi. Rukiya Harith Swaleh

Nambari ya simu: 0721432510

Barua pepe: rukiya2harith@yahoo.com

KIAMBATISHO B: Hojaji 1**JINA :** (SIO LAZIMA): -----**MIAKA:** -----

TAFADHALI TAFSIRI KWA KITIKUU SENTENSI ZIFUATAZO NA KISHA UKANUSHE SENTENSI HIZO.

1. Mtoto huyu mzuri anapenda kulia sana.

Mwana huu ndhuri hupenda kulia sana.

Mwana huu ndhuri hapendi kulia sana

2. Mzee ameenda sokoni kununua mchele.

Ndhee ndokwendra sokoni kununua ntee.Ndhee wendee sokoni kununua ntee.

Ndhee hayendra sokoni kununua ntee.

3. Fatuma alicheza sana jana.

Fatuma alitedha sana yana.

Fatuma hakutedha sana yana.

4. Mtoto alinunua peremende jana.

Mwana alinunua paramandi yana.

Mwana hakununua paramandi yana

5. Amina huja hapa mara kwa mara.

Amina huya hapa mara kwa mara.

Amina hayi hapa mara kwa mara.

6. Nitakuja na Amina kesho.

Nitakuya na Amina kesho.

Siyi na Amina kesho.

7. Mbuzi wala manyasi ya kijani.

Mbudhi hula magugu a kijani.

Mbudhi hali magugu a kijani.

8. Dada anasema kuwa anataka mchele wa pishori.

Dada hunena kuva wataka ntee wa pishori.

Dada haneni kuva wataka ntee wa pishori.

9. Ali anataka kuimba wimbo wa taifa.

Alii wataka kuimba wimbo wa taifa.

Alii hataki kuimba wimbo wa taifa.

10. Nimekwisha kula chakula.

Nindokwisha kula chakula.

Siyesha kula chakula.

11. Fathiya ataimba wimbo wa taifa.

Fatihiya taimba wimbo wa taifa.

Fatihiya haimbi wimbo wa taifa.

12. Juma atakuwa yuenda sokoni.

Jumaa takuva wendrao sokoni.

Jumaa havi wendrao sokoni.

13. Twende shamba tukalime mahindi.

Twenendre hondreni chukalime nchama.

Twenendre hondreni chukalime nchama.

14. Akipita mtihani nitamnunulia zawadi nzuri.

Akipicha ntihani tan'nunulia dhawadi nduri.

Akipicha ntihani sin'nunulii dhawadi nduri.

15. Angekuwa raisi angejenga jumba kubwa.

Angalikuva raisi angalijenga ijumba ikuru.

Angalikuva raisi hangalijenga ijumba ikuru.

16. Akifika mapema mwambie anione.

Akisikilia mapema mwambie anivone.

Akisikilia mapema mwambie asinivone.

17. Angaliimba tarabu angalipata pesa nyngi.

Angaliimba tarabu angalipacha senti ningi.

Angaliimba tarabu hangalipacha senti ningi.

18. Hamisi amekuja akaoga, akala, akalala.

Hamisi ndokuya, kakoa, kala, kaiyala.

Hamisi hayaya kukoa,kula na kuiyala.

19. John anasaidia sana maskini.

Joni husaidia sana masikini.

Joni hasaidii sana masikini.

20. Je, Amina atafika leo?

Amina tasikilia eo.?

Amina hasikili eo?

21. Mungu amuveke mahali pema.

Mungu amveke mahali pema.

Mungu asimveke mahali pema.

22. Mungu atupe mazuri daima.

Mungu achupe madhuri daima.

Mungu asichupe madhuri daima.

23. Ule chakula chote!

Ule chakula chote!

Hakula chakula chote!

24. Mpeleke mtoto hospitali!

Mpeke mwana sipichali!

Usimpeke mwana sipichali!

25. Mwachie chakula chote.

Mwatie chakula chote.

Usimwatie chakula chote.

KIAMBATISHO C : Hojaji 2**TAFADHALI TAFSIRI SENTENSI ZIFUATAZO KWA KITIKUU.****JINA (SIO LAZIMA) ----- MIAKA:-----****TAFSIRI SENTENSI HIZI KISHA UKANUSHE KWA KITIKUU.**

1. Nilikuwa nataka kuja kwako kesho.

Nalikuva nataka kuya kwako kesho.

Sikuva nataka kuya kwako kesho.

2. Atakuwa anaimba kesho saa saba za mchana.

Takuva huimba kesho saa sabaa dha ntana.

Havi huimba kesho saa sabaa dha ntana.

3. Ameambiwa kuimba wimbo wa taifa.

Ndoambiwa kuimba wimbo wa taifa.

Hayaambiwa kuimba wimbo wa taifa.

4. Atakuwa akicheza wakati kama huu.

Takuva akitedha wakati kama huu.

Takuva hatedhi wakati kama huu.

5. Alikuwa huimba saa kama hizi.

Alikuva huimba saa kama hidhi.

Alikuva haimbi wakati kama huu.

6. Nilikuwa nala chakula.

Nalikuva hula chakula.

Sikuva hula chakula.

7. Nilikuwa hunywa maji alipowasili.

Nalikuva hunwa mayi aliposikilia.

Sikuva hunwa mayi aliposikilia.

8. Akija niletee kalamu yangu.

Akiya nechea kalamu angu.

Akiya sinechee kalamu angu.

9. Ningekuwa tajiri ningejenga jumba kubwa.

Ningalikuva tajiri nigalijenga ijumba ikuru.

Ningalikuva tajiri singalijenga ijumba ikuru.

10. Utakuwa umemaliza ikifika saa nane.

Takuva ndomalidha ikisikilia saa nane.

Takuva huyamalidha ikisikilia saa nane.

11. Itakuwa imefika ikifika jioni.

Itakuva imesikilia ikisikilia iyoni.

Itakuva haiyasikilia ikisikilia iyoni.

12. Juma alikuwa anakwenda sokoni.

Jumaa alikuva endrao sokoni.

Jumaa alikuva hendri sokoni.

13. Nilikwenda sokoni nikanunua maembe nikala, nikampa pesa.

Nalikwendra sokoni kanunua mahembe kala, kampa senti.

Sikwendra sokoni kanunua mahembe kala, kampa senti.